Nipashe
Jumanne Machi 12, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0579863
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper



## Wananchi washikwa butwaa mwanafunzi kutapika mawe

UKURASA 12




UKURASA 13

RIPOTI MAALUM

# Kiini mauaji watoto, wanawake bayana

**WANASIASA** watajwa, wazazi wadaiwa kutoa kafara watoto ili kupata utajiri, mazao mengi... *Endelea ukurasa wa 2*



## Shehena ya samaki wenye sumu yanaswa

UKURASA 2

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina (kushoto), akijadiliana jambo na Mkurugenzi Msaidizi wa Ulinzi na Rasilimali za Uvuvi, Nchama Marwa, kabla ya kuteketeza shehena ya samaki aina ya sato waliokamatwa wakiwa wameingizwa nchini kutoka China kinyume cha sheria, katika dampo la Pugu Kinyamwezi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### CUF WASHANGAA UKIMYA WA POLISI, MSAJILI VYAMA



CHAMA cha Wananchi (CUF) upande unaomuunga mkono Katibu Mkuu wa chama hicho, Maalim Seif Sharif Hamad, umedai kushangazwa na kutojibiwa kwa barua zake...

## Zitto ategwa kutofika kortini

UKURASA 3

TAIFA STARS VS UGANDA
MACHI 24, 2019 • UWANJA WA TAIFA




18+ TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU
xxxxxx

RIPOTI MAALUM

# Kiini mauaji watoto, wanawake bayana

**Na Waandishi Wetu**

GABRIEL Ruhumbika katika kitabu chake cha Janga Sugu la Wazawa (1985), anatahadharisha kwamba ikiwa hatua stahiki hazitachukuliwa, kitafika kipindi ambacho mtu akitaka kuwa mwanasiasa au mfanyabiashara mkubwa, ataua na kupeleka kwa mganga wa kienyeji kiungo cha binadamu.

Ruhumbika anamtumia mhusika mkuu Bugonoka Ninalwo 'Nseko' kuwakilisha kundi la wazee na watu wasio na hatia wanaouawa kikatili, kisha kunyofolewa viungo vyao kutokana na imani potofu za kishirikiana.

Mwandishi wa riwaya hiyo pia anamtumia mhusika mkuu msaidizi Padri Sheikh Issa 'Profesa Simbambiti' kuwakilisha kundi la viongozi wa dini na waganga wa kienyeji wanaotumia vibaya nafasi zao, kufanya ukatili wa kijinsia na mauaji dhidi ya wazee kwa imani za kishirikina na kutafuta utajiri.

Mtazamo huo wa kidhanifu wa Ruhumbika alioubuni miaka 34 iliyopita, sasa umekuwa ukweli wa kitaaluma unaoungwa mkono na wataalamu wa ustawi wa jamii wanaoyahusisha na imani za kishirikiana, matukio ya hivi karibuni ya mauaji dhidi ya watoto wa wanawake nchini.

Karne iliyopita, matukio ya mauaji dhidi ya wazee yalikuwa yanaripotiwa kwa wingi katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, hasa Mkoa wa Shinyanga, lakini sasa matukio ya mauaji dhidi ya kundi hilo yanaripotiwa karibu mikoa yote ya Tanzania Bara.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inabainisha kwamba, katika kipindi kilichoanzia Julai 2017 hadi Machi mwaka huu, wazee 117 waliuawa nchini, sawa na mauaji ya wazee 13 kila mwezi.

Mei 3, mwaka jana, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Dk. Mwigulu Nchemba, aliwasilisha bungeni jijini Dodoma makadirio ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/19 na kusema kuwa, kati ya wazee hao 117 waliouawa, 91 ni wanaume (asilimia 77.8).

Alisema matukio hayo yaliripotiwa kwa Jeshi la Polisi katika mikoa ya Arusha, Mbeya, Dodoma, Geita, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Njombe, Mara, Songwe, Shinyanga, Mwanza, Morogoro, Singida, Simiyu na Tabora.

Dk. Mwigulu alifafanua kuwa katika kipindi hicho cha miezi tisa, mkoani Arusha waliuawa wazee sita, Dodoma (1), Geita (9), Iringa (1), Kagera (10), Katavi (3), Kigoma (1), Mara (2), Mbeya (7), Morogoro (2), Mwanza (9), Njombe (5), Rukwa (10), Shinyanga (3), Simiyu (5), Singida (6), Songwe (12) na Tabora (25). Kiongozi huyo wa serikali aliliahidi Bunge kuwa Jeshi la Polisi litaendelea kudhibiti na kuzuia mauaji ya wazee, huku likishirikiana na wadau kutoa elimu kwa umma ili kuacha mila na imani potofu.

Wakati serikali ikikabiliana na mauaji dhidi ya wazee, mwanzoni mwa mwaka huu, kuliripotiwa matukio ya mauaji dhidi ya watoto na wanawake katika mikoa ya Njombe, Simiyu na Arusha.

Januari 27, mwaka huu, yaliripotiwa matukio ya mauaji ya watoto 10 mkoani Njombe yakihusishwa na imani za kishirikina na kulipiza kisasi.

Watoto hao walichinjwa, kisha kunyofolewa sehemu za siri, masikio na ulimi. Kati yao, wanne ni wa Halmashauri ya Njombe na sita ni wa Halmashauri ya Mji wa Njombe mkoani Njombe.

Siku chache baadaye, watoto watatu wa kike waliripotiwa kuuawa na kunyofolewa viungo vyao na watu wasiojulikana katika Mji wa Lamadi wilayani Busega mkoani Simiyu.

Pia, kwa takribani miezi mitatu kuanzia mwishoni mwa mwaka jana hadi Februari mwaka huu, wanawake tisa waliuawa Mto wa Mbu wilayani Monduli mkoani Arusha.

Kutokana na mauaji hayo Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alimwagiza Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, kuunda timu kutoka makao makuu kuchunguza matukio hayo.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, pia alilaani mauaji hayo na kuvitaka vyombo vya dola kuchukua hatua dhidi ya wanaohusika.

Vilevile, Dk. Ndugulile alitoa wito kwa waganga wa tiba asili kuacha kutumia viungo na miili ya watoto kama njia ya kutatua matatizo ya wateja wao.

**KIINI CHA MAUAJI**

Mtaalamu wa Ustawi wa Jamii, Mariola Nyambuta, aliiambia Nipashe kuwa mauaji dhidi ya watoto kwa kiasi kikubwa yanatokana na imani za kishirikina.

INAENDELEA UK. 8



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Uganda, Philemon Mateke, alipowasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Entebe tayari kwa kushiriki mkutano wa Africa Now Summit 2019, utakaofanyika mjini Kampala tarehe 12 na 13 mwezi huu. **PICHA: OMR**

# Shehena samaki wenye sumu yanaswa

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imeteketeza tani 11 za samaki aina ya sato wenye thamani ya Sh. milioni 66, baada ya kubaini wana sumu na hawafai kwa matumizi ya binadamu.

Samaki hao waliotoka China wakiwa kwenye kontena lenye urefu wa futi 40 lililoingizwa nchini kwa njia zinazodaiwa za panya, walitekezwa jana Pugu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuteketezwa kwa samaki hao, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, alisema shehena hiyo ilikamatwa na baada ya kufanyiwa vipimo, samaki hao waligundulika kuwa na kiwango kikubwa cha zebaki.

"Wao (wamiliki) walipita kwa njia za panya hadi kufika hapa nchini na baadaye kulitelekeza kontena na kufikia hatua ya kupigwa mnada, ilitubidi kufanya vipimo vya ubora tukabaini kiwango cha zebaki kilikuwa PPB 690 wakati kiwango kinachoruhusiwa ni chini ya PPB 500," Mpina alisema.

Waziri huyo aliongeza: "Sumu nyingine tulizokuta ni DDT 2,4' ambayo kiwango chake kipo 19.4 wakati kinachotakiwa ni chini ya 10, na Methoxychlor imekutwa kiwango cha 19.8 ilhali kiwango kinachotakiwa ni chini ya 10."

Alisema madhara ya sumu hizo yanaonekana baada ya muda mrefu kupita na baadhi ya magonjwa ni saratani, matatizo katika mfumo wa uzazi, kuzaliwa kwa watoto wenye upungufu wa akili na kusababisha vifo.

Mpina alisema kuwa mbali na madhara hayo ya kiafya, samaki hao wanasababisha ushindani usio sawa sokoni na kwenda kupora ajira za Watanzania.

Alisema kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi ya Mwaka 2003 na kanuni zake, zinazuia mtu yeyote kuingiza bidhaa nchini bila kufuata taratibu zilizowekwa hasa mazao ya uvuvi.

Mpina alisema umuhimu wa kusimamia na kufuata sheria ni kulinda haki za walaji na afya zao, rasilimali za uvuvi za nchini zinakuwa endelevu kwa kuvuliwa kwa njia zilizo salama, kulinda ajira za Watanzania na kulinda biashara uwekezaji nchini.

Mkurugenzi Msaidizi wa Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi, Nchama Marwa, alisema usimamizi wa rasilimali za uvuvi pamoja na uvunaji wa biashara

INAENDELEA UK. 8

# CUF washangaa ukimya wa Polisi, Msajili Vyama

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Wananchi (CUF) upande unaomuunga mkono Katibu Mkuu wa chama hicho, Maalim Seif, umedai kushangazwa na kutojibiwa kwa barua zake zilizopelekwa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa pamoja na Jeshi la Polisi.

Chama hicho kimedai kuviandikia barua mamlaka hizo mbili ili vizuie kufanyika kwa mkutano mkuu wa CUF ulioandaliwa na upande wa Mwenyekiti wa chama hicho anayetambuliwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Prof. Ibrahim Lipumba.

Mkutano huo unatarajiwa kuanza kufanyika leo jijini Dar es Salaam ukiwa na ajenda mbalimbali zikiwamo za kuchagua viongozi wa ngazi mbalimbali ndani ya chama hicho kilichokumbwa na migogoro kwa miaka minne mfululizo sasa. Akizungumza na Nipashe jana, Naibu Mkurugenzi wa Habari na Mawasiliano wa CUF, Mbarala Maharagande, alidai wameshapeleka barua kwa Msajili wa Vyama vya Siasa nchini pamoja na Jeshi la Polisi, lakini mpaka sasa hakuna walichojibiwa.

"Tulishapeleka barua kwa Msajili wa Vyama vya Siasa pamoja na Jeshi la Polisi nchini, lakini mpaka sasa hatujajibiwa. Tutaamua baadaye nini cha kufanya," Maharagande alisema.

Nipashe ilimtafuta Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, kuzungumzia suala hilo, akasisitiza kuwa ni vyema kusubiri uamuzi wa mahakama kwa kuwa shauri hilo tayari liko mahakamani.

"Unajua hili suala tayari liko mahakamani, sasa ni vyema kusubiri uamuzi wa mahakama, vinginevyo ni

INAENDELEA UK. 8

# Zitto awekwa mtegoni kutofika mahakamani

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imemtaka Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe, anayekabiliwa na kesi ya uchochezi pamoja na wadhamini wake, kufika mahakamani kujieleza kwa nini hawakufika kwenye kesi jana.

Kadhalika mahakama imemwonya shahidi wa kwanza Mrakibu Msaidizi (ASP) Shamila Mkoma, kufika mahakamani hapo Aprili 9, mwaka huu, kutoa ushahidi dhidi ya mshtakiwa huyo.

Amri hiyo ilitolewa jana na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Wakili wa Serikali Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kuanza kusikilizwa ushahidi na Jamhuri imeita shahidi mmoja, ASP Mkoma. Hata hivyo, alidai kuwa mshtakiwa hayupo mahakamani.

Wakili wa utetezi, Steven Mwakibolwa, alidai kuwa amepata taarifa kutoka kwa shemeji wa mshtakiwa, Vicent Kasala, kwamba Zitto ni mgonjwa lakini hafahamu mahali alipo.

"Kasala amenieleza kwamba mkewe Zitto kampigia kumfahamisha kwamba ni mgonjwa, lakini hajui yuko wapi," alidai Mwakibolwa.

Hakimu alihoji wakili amepewa taarifa kwamba mshtakiwa ni mgonjwa lakini hana uhakika.

"Umepewa taarifa kwamba mshtakiwa anaumwa, lakini huna uhakika. Tusitafutane maneno hapa, siku ya kesi wadhamini na mshtakiwa waje hapa mahakamani kujieleza kwa nini hawakufika mahakamani," alisema Hakimu Shaidi.

Alisema kesi hiyo itaanza kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri Aprili 9, mwaka huu na shahidi afike siku hiyo.

Awali, upande wa Jamhuri ulidai kuwa unatarajia kuita mashahidi 15 na kuwasilisha vielelezo vitatu kuthibitisha kesi yao dhidi ya Zitto.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa Oktoba 28, mwaka jana, akiwa katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika katika Makao Mkuu ya ofisi za Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto alitoa maneno ya uchochezi yenye kuleta hisia ya hofu na chuki.

Ilidaiwa kuwa Zitto alinukuliwa kuwa: "Watu ambao walikuwa majeruni katika tukio la mapambano baina ya wananchi na polisi wakiwa wamekwenda

INAENDELEA UK 26



Kinamama wakichambua kunde katika Soko Kuu la Kariakoo jijini Dar es Salaam jana, ambapo kwa kila kiroba cha kilo 50 huchambua kwa 4000/-. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Azaki, taasisi binafsi zateta malengo UN

**Na Mary Geofrey**

ASASI za kiraia (Azaki) na sekta binafsi nchini, zimekutana kujadili ushiriki wake katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDG).

Mkutano huo ulifanyika jijini Dar es Salaam jana kujadili ushiriki wa sekta binafsi katika malengo hayo ili kufahamu wanakwama wapi katika utekelezaji wake, kabla Tanzania haijawasilisha ripoti yake Umoja wa Mataifa (UN) Juni mwaka huu.

Tanzania ni miongoni mwa nchi 51 zilizochaguliwa na UN kutekeleza malengo hayo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Jukwaa la Hiyari linaloshirikisha kampuni zinazofanya biashara nchini na Azaki zinazochangia utekelezaji wa malengo hayo, Simon Shayo, alisema wameandaa mkutano huo ili kuwasikia mawazo ya wadau kuhusu utekelezaji wa malengo hayo.

"Sekta binafsi inafanya shughuli za kibiashara katika maisha ya watu, hivyo tunaangalia wanashiriki kwa kiasi gani kuimarisha mazingira, kupambana na rushwa, kuheshimu haki za binadamu na kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani," Shayo alisema.

Aliongeza kuwa wameanza mkutano wa kujipima katika Mkoa wa Dar es Salaam na baadaye wataenda Arusha na Mwanza ili kushirikisha sekta binafsi kufahamu kwa kiasi gani wanawezesha utekelezaji wa malengo hayo.

Mratibu wa Jukwa la Maendeleo Endelevu Tanzania, Renald Mayeda, alisema serikali inatoa ripoti ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo mwaka huu, hivyo taasisi binafsi zimekutana kuangalia maeneo ambayo wanakwama.

Alisema kupitia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2015, utekelezaji wa malengo hayo unakwenda vizuri, lakini changamoto iliyoko ni watu kukosa uelewa wa malengo na kukosekana ushirikishwaji kutoka serikalini.

"Taasisi za kiraia ni watu, hivyo kwa sehemu kubwa malengo haya yanatekelezwa kikamilifu isipokuwa ushirikishaji na elimu haijawafikia vizuri wananchi," Mayeda alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Godfrey Simbeye, alisema lengo la mkutano huo ni kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa malengo hayo, huku akisisitiza kuwa sekta binafsi inatekeleza kikamilifu malengo Na. 4, 8, 16 na 17 kati ya malengo 17.

Alisema kazi ya sekta binafsi si tu kulipa kodi, kutoa ajira na kufanya bishara, bali pia kushiriki kwa kiasi kikubwa katika kutekeleza malengo ya milenia.

Alitaja sekta ambazo wanagusa moja kwa moja kuwa ni elimu, akieleza kuwa wameanzisha shule na vyuo binafsi maeneo yote nchini, kutengeneza kazi nzuri na kuanzisha viwanda.

Alisema lengo la kuweka mazingira safi pia wamefanikisha kwa kiasi kubwa katika maeneo mbalimbali nchini.

# Jamhuri yabanwa kesi 'Mpemba wa Magufuli'

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa utetezi katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Yusuf Ali, maarufu kama 'Mpemba wa Magufuli' na wenzake watano, umeiomba mahakama kuongeza juhudi kukamilisha upelelezi kesi ili kusonga mbele kwa kuwa ina muda mrefu.

Madai hayo yalitolewa jana na wakili Nehemia Nkoko katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba, kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa.

Mpemba na wenzake watano, wanakabiliwa na mashtaka manne ikiwamo kujihusisha na biashara haramu ya meno ya tembo yenye thamani ya Sh. milioni 785.6.

Wakili wa Serikali Candid Nasua, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kwamba Jamhuri inaomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Pia alidai kuwa kesi hiyo inaendeshwa na Wakili wa Serikali Mkuu Faraja Nchimbi na kwamba amepangiwa majukumu mengine.

Hata hivyo, Nkoko alidai kumbukumbu za mahakama zinaonyesha tangu 2017 kuwa upelelezi wa shauri hilo umekamilika, hivyo wameshangazwa kusikia upande wa Jamhuri kuwa upelelezi bado haujakamilika.

"Mheshimiwa Hakimu, tunasikitika kusikia taarifa hizi za upande wa Jamhuri zinatuchanganya, tunaiomba mahakama itumie mamlaka yake tujue hatima ya wateja wetu. Kumbukumbu zipo tangu mwaka juzi, zinaonyesha upelelezi umekamilika halafu leo hii mnatuambia eti upelelezi haujakamilika! Inashangaza sana kwetu," alidai Nkonko.

Hakimu Simba alisema Oktoba 23, mwaka jana, upande wa Jamhuri, kumbukumbu zinaonyesha, ulidai kukamilisha upelelezi hivyo aliwataka wamweleze wakili wa utetezi maelezo sahihi tarehe ijayo ya kesi.

"Kesi hii tunapata maswali sana, tunaulizwa kuna tatizo gani kwa kuwa hatutakiwi tuendelee kuwa nalo. Hii kesi ipo tangu 2016, hivyo nawaagiza mkamwambie Nchimbi ile kauli aliyoitoa imefikia wapi maana inatugombanisha na hawa washtakiwa," alisema Hakimu Simba.

Hakimu Simba alisema kesi hiyo itatajwa Februari 25, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mowc.go.tz

S.L.P. 2888,
40470 DODOMA.

04 - 03 - 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 12-03-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar -Es -Salaam** kuelekea **Singida**, gari hilo lenye namba za usajili:

**T 135 CCP / T 161 BDU**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

Urefu - mita 28
Upana - mita 3.7
Kimo - mita 5.4

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam hadi Singida Kupitia Morogoro,**

gari litasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

115098602

# Mpina azindua mkakati kuendeleza sekta ya mifugo

**Na Mwandishi Maalum**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amezindua Mpango Kambambe wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo nchini (Tanzania Livestock Master Plan-TLMP) huku akimtaka Katibu Mkuu Mifugo kuandaa mpango wa utekelezaji wa mkakati huo ndani ya siku 30 ili utekelezaji uanze mara moja.

Akizindua mpango huo jijini Dar es Salaam, Waziri Mpina alisema, ni lazima mpango mkakati wa utekelezaji uwasilishwe ofisini kwake ndani ya kipindi hicho ili kuondoa dhana iliyojengeka ya mipango mingi kuandaliwa kwa muda mrefu na gharama kubwa, lakini usimamizi na utekelezaji wake kuwa dhaifu na kushindwa kuleta matokeo yaliyotarajiwa.

Alisema Tanzania ina mifugo mingi, ikiwa na asilimia 1.4 ya ng'ombe duniani na asilimia 11 ya ng'ombe Bara la Afrika wako Tanzania huku ikiwa ya pili barani Afrika baada ya Ethiopia. Waziri Mpina alisema fursa na changamoto zimefanikisha kuandaliwa kwa mpango huo ili kuondoa vikwazo na kuweka mazingira wezeshi ya ufugaji, biashara na uwekezaji.

Alizitaja changamoto hizo kuwa ni pamoja na ukosefu wa malisho na maji, wafugaji kufukuzwa kila mahali, ukosefu wa dawa na chanjo za mifugo, ongezeko la bidhaa za mazao ya mifugo kutoka nje ya nchi, uwekezaji wa kusuasua, ukosefu wa bei nzuri, soko la uhakika na mitaji na ukosefu wa mifugo iliyoboreshwa na huduma za utafiti.

Aliwataka wadau wa maendeleo walio ofadhili mpango huo Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI) na Taasisi ya Bill & Melinda Gate Foundation, kutoishia kufadhili uandaaji wa mpango huo badala yake washiriki moja kwa moja kwenye utekelezaji wake. Pia aliwataka watendaji wote wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa kujipanga na kushiriki katika utekelezaji wa mpango huo ili kuleta matokeo ya haraka.

Waziri Mpina pia aliitaka sekta binafsi, wafugaji, jumuiya za wafugaji, wafanyabiashara, wawekezaji, taasisi za fedha kila mmoja kwa nafasi yake ashiriki kutekeleza mpango huo. Kufuatia mpango huo, serikali italazimika kufanya marekebisho ya sera na sheria pamoja na kuanzisha mikakati na miongozo mipya ili kufanikisha utekelezaji wa mpango huo kwa ufanisi mkubwa.

Naye Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema kuzinduliwa kwa mpango huo kumeiwezesha wizara yake kupanga matumizi bora ya ardhi ili kufanikisha utekelezaji wa mpango huo.

"Ardhi yangu haina maana kama haitumiki vizuri, mimi nafurahi sasa mmejipanga na mmetengeneza mpango mzuri ambao utasaidia hata kunipa kazi ya kupanga matumizi ya kufanikisha mpango wenu, nataka nikuhakikishie mheshimiwa Mpina tuko pamoja najua mahitaji yenu," alisema Lukuvi.

Katibu Mkuu Mifugo, Profesa Elisante Ole Gabriel, alisema mpango huo ulianza kuandaliwa miaka mingi iliyopita, lakini sasa umekamilika na kuzinduliwa huku akimhakikishia Waziri Mpina kuwa atasimamia kikamilifu utekelezaji wake ili kuleta matokeo ya haraka yanayotakiwa na Watanzania.

Kwa upande wao mawaziri wastaafu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Titus Kamani na Dk. Charles Tizeba, walimpongeza Waziri Mpina kwa kufanikisha mpango na kukiri kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi sasa imejizatiti kusimamia sheria, hatua itakayoiwesha kupiga hatua kubwa ya maendeleo.

Wenyeviti wa CCM, mikoa ya Dar es Salaam na Pwani wamepongeza mpango huo na kusisitiza kuwa CCM kinathamini na kuunga mkono juhudi zinazofanywa na waziri Mpina katika kuleta mageuzi ya kweli katika sekta ya mifugo nchini.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Tanzania, George Bajuta alimshukuru Rais Dk. John Magufuli kwa jitihada anazofanya za kuwasaidia wafugaji nchini huku akimpongeza waziri Mpina kwa kuendelea kuwa kielelezo cha mageuzi katika sekta ya mifugo nchini.

## Wapendekeza Sheria ya Ndoa ifanyiwe marekebisho

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Agape mkoani hapo ambalo linajishughulisha na kutetea haki za watoto, limeilalamikia Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ambayo wameitaja kuwa kikwazo katika mapambano ya kutokomeza mimba na ndoa za utotoni mkoani Shinyanga.

Kwa mujibu wa takwimu za kitaifa za mwaka 2012, Mkoa wa Shinyanga unaongoza kwa tatizo la ndoa za utotoni kwa asilimia 59, ikifuatiwa na Mara (55) na Dodoma (51), huku asilimia za kitaifa zikiwa ni 37.

Hayo yalibainishwa jana na Meneja wa miradi kutoka Shirika la Agape, Mustapha Isabuda, kwenye semina na waandishi wa habari mkoani Shinyanga kuhusu kushirikiana kwa pamoja kupaza sauti kwa kutumia kalamu zao, kuipinga sheria hiyo ambayo imekuwa chanzo cha ndoa za utotoni.

"Katika kutekeleza miradi yetu ya kupinga mimba na ndoa za utotoni mkoani hapo tangu tulipoanza kufanya kazi mwaka 2009, kikwazo kikubwa ambacho kimekuwa kikitukwamisha kutokomeza tatizo hili ni Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, ambayo ina ruhusu mtoto kuolewa kwa ridhaa ya wazazi au mahakama," alisema Isabuda.

Pia alisema sheria hiyo inaweza kukwamisha mpango kazi wa serikali kitaifa (MTAKUWWA), kufikia malengo yake ya miaka mitano ya kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ambao umelenga kupunguza takwimu za ndoa za utotoni kutoka asilimia 37 hadi kufikia 10, mwaka 2022.

Kwa upande wake wakili wa kujitegemea mkoani Shinyanga, Maria Mwaselela, kutoka ofisi ya Mwaselela (Advocate), akiwasilisha mada alisema sheria hiyo inapaswa kufanyiwa marekebisho ya haraka kutokana na changamoto ya kuendesha kesi za ndoa za utotoni.



Wachuuzi wa samaki wakiwamwagia maji ili wasikauke wakati wakisubiri wateja katika soko la Kimataifa la Feri jijini Dar es Salaam. **PICHA: HALIMA KAMBI**

## TGC yaomba serikali kusimamia sheria ya madini

**Novatus Makunga,** ARUSHA

SERIKALI imeombwa kusimamia sheria ya kampuni ya madini ya vito inayotaka Mtanzania kuwa na mashine tano na mgeni tisa za kuchongea, kukata na kusanifia ili kudhibiti uuzaji wa madini ghafi nje ya nchi.

Ombi hilo limetolewa na Mratibu wa Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC), Ernest Mpese, alipokuwa anaongea na Nipashe ofisini kwake mjini hapa jana.

Alitaka kila mwenye kampuni ya madini kutimiza masharti ya leseni inayotaka mashine ya kusanifu madini ya vito, kutatengeneza ajira kwa vijana wa kitanzania, kuleta utaalamu na teknolojia pamoja na kuiingizia nchi fedha nyingine za kigeni.

Mpese alisema kuwa hivi sasa kuna shinikizo kubwa kutoka kwa wanunuzi wa madini wa kigeni kutaka madini ya vito yauzwe na kusafirishwa yakiwa ghafi kwa kuwa katika nchi zao yanatengeneza ajira nyingi.

"Wengi wamekuwa wakidai kwamba hatuna uwezo wa kusanifu kwa aina ya mikato wanayotaka na hivyo kushinikiza yasafirishwe yakiwa ghafi na kazi ya kuyasanifu na kuyakata ikafanyike katika nchi wanazotoka," alisema.

Mpese alifafanua kuwa kituo anachokisimamia cha Jemolojia kilichopo chini ya Wizara ya Madini kuanzia mwaka 2014 kimekuwa kikitoa mafunzo ya muda mfupi katika ukataji na usanifu na utambuzi wa madini ya vito pamoja na usonara.

Alisema kuwa kituo hicho katika kuongeza maarifa ya ufundisha kiliwahi kuwa na mkufunzi kutoka nchi inayosifika na kutambulika duniani kwa usanifu wa madini ya vito, Sri Lanka.

Aidha, Mpese alisema kuwa kituo hicho tayari kimeshakamilisha mchakato wa kuanza kwa mafunzo ya stashahada ya teknolojia katika madini ya vito na usonara inatakayochukua miaka mitatu.

"Tunakamilisha taratibu ndogondogo na wenzetu wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE), ili tuweze kutoa mafunzo ya muda mrefu na bahati nzuri tuna wakufunzi ambao tuliwapeleka nje kuongeza ujuzi zaidi," aliongeza.

Alisema kituo hicho ni cha pekee katika ukanda wa Afrika ya Mashariki na Kati chenye vifaa vya kisasa na kinachofundisha utaalamu wa usanifu wa madini na utambuzi wa madini ya vito pamoja na usonara.

Mpese aliipongeza kampuni ya Tanzanite Forever Lapidary ya mjini hapa ambayo imewaajiri wasichana 20 waliohitimu katika kituo hicho na kuanzisha kiwanda cha kampuni hiyo cha kusanifu madini ya vito.

## Kiwanda chalia uhaba wa maji

**Na Boniface Gideon, TANGA**

KAMPUNI ya Saruji ya Kilimanjaro, imelalamikia uhaba wa maji unaoendelea kuikumba katika kiwanda cha kutengeneza bidhaa hiyo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari waliotembelea kiwandani hapo kwa lengo la kufahamu changamoto zinazoikabili kampuni hiyo, msimamizi mkuu wa kiwanda hicho Pascal Demello alisema kuna baadhi ya siku wanalazimika kufunga kiwanda ili kusubiri maji yarudi.

Demello alisema hatua hiyo inatokana na mitambo yote inayotengeneza saruji kutegemea maji ili kujiendesha. Alisema hadi sasa kuna mitambo mingi imezimwa kwa kukosa maji.

"Mpaka sasa tumezima baadhi ya mitambo ili kusubiri maji yarudi na hatujui yatarudi lini. Hii ni changamoto kubwa sana kuliko changamoto zingine," alisema.

Kutokana na changamoto hiyo, alisema wamelazimika kuchimba visima, lakini bado mpaka sasa maji ya visima hayajasaidia kutatua changamoto hiyo kiwandani hapo kwa kuwa mahitaji ya maji ni makubwa kuliko uwezo wa visima.

"Tumechimba visima na tunaongeza vingine lakini hata tukiongeza kuchimba vingine, haviwezi kutatua changamoto kwa kuwa mahitaji ni makubwa kuliko uwezo wa visima," aliongeza.

Alisema kiwanda hicho kwa sasa kimeongeza uzalishaji lakini kama tatizo la maji halitatuliwa watalazimika kufunga kiwanda. "Tunaomba serikali itusaidie kutatua changamoto ya maji kwa kuwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (Tanga Uwsa) wameshindwa kutatua changamoto," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Usambazaji Maji wa Tanga Uwsa, Tito Lukanya, alisema kwa sasa mamlaka hiyo inakabiliwa na changamoto kubwa ya wizi wa maji kutoka kwa baadhi ya wateja wasio waaminifu, hivyo wako kwenye msako wa kuwasaka.

Pia alisema wako kwenye matengenezo ya mabomba kwenye maeneo yenye ujenzi wa barabara zilizoko ndani ya Jiji la Tanga na kwamba changamoto hiyo itakwisha hivi karibuni.

# Madereva wawashtaki mabosi kisa fedha za mafuta safarini

**Na Consolata Evarist, GEITA**

UMOJA wa Madereva wa Serikali mkoani Geita, umeuomba uongozi wa juu kukemea tabia ya baadhi ya mabosi wa halmashauri kuchukua fedha za mafuta zinazotolewa na serikali kwa ajili ya safari.

Madereva hao waliyasema hayo jana kupitia Maduhu Manjale, aliyesoma taarifa iliyoandaliwa na mwenyekiti wao lengo la kuisaidia kazi ya udereva kuonekana ina umuhimu kama zingine.

Taarifa hiyo ilitolewa katika kikao kilichofanyika kwa lengo la kuwakutanisha madereva wote na kueleza changamoto zao ili kuziwasilisha kwenye ngazi husika na hatimaye kupatiwa ufumbuzi.

Alisema katika baadhi ya halmashauri, mabosi wamekuwa na tabia ya kuchukua fedha ambazo zinatolewa kisha kuwapimia mafuta kidogo kidogo pindi wawapo njiani, hatua ambayo husababisha madereva kutokujiamini wakati fedha hizo zinatolewa kwa lengo la kukidhi mahitaji ya safari na si matumizi binafsi.

Manjale alisema katika Halmashauri ya Wilaya ya Chato hususan Idala ya Elimu, viongozi wamekuwa na tabia ya kulazimisha safari za usiku, kulazimisha mwendokasi na kuwatolea kauli mbaya madereva wawapo barabarani.

"Madereva wanalazimishwa safari za usiku, tunatolewa kauli mbaya. Mfano kuna kiongozi alimwambia dereva wake kuwa "huyu ni dereva tu wa kuokotwa mitaani". Tunalazimishwa kubadili mielekeo, mwendokasi hatua ambayo inasababisha kutokufuata alama za barabarani," alisema Manjale.

Alisema madereva wanakumbwa na changamoto nyingi kama kufanya kazi bila malipo ya ziada hasa kwa wale wanaoendesha magari ya wagonjwa, hawapewi muda wa mapumziko hali ambayo inasababisha msongo wa mawazo wawapo barabarani na kusababisha ajali nyingi.

"kinachosikitisha ni kuona wahudumu wa afya wanalipwa malipo ya ziada lakini madereva wanaowaendesha na kuwafikisha wagonjwa hawalipwi na wanafanya kazi saa 24. Hawana muda wa kutafuta liziki. Kwa upande mwingine dereva anakuwa mmoja, anatakiwa awepo kituoni muda wote na mishahara yetu ni midogo sana na familia zinatutegemea," alisema Manjale.

Mwenyekiti wa Chama cha Madereva wa Serikali Tanzania, Charles Mwaihojo, aliwataka madereva wa serikali mkoa wa Geita kuacha kuendesha magari kwa mazoea kwa kuwa tabia hiyo inadhalilisha taaluma yao.

Alisema madereva wengi wanaendesha magari yenye gharama kubwa bila mikataba ya kudumu hali ambayo itawasababishia matatizo pindi magari yatakapoharibika au kupata ajali kwa kuwa baadhi ya magari ya serikali hayana bima.

"Gari la mamilioni ya fedha ni vizuri mtu anayeendesha awe na mkataba ili kulinda chombo hiki. Nimefuatilia na kugundua magari yote katika mkoa huu hayana bima hali hii ni hatari kwa dereva na ni hatari kwa chombo," alisema Mwaihojo.

Pia aliziomba mamlaka za afya katika wilaya zote kuhakikisha zinawapatia madereva nyumba za kuishi karibu na maeneo yao ya kazi kwa sababu wanafanya kazi saa 24 na wanaishi mbali.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Geita, Japhet Simeo, alisema serikali ina uwezo mdogo sana wa kubeba dhamana yote ya mahitaji, hivyo inahitaji msaada mkubwa wa maoni na mawazo ili kuzifanya ofisi ziendelee kufanya kazi.


CAPITAL RADIO

POPOTE ULIPO SIKILIZA CAPITAL RADIO KATIKA MASAFA YAFUATAYO




www.capitalradioco.tz @capitalradiotanzania @CapitalRadiotz capitalradiotz



FARM AFRICA

## TANGAZO KWA UMMA

Farm Africa imesajiliwa nchini Tanzania mwaka 1990 kama shirika lisilo la kiserikali chini ya sheria ya mashirika yasiyo ya kiserikali ya mwaka 2002. Lengo lake la muda mrefu ni kuchangia kwenye kupunguza umasikini kwa kuendeleza mbinu za jamii kwaajili ya kuboresha uzalishaji kwenye kilimo na utumiaji endelevu wa ardhi hapa Tanzania.

Wazo kuu la Farm Africa ni Afrika yenye mafanikio wakati kazi yake kuu ni kuendesha mabadiliko kwenye kilimo na mazingira kwaajili ya kuboresha maisha. Mkakati wa Farm Africa una nguzo kuu tatu ambazo ni utaalamu wa kilimo, usimamizi na uhifadhi wa mazingira na nguvu ya biashara kuendesha kwa mafanikio. Farm Africa inafanya kazi na wazalishaji wa aina tofauti kama vile wakulima, wafugaji, wanaotegemea misitu na wafugaji wa samaki – kwenye maeneo tofauti ya kilimo na mazingira kama vile hali ya jangwa na nusu jangwa. Kwa mwaka 2016, Farm Africa imekuwa ikifanya kazi chini ya mkakati wake wa kimataifa wa mwaka 2016 – 2020.

Tarehe 04 Mwezi wa tatu Mwaka 2019 Farm Africa ilisaini mkataba na Shirika la Umoja wa mataifa la mpango wa chakula duniani (UNWFP- United Nations World Food Program) kutekeleza mradi wa majaribio kwa miezi saba wenye dhumuni la kusaidi kuboresha mnyororo wa dhamani kwenye zao la mtama mkoani Dodoma.

Mradi huu utasaidia kuongeza masoko ya kilimo, kuimarisha usalama wa chakula na lishe kupitia uimarishaji wa uzalishaji na Kipato ifikapo 2030. Jumla ya kiasi kitakachowezesha mradi huu wa miezi saba kutoka WFP ni shilingi za kitanzania million mia nne hamsini na tano laki tisa arobaini na nane elfu mia moja arobaini na mbili (TZS 455,948,142).

**Mradi unakusudia kufikia malengo yafuatayo;**

1. Wakulima wadogo wadogo wanaolengwa kufaidika na mnyororo wa dhamani unaofadhiliwa na WFP kuweza kuboresha njia za upatikanaji wa masoko yenye faida na kuongeza kipato.
2. Wakulima wadogo wadogo wanafaidika na uboreshaji wa huduma na bidhaa za kuepuka mabadiliko ya tabia-nchi kwaajili ya kuongeza uzalishaji, kipato na kupunguza athari za mabadiliko hayo.
3. Wakulima wadogo wadogo wanafaidika na fursa ya kufikia miundombinu ya kuhifadhi katika kaya na jamii kwaajili ya kupunguza upotevu na kuongeza ubora wa mazao

Mradi huu unatekelezwa mkoani Dodoma katika wilaya za Kongwa, Kondoa, Bahi, Chamwino na Mpwapwa. Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana nasi kupitia barua pepe: **infotanzania@farmafrica.org**

215108802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Msako wa wadaiwa sugu ardhi ufanyike kwa haki

**HATIMAYE** Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ametangaza kuanza kwa kampeni ya nyumba kwa nyumba kuwasaka wadaiwa sugu wa kodi ya pango ya ardhi na wale wa kodi ya ardhi ambao hawajalipa hadi mwaka huu.

Lukuvi alitangaza kampeni hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita Karatu mkoani Arusha alikokuwa ziarani kwa ajili ya kusikiliza na kutatua migogoro ya ardhi kwa wananchi wa wilaya hiyo katika kampeni yake ya Funguka kwa Waziri.

Katika kufanikisha kampeni hiyo ya kuwasaka wadaiwa sugu, Lukuvi aliwaagiza makamishna wasaidizi, maofisa ardhi katika wilaya na halmashauri zote nchini kuhakikisha wanawasaka watu hao kila nyumba.

Alisisitiza kuwa watu hao katu wasionewe huruma kwa kuwa wanarudisha nyuma mipango ya serikali katika kukusanya mapato kwa ajili ya maendeleo.

Katika kuonyesha kuwa hana mzaha na jambo hilo, alisema mtu yeyote anayedaiwa asionewe huruma kwa kuwa fedha hizo zingesaidia kuendeleza miundombinu ya kiuchumi na huduma kama vile afya, elimu na maji.

Sambamba na hilo, Lukuvi aliwaagiza wakuu hao wa idara za ardhi katika ngazi mbalimbali kuwafikisha katika vyombo vya sheria wale wote watakaobainika kuwa hawajalipa kodi hiyo ili sheria ichukue mkondo wake.

Hata hivyo, Waziri Lukuvi alitoa ahueni kwa wananchi hasa wamiliki wa ardhi ambao wanadaiwa fedha hizo za kodi ya ardhi kwa kuwataka wajitathmini na kulipa haraka kabla hawajakumbwa na msako huo na kufikishwa mbele ya sheria.

Uamuzi wa kuanzishwa kwa kampeni hiyo umetolewa baada ya viongozi wakuu wa wizara hiyo, wakiwamo Lukuvi na Naibu wake, Angelina Mabula, kufanya ziara katika maeneo mbalimbali na kushuhudia madudu ndani ya idara za ardhi kwenye halmashauri.

Katika ziara za Mabula, kwa mfano, ilishuhudiwa wananchi wanaomiliki ardhi wakiwa wanadaiwa mabilioni ya shilingi huku maofisa wake wakishindwa hata kuwapelekea hati za madai wahusika.

Hatua hiyo ilimfanya Mabula kuwanyooshea vidole maofisa ardhi katika wa halmashauri zikiwamo za mikoa ya Pwani na Mwanza ambao walikuwa hawajatoa hata asilimia 20 ya hati za madai kwa wamiliki wa ardhi.

Mabula hakuishia hapo tu kwani aliweka bayana kuwa suala la makusanyo ya serikali kupitia sekta ya ardhi si lelemama na waliopewa kusimamia dhamana hiyo wahakikishe wanatimiza wajibu wao na wale wasiofanya hivyo wajitafakari kama wanastahili kuendelea kuwa katika nafasi hizo.

Hata Waziri Lukuvi amekuwa akisisitiza mara kwa mara kuwa serikali kupitia wizara yake haina msalie mtume katika jambo hilo na atakayeshindwa kuwajibika hatavumiliwa hata kidogo.

Hatua iliyofikiwa na serikali katika kuwasaka wadaiwa sugu wa ardhi na kuwafikisha mahakamani ni ya kuungwa mkono kwa sababu watu hao ni washirika wakuu katika kurudisha maendeleo ya nchi.

Tunasema hivyo kwa sababu hicho ni chanzo kimojawapo cha serikali katika kukusanya mapato, hivyo kunapokuwa na kasoro au tatizo, ina maana kwamba mapato ya serikali yatadorora na matokeo yake miradi ya maendeleo haitatekelezwa kwa wakati na viwango vinavyotakiwa.

Pamoja na hayo, msako huo ufanyike kwa misingi ya haki kwa sababu katika operesheni mbalimbali, tumeshuhudia malalamiko mbalimbali watu kuwa wahusika walikuwa wakifanya vitendo vya kinyama ikiwamo kuomba rushwa na hata kudhalilisha watuhumiwa.

Kwa mantiki hiyo, ni vyema wahusika wa msako huo wakahakikisha wanatenda haki na wakati huo huo, wale wanaodaiwa wajitokeze kwa wingi kuhakikisha wanalipa madeni wanayodaiwa kabla ya kufikiwa na maofisa wa ardhi ambao watakuwa wanatekeleza amri halali ya serikali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

BUSARA

**MSAMIATI USIOUJUA UTATUMIAJE**
**KILA LUGHA INA MANENO YAKE AU MSAMIATI WA KUTUMIA. KAMA MANENO YA KIMASAI HUYAJUI KAMWE HUWEZI KUYATUMIA. KATIKA MAENDELEO HALI NI HIYO HIYO. MIKAKATI MIPYA YA MAENDELEO USIIPARAMIE BILA KUJIFUNZA KWANZA.**
**NA BALOZI CHRISTOPHER LIUNDI**




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Elimu ya watoto wetu wamiliki ni sisi wazazi

**KATIKA** juhudi za kuboresha elimu, serikali ilishatoa maelekezo kuwa kila shule ya msingi, ni lazima iwe na darasa la awali, kwa ajili ya watoto wadogo wanaojiandaa kuanza darasa la kwanza.

Maelekezo hayo yanatokana na ukweli kwamba msingi mkubwa wa elimu, unaazia chini kabisa, kwa maana ya shule ya awali, kwa sababu huko ndiko ambako kunakopatikana mwanafunzi anayefaa au asiyefaa.

Kutokana na ukweli huo, serikali ilitoa maelekezo hayo ili kwamba wanafunzi wanaoingia darasa la kwanza wawe wanajua kusoma na kuandika, kwani hatua hiyo ni utekelezaji wa mpango wa Kukuza Stadi za Kusoma (KKK) kwa ajili ya kuboresha elimu kwa wanafunzi.

Hata hivyo, pamoja na lengo hilo nzuri, bado kumekuwapo changamoto ambazo zinaweza kukwamisha maendeleo ya watoto, iwapo wazazi hawatazivalia njunga na kuzimaliza haraka iwezekavyo. Ninasema hivyo, kwa sababu baadhi ya changamoto zipo chini ya uwezo wao, hivyo wakiwa kimya zinaweza kuathiriwa zaidi kwa elimu ya awal, hivyo kuendelea kuwapo wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika.

Kuna taarifa zilizowahi kuandikwa na vyombo vya habari miaka michache iliyopita, kwamba wanafunzi wa darasa la awali katika Shule ya Msingi Mkambarani mkoani Morogoro, walikuwa wakisomea jikoni, kwa sababu ya uhaba wa vyumba vya madarasa shuleni hapo.

Hizo ni taarifa za sehemu moja, lakini inawezekana kuna shule nyingi zenye changamoto za aina hiyo, ambayo kimsingi kama nilivyosema awali, zipo kwenye uwezo wa wazazi.

Wakati baadhi ya shule zikikumbwa na ukosefu wa vyumba vya madarasa, wazazi na walezi wapo, ni kama wameridhika nayo, kwa watoto wao kusoma katika mazingira hayo.

Mchango walionao kuboresha elimu ya watoto wao ni upi? Hapo tunapaswa kujuliza. Hivi, wanasubiri wafanyiwe kila kitu na serikali? Kuna ugumu gani wa kuitisha vikao kwa ajili ya maendeleo ya shule na watoto wao kwa ujumla?

Siyo vizuri kusubiri serikali itufanyie kila kitu, bali jamii sasa ibadilike kwa kutambua wajibu wake katika kuhakikisha watoto wanapata elimu, tena katika mazingira bora kuliko kujiweka pembeni, kana kwamba haihusiki.

Mazingira kama hayo ya kusomea jikoni, yanaweza kusababisha watoto wengi wakahitimu shule ya awali bila ya kujua kusoma na kuandika. Watoto wasaidiwe kwa kila hali, ili kuhakikisha wanakuwa na madarasa yao.

Ikumbukwe, miaka ya nyuma msingi wa ufundishaji watoto elimu ya awali ulikuwa haupewi kipaumbele hasa maeneo ya vijijini na kusababisha baadhi ya wanafunzi kuhitimu hata elimu ya msingi, bila kujua kusoma na kuandika.

Serikali ililibaini hilo na kuamua kila shule ya msingi ni lazima iwe na darasa la awali kwa ajili ya 'kuwanoa' watoto ili wanapoanza darasa la kwanza wawe wanajua kusoma na kuandika.

Kinachotakiwa ni wazazi na walezi kuhakikisha wanakuwa mstari wa mbele katika kuchangia maendeleo ya elimu kwenye maeneo yao, badala ya kutegemea serikali ifanye kila kitu.

Vilevile, ni muhimu wazazi na walezi kutambua kwamba walimu ni msingi mzuri kwa ajili ya kuwasaidia watoto kupiga hatua, hivyo ni muhimu kushirikiana nao kwa kila hali.

Karne hii ya sayansi na teknolojia siyo tena ya kuwa na wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika, hivyo wazazi na walezi wasichangie kuwapo kwa wanafunzi wa aina hiyo.

Wambue kwamba elimu ya watoto wao iko mikononi mwao, kwani wanapaswa kushrikiana kwa karibu na walimu ili kutatua changamoto zinazozikabili shule ikiwamo ukosefu wa madarasa ya elimu ya awali.

Bila wazazi na walezi kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa madarasa hayo, elimu ya awali inaweza kusuasua kwenye baadhi ya shule za serikali.

Serikali ilishaweka wazi kwamba huwa inaunga mkono pale wananchi wanapoonyesha juhudi zao, hivyo ni vyema jamii ikatambua hilo na kulizingatia kuliko kungojea kufanyiwa kila kitu.

# MJADALA & BARUA

## *Kazi yenu nzuri Sumatra*

**Mhariri**

*NAPENDA kutumia nafasi hii kuipongeza Mamlaka ya Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (Sumatra), kwa jitihada inazozifanya kuboresha uwepo wa njia nyingi za usafiri ndani ya jiji letu la Dar es Salaam.*

*Ni maboresho ambayo kadri muda unavyoenda nazidi kushuhudia mapya, ikiwamo njia nyingi za magari ya usafiri wa umma zilizopewa kibali, kutoka sehemu moja hadi nyingine.*

*Nadhani nilieleze hilo kwa kutumia mfano wa kuwapo njia nyingi za usafiri kutoka Mbagala, kwenda sehemu nyinginezo za jiji, mbali na kulikozoeleka katikati ya jiji; Kariakoo, Muhimbili, Posta na Kivukoni.*

*Kikubwa kinachonifanya nitumie mfano huo, inatokana na ushuhuda wa adha hiyo kwa ndugu zangu wakazi wa Mbagala, kunakoonekana kuwapo wakazi wengi sana na wamekuwa wakitaabika na usafiri, ambao awali ulikuwa wa kuja mjini tu .*

*Sasa tunashuhudia makubwa, kuwepo kwa njia nyingi za usafiri lama vile kutoka Mbagala hadi Makumbusho na maeneo mengi  nje ya mji.*

*Jambo hili, pia katika sura nyingine kumepunguza adha ya mlolongo wa magari katikati ya jiji la Dar es Salaam, ambako sasa kumepunguziwa mzigo na msuguano wa foleni, ikizingatiwa pia sehemu kubwa ya watumishi wa umma na ofisi zao, zimehamia jijini Dodoma.*

*Sasa nawashauri Sumatra watanue zaidi huduma zao katika mustakabali mpana zaidi, kwa kuchungulia njia ambazo kuna makazi, shughuli za umma na watu wanaongezeka, kunapata huduma zaidi ya usafiri. Hii ndio tunayohitaji kuiona katika ukuaji wa jiji.*

*Hayo yakiendelezwa na kuboreshwa, hapana shaka huduma ya usafiri Dar es Salaam, itakuwa imeimarika zaidi, wakazi kunufaika na hapo inajengwa maana ya hali ya maendeleo.*

*Kwa vile, Sumatra ni chombo cha kitaifa, katika miji na manispaa zote zinazokua, inapendeza zaidi kushuhudiwa aina hii ya maendeleo.*

**Maskon Habina,**
**Majohe, Dar es Salaam.**




# Ikoje hii ya saa moja kasoro dakika 25 na saa 12: 35?

**Na Lazaro Mateko**

**MOJA** ya sekta za umma yenye watumishi wengi, ni elimu. Pia, imo katika zinazokabiliwa na changamoto nyingi sana.

Hapo tunataja mambo kama kufanya kazi katika mazingira magumu, hali ambayo kimsingi inawakatisha tamaa wengi kuwa na upendo wa kutumikia fani hiyo.

Si ajabu kushuhudia kuna shule walimu wanafundishia katika mazingira yasiyofaa, baadhi wako katika kiwango kibaya, wanasomea chini ya miti na hata madarasa ya 'mbavu za mbwa'.

Serikali nayo kwa upande wake imekuwa ikijitahidi kuhakikisha inaboresha mazingira ya kufanyia kazi walimu, ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi bila ya kuvunjika moyo.

Viongozi wa serikali katika maeneo yao ya kazi, wamekuwa wakibuni mbinu mbalimbali za kuwaboreshea walimu mazingira ya kazi, pia kubuni njia za kuwafanya wafurahie kazi yao.

Mfano mmojawapo, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, aliwahi kutamka kwamba katika vitu vinavyomnyima usingizi, ni pale anapoona walimu wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Kutokana na hali hiyo, amewahi kuanzisha kampeni ya ujenzi wa ofisi nzuri na za kisasa, kwa ajili ya walimu, ili kuhakikisha heshima yao inarejea.

Siyo kampeni hiyo tu, pia alianzisha mkakati wa kuwapa walimu vitambulisho vinavyowawezesha walimu kupanda daladala bila ya kulipa nauli, kama njia ya kuwapunguzia makali ya maisha.

Hatua hiyo inasaidia kuwatia moyo walimu ili waendelee kufanya kazi yao kwa bidii ingawa changamoto zao hazijaisha, lakini kwa kiasi fulani kuna unafuu, hivyo ni vyema mfano huo uigwe, ili walimu wajione wanathaminiwa.

Wakati kukiwapo juhudi hizo za kuwatia moyo walimu, kuna baadhi ya watu ambao wamekuwa wakiwaona walimu katika sura ya ukakasi, kwa sababu wanazozijua wenyewe, hawataki kushirikiana nao.

Baadhi ya wazazi wakiitwa shuleni kuelezwa matatizo ya watoto wao hugeuka mbogo na kuwatishia walimu, hali inayoweza kuchangia kushusha ari yao ya ufundishaji.

Wapo wengine ambao wamekuwa wakituhumiwa kuwapiga walimu eti kwa sababu tu wamewaadhibu watoto wao, hali kama hiyo ni sawa na kuwanyong'onyeza na kudhalilisha.

Wengine wakiambiwa kushiriki shughuli za maendeleo ya shule hawataki kusikia kabisa habari hizo, kana kwamba maendeleo ya shule siyo jukumu lao.

Walimu wanapodharauliwa, ni wazi kwamba ufundishaji wao nao hauwezi kuwa mzuri na matokeo yake ni kushuka kwa kiwango cha elimu.

Siyo wazazi na walezi tu bali hata wanasiasa nao wamekuwa wakichangia kuwakatisha tamaa walimu kwa kuwasingizia mambo ambayo hawakufanya.

Hebu fikiria mwalimu anafika shuleni saa moja kasoro dakika 25 asubuhi halafu anakuja kiongozi wa kisiasa anamkaripia, kwa madai siyo kweli bali amefika shuleni saa 12 na dakika 35.

Kisha mdai huyo anakuwa mkali kwamba mwalimu anatamka uongo, kwa vile ameona katika kitabu cha mahudhurio imeandikwa saa 12: 35.

Hivi, kuna tofauti gani kati ya saa moja kasoro dakika 25 na saa 12: 35 na katika mabishano hayo ya hoja ya kutaalamu, nani amesimama mahali sahihi?

Ni vizuri, viongozi wetu mjitahidi kutokuwa sehemu ya kuwakatisha tamaa walimu na kama mtu hujui kitu ni vyema akauliza au kuzama mbali kujifunza, kuliko kulazimisha mada katika mwelekeo usiofaa.

Inapendeza, kama taaluma ya ualimu ikaheshimiwe kwa kiwango stahiki, kwa mujibu wa matendo mbalimbali yanayohusiana na fani yenyewe. Hii ndio fani inayozalisha kila kada iliyoko, iwe viongozi au wasomi wa kila aina.

Pia, isipothaminiwa, matokeo yake ndio hayo ya watu kuwalaumu walimu katika staili ya saa moja kasoro dakika 25 na saa 12: 35 kuwa vitu tofauti.

Tatizo ni kwamba baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakijiona ni wataalamu wa elimu hadi kufikia kuwasimamisha walimu hadharani, ili wajieleze ni kwanini wanasema wamefika shuleni saa moja kasoro dakika 25 huku katika daftari la mahudhurio wakiwa wameandika saa 12: 35.

Hapa anayeonekana hajui ni nani kati ya mwalimu na huyo kiongozi wa kisiasa? Walimu waheshimiwa,watiwe moyo na wapewe ushirikiano kwa ajili ya maendeleo ya elimu, kwa kuwa ndio chimbuko la wasomi wote.

Mwalimu ana utaalamu wa kumwezesha mtoto kuanza kuhesabu, kusoma na kuandika, baadaye mwalimu humfundisha mwanafunzi maarifa ya jamii, hisabati, stadi za kazi, sayansi, afya, lugha na taaluma mbalimbali.

Hivyo, kwa majukumu hayo aliyo nayo, ni muhimu nafasi yake ikaheshimiwa.

## KABWELA NA FADHIL MOHAMMED




## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Kiini mauaji watoto, wanawake bayana

INATOKA UK. 2

"Wanaoua watoto wanaamini watapata mali. Lakini pia kuna mauaji ambayo yanafanyika kwa sababu ya kulipa kisasi. Kuna wahalifu pia wanateka watoto ili wapate fedha, wasipopewa fedha, wanaua watoto," alisema.

Nyambuta aliongeza: "Mauaji dhidi ya wanawake nayo yanahusisha na imani za ushirikiana, lakini pia jamii inalihusisha suala hili na harakati za uchaguzi.

"Kwa kuwa na matukio ya aina hii, jamii inarudi nyuma kimaendeleo, yanajenga hofu kwa watoto na wanawake, wanaogopa kutoka kushiriki kwenye shughuli za maendeleo kwa hofu ya kuuawa."

Nyambuta alishauri serikali iimarishe ulinzi na kutokomeza vitendo hivyo ili kuondoa hofu iliyotanda miongoni mwa jamii na kuwezesha shughuli za uzalishaji mali kuendelea kwa utulivu na amani nchini.

Mtazamo huo wa Nyambuta unaungwa mkono na timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto iliyokwenda mkoani Njombe mwanzoni mwa mwaka huu kuchunguza kiini cha mauaji dhidi ya watoto mkoani humo.

Kiongozi wa timu hiyo, Hanisa Selengu, alisema kuwa katika kipindi cha siku tatu walizokaa mkoani Njombe, walibaini sababu tatu zilizochangia kuwapo kwa vitendo vya mauaji dhidi ya watoto mkoani humo.

Selengu alizitaja sababu zilizochangia kuwapo kwa changamoto hiyo kuwa ni tabia ya kukumbatia mila potofu na zisizofaa zinazochangia kuwa na mifarakano katika jamii, migogoro ya kifamilia ambayo imekuwa ikisababishwa na visasi vya wazazi na ndugu pamoja na desturi ya ukimya na ugumu wa kueleza uhalifu unaotokea.

**KUTOA KAFARA**

Katika mikoa ya Njombe na Iringa, vitendo vya mauaji ya watoto kutokana na imani za kishirikina vimekuwa vikiripotiwa kwa muda mrefu kutokana na sababu mbalimbali. Miongoni mwa sababu hizo ni kujipatia utajiri au mazao mengi kutokana na shughuli za kilimo.

Katika kufanya hivyo, baadhi ya watu wenye imani za kishirikina ambao huamini kuwa kufanya hivyo, husaidia mtu kupata utajiri.

Mmoja wa wazee wa Mkoa wa Iringa (jina tunalihifadhi) aliiambia Nipashe mwezi uliopita kuwa, kuna uwezekano mkubwa wa wagan-ga wa jadi katika mikoa hiyo na ya jirani huwapa masharti wateja wao wanapowapa dawa, kwamba wanapaswa kuwaua kimiujiza au kwa namna yoyote watoto wao.

Mzee huyo pia alidai kuwa, mbali na kuwaua, baadhi ya wazazi huwafanya watoto wao kuwa na dalili za mtindio wa ubongo (mazezeta) na wengine huwageuza misukule.

Aliendelea kueleza kuwa kukithiri kwa vitendo hivyo katika mikoa hiyo, ambayo zamani ulikuwa mmoja wa Iringa kabla ya kugawanywa na kuwa Iringa na Njombe, hutokana na ushirika miongoni mwa watu katika jamii husika ambao huwekeana ahadi ya kuua mtoto wa kila mmoja wa washirika kwa mzunguko. Hatua hiyo husababisha watoto katika familia hizo kufariki dunia kwa namna mbalimbali.

Sambamba na hilo, mzee huyo alidai kuwa baadhi ya watu ambao hujishughulisha na kilimo katika mikoa hiyo miwili, hudiriki kushiriki vitendo vya mauaji ya watoto kwa njia za kishirikina wakiamini kufanya hivyo huwawezesha kupata mazao mengi.

Alidai kuwa kufanya mauaji ya watoto kwa imani hiyo, wenyeji wa mikoa hiyo miwili hukuita 'ndimilo', wakiamini kwamba kutekeleza mauaji hayo husababisha kupata mazao mengi wakati wa mavuno.

"Mauaji hayo yatokanayo na imani za kishirikina pia husababisha kuibuka kwa visasi na malipizo ambayo huwafanya baadhi ya watu wa familia kuchukua hatua kwa kutekeleza mauaji kwa watoto wa baadhi ya ndugu ambao hudaiwa kushiriki vitendo hivyo," mzee huyo alidai.

Febuari 19, mwaka huu, akiwa mkoani Simiyu, IGP Sirro alisema aliwahakikishia viongozi wa mkoa huo kuwa Jeshi la Polisi litamaliza matukio hayo ya mauaji, huku akibainisha kuwa yanaonekana kusababishwa na imani potofu za kishirikina.

"Nimeongeza nguvu kutoka makao makuu ya jeshi kushughulikia suala la matukio ya Lamadi. Njia pekee ya kukomesha mauaji ni elimu zaidi itolewe kwa wananchi, kuna watu bado wanaamini kupata samaki wengi mpaka watumie hizo njia za kishirikina," alisema.

IGP Sirro aliongeza: "Tulifanikiwa kudhibiti na kukomesha mauaji ya vikongwe na watu wenye ualbino, lakini sasa yameanza kujitokeza mauaji ya watoto ambayo yanatokana na uchonganishi wa waganga wa jadi."



Mkazi wa jiji akikokota baiskeli yake iliyosheheni matunda aina ya matikiti maji, katika makutano ya Barabara ya Uhuru na Mandela, eneo la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

## Awataka wanawake kuchangamkia fursa

**Na Mary Geofrey**

MKURUGENZI Mtendaji wa Benki ya NIC, Margaret Karume, amewataka wanawake kuchangamkia fursa mbalimbali za kukuza uchumi katika ukuaji wa teknolojia ya huduma za kibenki zinazotolewa nchini.

Karume alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati akikabidhi msaada kwa wagonjwa katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

"Katika kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani, tunawasihi wanawake kuchangamkia fursa zinazotolewa na benki katika kukuza uchumi wao ikizingatiwa kuwa tupo zama za ukuaji wa teknolojia," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa katika kuadhimisha siku hiyo, Benki ya NIC ilijitolea kutoa msaada kwa wanawake wanaougua saratani wanaopata matibabu katika taasisi hiyo.

"Leo tunaadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, tumeona ni vyema kuja kushiriki na wagonjwa katika hospitali hii ili kuwapa misaada tuliyojaliwa kuja nayo kwa kutambua thamani ya wanawake nchini," alisema.

Aliongeza kuwa benki hiyo imefungua milango ya mikopo kwa watu wote ili kuwawezesha kufikia malengo yao na kukuza uchumi wa taifa.

Alisema misaada waliyowapatia wagonjwa hao wa saratani ni kanga, miswaki, sabuni, dawa za meno, kandambili na taulo za kike. Alisema misaada hiyo itakuwa chachu ya kutambua thamani ya wanawake katika jamii.

Alisema jamii inatakiwa kuwasaidia wahitaji, hasa ya wagonjwa ya saratani ambao matibabu yao ni ghali na yanawasumbua watu wengi nchini.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Taasisi ya Saratani Ocean Road, Malkiory Nimiko, aliyepokea misaada hiyo, aliishukuru benki hiyo kwa msaada waliotoa na kuwahakikishia kuwa itawafikia walengwa wote.

## CUF washangaa ukimya Polisi

INATOKA UK. 2

kutaka tu kushinikiza maoni yao," Jaji Mutungi alisema.

Simu ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) Simon Sirro, haikupokewa alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia suala hilo. Naibu Mkurugenzi wa Habari na Mawasiliano wa CUF, upande unaomuunga mkono Prof. Lipumba, Abdul Kambaya, alisema wanaendelea na mkutano wao kwa kuwa hakuna zuio lolote walilopewa mpaka sasa.

"Hatuna zuio lolote kwa sasa, tutaanza kesho (leo) mkutano wetu, lakini waandishi wa habari mnaruhusiwa kushiriki mkutano huu kuanzia tarehe 14 (keshokutwa)," Kambaya alisema.

CUF imekuwa na mgogoro wa kiongozi tangu mwishoni mwa mwaka 2015 baada ya Prof. Lipumba kutangaza kujiuzulu nafasi yake na baadaye kurejea na kutengua barua ya kujiuzulu kwake.

## Shehena samaki wenye sumu yanaswa

INATOKA UK. 2

ya samaki na mazao ya uvuvi unaongozwa na Sera ya Uvuvi ya Mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2009.

Alisema kufuatia sera na kanuni hizo, sekta binafsi inaweza kuwekeza kwenye viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi.

Alisema uwekezaji huo unahusisha kampuni ambazo zinamilikiwa na wazawa na wageni.

Alisema kampuni inayofanya biashara ya uvuvi ni lazima kukidhi matakwa ya kisheria ikiwamo kutambulika na mamlaka mbalimbali zinazohusika na biashara.

# TFS yapewa somo ufugaji nyuki pembezoni mwa hifadhi

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

BODI mpya ya Ushauri ya Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), imetakiwa kuanzisha utaratibu wa ufugaji nyuki pembezoni mwa hifadhi za taifa ili kusaidia wanyama wasitoke na kuingia kwenye makazi ya watu.

Ushauri huo umetolewa juzi na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, wakati akizindua bodi mpya ya TFS jijini Mwanza.

Alisema ufugaji nyuki utaongeza ajira katika nyanja mbalimbali zikiwamo za kiuchumi kwa wananchi.

"Ufugaji huo utasaidia serikali kuhifadhi misitu bila kutumia nguvu kubwa ya kidola, kutokana na baadhi ya wananchi kuvamia maeneo ya hifadhi za wanyama, itasaidia hata wananchi kuvuna asali na kuuza katika masoko ya nje," alisema.

**Ufugaji huo utasaidia serikali kuhifadhi misitu bila kutumia nguvu kubwa ya kidola, kutokana na baadhi ya wananchi kuvamia maeneo ya hifadhi za wanyama.**

Dk. Kigwangalla alisema ikiwa asali itakuwapo kwa wingi wawekezaji wa bidhaa zitokanazo na asali watakuja nchini na kushauri kuwapo mkakati wa kuwawezesha wananchi kushiriki ufugaji huo ili uweze kuwaingizia kipato na maendeleo ya kiuchumi.

Alisema wanyama wamekuwa wakivamia makazi ya watu na kusababisha vifo, uharibifu wa mashamba, mazao na kuitaka TFS kuona umuhimu wa ufugaji wa nyuki ili wananchi wanaoishi karibu na hifadhi hizo waweze kunufaika kupitia miradi hiyo.

Aliitaka bodi kuhakikisha inasimamia vema misitu pamoja na ufugaji huo kwa kutumia teknolojia za kisasa ili kutimiza majukumu yao na kasi ya Rais John Magufuli ya awamu ya tano.

Dk. Kigwangalla aliitaka TFS kutumia taratibu za kisheria ili misitu iliyo chini ya usimamizi wa vijiji na halmashauri nchini iweze kuchukuliwa na kuwa chini ya wakala huo, ikiwa miaka minane iliyopita misitu iliyokuwa chini ya vijiji na halmashauri, ilitumika vibaya na kuifanya kama kitenga uchumi wao.




Ofisa Muuguzi kutoka Mpango wa Taifa wa Damu Salama, Rosemary Bulemo, akimtoa damu mmoja wa wafanyakazi wa Diamond Trust Bank Tanzania (DTB), wakati wa zoezi la kuchangia damu ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU**

# DTB kufungua tawi la wanawake

**Na Beatrice Shayo**

BENKI ya DTB inakusudia kupata usawa wa kijinsia katika nguvu kazi yake ndani mwaka huu na kufanya mchakato wa kufungua tawi maalum lenye wafanyakazi wanawake jijini Dar es Salaam.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam na Meneja Mkuu wa Idara ya Mawasiliano na Teknolojia DTB, Stella Masha, wakati wa kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani.

Alisema benki hiyo inazingatia usawa na ndio maana wanataka kufungua tawi maalum litakalohudumiwa na wanawake.

Alisema Siku ya Wanawake Duniani inaadhimishwa kwa dhumuni la kufurahia maendeleo ya wanawake katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

"Wito ni kuzingatia usawa wa kijinsia ulimwenguni na kaulimbiu ya Siku ya Wanawake kwa mwaka huu ni "Kuzingatia usawa katika jamii zetu. Ulimwengu ulio sawa kijinsia ni ulimwengu bora zaidi," alisema.

Masha alisema kama ilivyo sera yao ya rasilimali watu benki ya DTB inaunga mkono usawa wa kijinsia katika kutoa ajira na wamefanikiwa kwa asilimia 49.1 ni wanawake.

Aidha, alisema katika matawi 14 yaliyopo Dar es Salaam asilimia 50 ni wanawake, benki imekusudia kupata usawa wa jinsia katika nguvu kazi yake katika mwaka huu.

"Pia tupo katika mipango ya kufungua tawi maalum lenye wafanyakazi wanawake pekee Dar es Salaam kabla ya mwisho wa mwaka huu, kwa kuwa tumeona mafanikio yao na ubora wao katika utendaji kazi wao," alisema.

Aliongezea kuwa: "Tunapenda kuwapa fursa wanawake na ndio maana nguvu kazi yetu tunawapa wanawake kipaumbele," alisema Masha.

Aidha, alisema katika kuadhimisha siku hiyo wameandaa mkusanyiko uliolenga kusaidia wanawake kufikia malengo yao katika ajira na maisha nje ya sehemu ya kazi.

Alisema wanajitolea kuchangia damu na wananchi wataelimishwa kufahamu bidhaa na huduma za benki maalum kwa wanawake.

"Wanawake ni nguvu kazi katika ukuaji wa uchumi na hazina ya maamuzi kwenye matumizi ya fedha katika uendeshaji wa benki kwa kuzingatia hilo tumejizatiti kuimarisha mazingira yetu ya kazi, ili kuongeza ufanisi na kuzingatia mahitaji ya wanawake wafanyakazi pamoja na wateja wetu kwa ujumla," alisema.

# Wenye ulemavu wa usikivu waelimishwa mitandao ya kijamii

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

CHAMA cha Viziwi Tanzania (Chavita) kwa kushirikiana na Taasisi kwa ajili ya Maendeleo Shirikishi (I4D), wameamua kuwapatia mafunzo maalumu ya matumizi ya mitandao ya kijamii watu wenye ulemavu wa kusikia (viziwi) ili waweze kuzitambua fursa mbalimbali zinazotolewa ndani ya nchi na nje ya nchi na kuwasaidia kujikwamua na umasikini.

Akizungumza katika mafunzo hayo yaliyoshirikisha wenye ulemavu huo kutoka mikoa ya Morogoro, Iringa, Dar es Salaam, Arusha, Dodoma na Tanga, Mkurugenzi Mtendaji wa Chavita, Dickson Mveyange, alisema lengo lingine ni kuhakikisha jamii hiyo haiachwi nyuma na inashiriki kikamilifu katika mkakati wa serikali wa kuelekea katika uchumi wa viwanda.

"Serikali ipo katika mkakati wa kuinua uchumi kupitia sekta ya viwanda na sisi tunataka jamii hii ya viziwi isibaki nyuma nayo ishiriki kikamilifu ndio maana tunawafundisha kutumia mitandao ya kijamii ambako hivi sasa kila kitu kinawekwa huko nao wazione fursa kupitia simu zao na kuchangamkia kama Watanzania wengine," alisema Mveyange.

Alisema wenye ulemavu wa usikivu wana changamoto nyingi hasa katika maeneo yanayotoa huduma za kijamii kama kwenye sekta za afya, elimu, mahakamani, polisi na sehemu nyingine kwenye mikusanyiko ya watu kutokana na kukosekana kwa mawasiliano, hivyo kupitia mafunzo hayo yatawezesha kusaidia njia ya mawasiliano.

"Wenye ulemavu wa usikivu wanakwenda hospitali kwa ajili ya tiba, lakini kwa kuwa hakuna mkalimani mganga wakati mwingine huandika dawa tofauti na kile anachoumwa," alisema mkurugenzi huyo.

Meneja Uhusiano wa Taasisi ya I4D, Noel Thomson, alisema, wamekuwa wakifanya kazi kwa karibu na Chavita ili kuhakikisha sauti wanazopaza kutokana na changamoto zinazowakabili zinafika kwa watoa maamuzi waweze kuchukua hatua mbalimbali.

Alisema kuwa taasisi hiyo inaamini kuwa endapo wenye ulemavu wa usikivu wataweza kutumia mitandao ya kijamii itawasaidia kufikisha ujumbe na mawazo yao kwa jamii pamoja na watoa maamuzi mbalimbali ikiwamo viongozi wa serikali kulisaidia kundi hilo.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Frank Jacob, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa huo, alisema serikali imepiga hatua katika kushughulikia ustawi wa watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na kutunga sheria zinazoinua na kulinda makundi mbalimbali ya kijamii ili yaweze kupata fursa za kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya taifa bila kuwapo vikwazo.

# Sababu uhaba maziwa bora zatajwa

**Na Boniface Gideon,** TANGA

KAMPUNI ya usindikaji wa maziwa ya Tanga Fresh, imetaja sababu za wafugaji wengi kushindwa kuzalisha maziwa yanayokidhi viwango ikiwamo kuchanganya maji kwenye maziwa.

Meneja Mkuu wa Tanga Fresh, yenye makao makuu jijini hapa, Michael Karata, alisema hayo juzi wakati wa ziara ya Mbunge wa Tanga Mjini, Mussa Mbarouk, kiwandani hapo.

Mbunge huyo alifanya ziara hiyo kwa lengo la kufahamu changamoto zinazoikabili kampuni hiyo ya uzalishaji na usindikaji wa bidhaa zitokanazo na maziwa nchini.

**Wengi wanafahamu ila wanafanya makusudi. Tunataka tuongeze soko ifikapo Juni, mwaka huu.**

Karata alisema kiwanda hicho kinahitaji lita 120,000 kwa siku lakini mpaka sasa wanasindika lita 50,000 tu. Alisema, sehemu kubwa ya maziwa wanategemea kutoka kwa wafugaji lakini wameshindwa wameshindwa kukidhi mahitaji ya kiwanda.

Licha ya kuchanganya maziwa na maji, Karata alisema sababu nyingine ni ng'ombe kukosa lishe bora na ukame.

Alisema awali walilazimika kununua maziwa nje ya nchi, lakini kwa sasa hawafanyi hivyo na kwamba licha ya kuongeza vituo vya kukusanyia maziwa kwa baadhi ya mikoa, bado kiasi kinachopatikana hakikidhi mahitaji ya kiwanda.

"Mahitaji ya maziwa bado ni makubwa sana. Tunahitaji maziwa bora na yenye viwango ili kushindana kwenye soko la kimataifa lakini kiwango kikubwa cha maziwa ya wafugaji wetu hayakidhi viwango na ubora unaohitajika," alisema.

Alisema kwa sasa wamefanya upanuzi wa kiwanda, hivyo mahitaji ya maziwa ni makubwa lakini changamoto kubwa ipo kwa wafugaji hasa wa vijijini kushindwa kukidhi viwango vinavyohitajika kutokana na ukosefu wa elimu ya ufugaji na uzalishaji bora wa maziwa.

"Niwaombe wafugaji wetu wazingatie ubora wa maziwa. Wengi wanafahamu ila wanafanya makusudi. Tunataka tuongeze soko ifikapo Juni, mwaka huu," alisema.

Mbarouk kwa upande wake, aliishukuru serikali kwa kudhibiti uingizwaji wa maziwa toka nje ya nchi hali iliyofanya Watanzania kupenda kutumia maziwa ya ndani.

Aliwataka wafugaji kuitumia fursa hiyo ya soko la ndani kwa kuzalisha maziwa bora na kumtaka mwekezaji huyo kutoa mikopo kwa wafugaji ili kuongeza uzalishaji wa maziwa.

"Nikuombe Karata utoe mikopo kwa wafugaji ili kuongeza uzalishaji wa maziwa bora maana wafugaji wengi wa Tanzania hawana vifaa na wengi wao ni wafugaji wa kuhamahama. Hii inapunguza uzalishaji wa maziwa bora," alisema.



Mchuuzi wa mahindi akisaka wateja pembezoni mwa barabara jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Waathirika mimba utotoni kuwezeshwa

**Na Magreth Magosso,** KIGOMA

WASICHANA walioathirika na mimba za utotoni katika wilaya za Kibondo, Kakonko na Kasulu, watanufaika na elimu juu ya kunyonyesha vichanga na kujikwamua kiuchumi ikiwa sehemu ya kutatua changamoto za malezi zinazowakabili.

Elimu hiyo inatarajiwa kutolewa baada ya Chama cha Wakunga Tanzania (TAMA) kukamilisha mpango wa kuwatambua wasichana walio chini ya umri wa miaka 18 ambao walipata ujauzito na kujifungua.

Lengo la elimu hiyo ni kuwajengea uwezo wa kujikwamua kiuchumi ikiwamo kupata misaada kutoka kwa jamii katika wilaya hizo.

Mpango huo utakuwa wa miaka minne na kaulimbiu yake ni "Ujana Wangu Nguvu Yangu" na umeanzishwa baada ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA) kubaini wasichana hao kuongezeka kwa kasi hali inayochangia maendeleo duni kuanzia ngazi ya familia hadi taifa.

Ofisa wa Tama, Hilda Kwezi, alisema mwishoni mwa wiki kuwa mpango huo ni matunda ya utafiti uliofanywa na UNFPA baada ya kubaini changamoto zilizopo juu ya wasichana kujifungua katika umri mdogo.

"Vijana watafundishwa juu ya unyonyeshaji, kumwangalia mtoto mchanga baada ya kujifungua, namna ya kukabiliana na jamii baada ya kujifungua, kupangilia uzazi na kuwasaidia kiuchumi wakiwa katika vikundi," alisema.

Alisema katika kutekeleza mpango huo, wataunda makundi ya wasichana yatakayokuwa na fursa ya kuzungumza mambo yanayowahusu, huku wahudumu wa afya na maofisa wa serikali ngazi za vijiji na kata wakiwezeshwa namna ya kutambua huduma rafiki kwa vijana.

"Vijana wengi wana changamoto ya mifumo ya utendaji kazi iliyopo katika vituo vya afya, hospitali na ofisi za serikali kwa kushindwa kuzifikia huduma mtambuka. Lakini mpango unatengeneza huduma ili ziwafikie hasa walio chini ya miaka 18 ambao wameathiriwa na mimba za utotoni," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika la Maendeleo ya Vijana Kigoma (Kivides), Babu Pascal, alisema atashirikiana na TAMA katika kupunguza changamoto ya mimba za utotoni kwa watoto wa kike ambao ni waathiriwa wa kwanza katika kukatisha ndoto zao za kimaisha siku za usoni.

Naye Sheik Hassan Ntabile alisema familia zinatakiwa kuwalea watoto katika maadili ya dini na misingi ya dini ni chagizo kwa watoto wa kike kupata ujauzito katika umri mdogo, huku akiikumbusha jamii kusaidia kulinda maadili.

Dk. Wilfred Mongo kutoka Shirika la Engender Health, kwa upande wake, alikiri kuwa uzazi katika umri mdogo unahatarisha afya ya mama na mtoto kwa kuwa wote au mmoja anaweza kupoteza uhai, hali inayochangia ulezi wa mazingira magumu hasa ukomavu wa mwili na akili.

# Waliokufa kwa ajali wasafirishwa kwao

**Na Steven William,** MUHEZA

WATU watatu waliofariki dunia katika ajali ya gari lori wiki iliyopita wilayani hapa, wamesafirishwa kwenda kwao, Tabora, Kigoma na Amani wilayani Muheza kwa ajili ya mazishi.

Watu hao walikuwa wafanyakazi wa Kampuni ya East Usambara Tea Company Ltd (Eutco) iliyoko Amani wilayani Muheza. Katika ajali hiyo, watu wengine 54 walijeruhiwa vibaya.

Mwenyekiti wa Chama Cha Wafanyakazi wa Kilimo na Mashambani (Tpawu) Tawi la Kwamkoro wilayani Muheza, Sylvester Kalingo, alisema wafanyakazi hao watatu wamesafirishwa kwa kwenda kwao kwa ajili ya mazishi kwa gharama ya kampuni.

Kalingo aliwataja wafanyakazi hao na mikoa walikopelekwa kuwa ni Mathayo Reuben (Kigoma), Paulo Mwagi (Tabora) na Ester Gorden (Amani).

Kwa mujibu wa Kalingo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Tpawu Kanda ya Kaskazini, majeruhi wanaendelea na matibabu katika Hospitali ya Teule ya Wilaya ya Muheza kwa gharama za kampuni.

Katika ajali hiyo, wafanyakazi watatu wa Eutco, walifariki dunia katika ajali ya gari na 54 kujeruhiwa vibaya wakati wakienda kazini asubuhi kuchuma chai mashambani.

Ajali hiyo ilitokea Ijumaa iliyopita katika eneo la kijiji cha Shebomeza, kata ya Amani, baada ya lori aina ya Tata walilokua wamepanda kutumbukia katika korongo na hatimaye kusababisha ajali hiyo na kuua watu watatu.

# Mkuu wa Mkoa ampiga mkwara mbunge CCM

**Na Mwandishi Wetu,** BABATI

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, amemjia juu Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, Vrajlal Jituson (CCM), kuwa atamchukulia hatua endapo ataendeleza kuchochea migogoro ya ardhi kwenye eneo hilo.

Alisema hayo katika kijiji cha Maweni wakati akiagiza ng'ombe 774 waliokuwa wameshikiliwa na serikali ya kijiji hicho kuachiwa baada ya kuingia katika Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Burunge (Juhibu) na kurudishiwa wafugaji.

Alisema amepata taarifa kwamba mbunge huyo anachochea wafugaji kuingia kwenye maeneo ya hifadhi kwa madai kwamba mwanasiasa mwakilishi huyo wa wananchi anafanya hivyo kwa malengo ya kisiasa mwaka 2020.

Alimwonya mbunge huyo kuwa akiendelea kuchochea wafugaji kwa kuwaambia wakachungie mifugo yao hifadhini, atamwonyesha kuwa yeye ndiye Mkuu wa Mkoa wa Manyara.

"Nataka nikwambie mbunge kwamba nakuheshimu sana, sitaki uendelee kuchochea migogoro na awamu hii mtu akivunja sheria simkamati aliyevunja, namkamata aliyemtuma kuvunja, sitaki mtu aje kunipapasa sharubu," alisema.

Alisema wafugaji hao wamepandikizwa chuki kuwa yeye hawapendi wafugaji wa jamii ya Wabarbaig jambo ambalo siyo kweli, kwasababu yeye anaongoza mkoa wote, wananchi wote ni wa kwake wakulima kwa wafugaji bila kuchagua.

"Anakuja mwanasiasa njaa kwa sababu ya kuangalia kura za mwakani anadanganya watu halafu wakipigana na kuuana yeye anakimbilia Dodoma hilo sitalikubali litokee Manyara," alisema.

Hata hivyo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, Vrajlal Jituson alikanusha madai hayo ya uchochezi yaliyotolewa na Mnyeti kwa kudai kuwa hakuwahi kufanya hivyo na anashangaa kuambiwa kuwa yeye ni mchochezi.

Jituson alisema migogoro ya ardhi katika Jimbo la Babati Vijijini ilikuwapo miaka mingi hata kabla hajawa mbunge na eneo hilo lina mgogoro wa zaidi ya miaka 10.

# Naibu Waziri Ole Nasha asifu matumizi nyuklia

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, amesema Tanzania imepiga hatua katika matumizi salama ya nyuklia katika miradi ya afya, maji, kilimo na mingine, ikilinganishwa na nchi zingine za Afrika.

Alisema hayo wakati akifungua mkutano wa siku tano wa waratibu wa miradi ya sayansi na teknolojia ya nyuklia kutoka nchi wanachama 46 wa Shirika la Nguvu za Atomiki la Kimataifa (IAEA).

Alisema wamekutana hapo kwa ajili ya kuweka mikakati ya matumizi sahihi ya atomiki.

Mkutano huo umewashirikisha wataalamu wa nguvu za atomiki kutoka nchi 46 za Afrika, wakijadili utekelezaji wa miradi ya matumizi salama ya sayansi na teknolojia ya nyuklia katika nchi zao.

Alisema nchi za Afrika zimepata manufaa makubwa katika matumizi ya atomiki hususani Tanzania ambayo imepata zaidi ya shilingi bilioni 9 zinazotekeleza miradi mbalimbali ikiwamo ya ununuzi wa vifaa tiba vya kuchunguza kansa Ocean Road na kuigundua.

**Tanzania ipo makini katika utumiaji wa teknolojia hiyo, kwa kuwa hivi karibuni waliweza kufungia hospitali 102 ambazo zilikuwa zikitumia teknolojia hiyo bila kuzingatia usalama wa watu.**

"Mionzi inayotumika katika matibabu ya kansa ni manufaa yaliyotokana na shirika hili ambalo Tanzania sisi ni wanachama na pia tumenufaika na ujenzi wa maabara ya kisasa ya nguvu za atomiki iliyopo Njiro na tunatumia katika kilimo pia teknolojia hii," alisema.

Ole Nasha alisema licha ya kupata baadhi ya manufaa hayo, bado wanaendelea kupata mafunzo mbalimbali ya jinsi ya kudhibiti mionzi ili isilete madhara na kupitia mkutano huo wataondoka na mbinu mpya za kukabiliana na hilo.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Nguvu za Atomiki nchini, Profesa Lazaro Busahala, alisema kupitia mkutano huo wanatarajia kufanya maamuzi ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika nyanja za afya, kilimo na maeneo mengine.

Alisema mionzi hiyo imeleta manufaa makubwa nchini kwa kuboresha matibabu ya saratani kupitia vifaa vya kisasa vinavyotumika vya mionzi hiyo.

Alisema Tanzania ipo makini katika utumiaji wa teknolojia hiyo, kwa kuwa hivi karibuni waliweza kufungia hospitali 102 ambazo zilikuwa zikitumia teknolojia hiyo bila kuzingatia usalama wa watu.

Alisema kati ya hizo hospitali 40 zimekidhi masharti wameshazifungulia kutoa huduma na 72 bado hazijatekeleza masharti zimefungiwa.

Mkurugenzi wa Ufundi upande wa Afrika wa Shirika la Atomiki, Shaukat Abdulrazak, alisema Tanzania itanufaika zaidi kupitia mkutano huo kwa kuboresha huduma za matumizi ya nyuklia.

Alisema kuna baadhi ya nchi zipo nyuma katika matumizi ya nyuklia na zingine ikiwamo Tanzania iko mbele katika matumizi hayo, hivyo kupitia mkutano huo watapeana mbinu za kuboresha ili wote wanufaike na teknolojia hiyo kwenye nyanja mbalimbali.



Wanawake wanaojihusisha na shughuli za ujasiriamali wakijiandaa kuingia ndani ya ukuta unaozunguka migodi ya madini ya tanzanite Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Sakata kuingia kuchimba tanzanite pasaua kichwa

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

OFISI ya Madini Simanjiro mkoani Manyara, inatarajia kuweka utaratibu wa kuingia ndani ya ukuta unaozunguka migodi ya madini ya tanzanite, kwa kutumia vitambulisho maalum.

Daudi Ntalima alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki na kusisitiza kwamba utaratibu huo utawezesha kubaini makundi yanayoingia ndani ya ukuta huo tofauti na ilivyo hivi sasa, ambapo wanatakiwa kuonyesha kitambulisho cha mpigakura ili kuingia.

Alisema baada ya masharti ya kuingia ndani ya ukuta kulegezwa idadi ya wanaoingia ni kubwa hivyo kuna haja ya kutoa vitambulisho ili kudhibiti wanaoingia.

Hata hivyo, alisema makundi maalum yatapewa kipaumbele katika kupewa vitambulisho hivyo, ikiwamo walemavu na wanawake hasa wanaochekecha mchanga.

Alisema tatizo la usafiri kwa madereva wa pikipiki wanaobeba abiria (bodaboda) ndani ya ukuta kuzidisha bei wakati wanawapandisha abiria kuwapeleka machimboni atalifanyia kazi.

"Tutakaa kikao na wenzangu na kujadili hili kisha tutaweka tangazo ya bei ya kupandisha abiria na bodaboda atakayetoza bei ya juu tupeni taarifa yake sisi tutamuondoa ndani ya ukuta," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake Wachimbaji Madini na Vito nchini, (Tawoma), mkoani Manyara, Rachel Njau, alisema ukuta huo unawapa ulinzi kwa kuwa madini yao hayataibiwa tena.


Alisema wanawake wenye umiliki wa viwanja vya madini wapo 30 na wengi wao ni wajane, walioachiwa migodi baada ya kufiwa na waume zao na kuachiwa watoto.

"Tumeachiwa migodi ambayo tumekuwa tukiiendeleza kidogo kidogo kwa kujituma katika ujasiriamali baada ya kushinda kesi za kutaka kudhulumiwa na ndugu wa marehemu," alisema.

Alisema serikali iangalie kwa jicho la tatu suala la baadhi ya wanawake wanaoingia ndani ya ukuta bila shughuli na kuvaa mavazi ya kujidhalilisha.

Mmoja kati ya wanawake wachekechaji, Halima Yusuph, alisema baadhi ya bodaboda wanakimbiza pikipiki kwenye barabara mbovu za machimboni na kusababisha viungo mbalimbali ikiwamo mbavu zao kuwauma.

Mfanyabiashara wa magonga, Salome Mnyawi, alisema hivi sasa anajivunia kulipa kodi tofauti na hapo awali alikuwa hajaelimishwa juu ya hilo.





# Mtalii aangusha neema ya masomo kwa mbeba mizigo

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SHEREHE ya kumbukumbu ya kuzaliwa ya raia wa Uholanzi, Frank Vitaal (80), zilizofanyika katika kilele cha Uhuru cha Mlima Kilimanjaro, zimeacha 'neema' kwa mpagazi mdogo zaidi wa kike anayefanya kazi ngumu, Fatma Halfan ambaye ameahidiwa ufadhili wa masomo ili aweze kukabiliana na changamoto za makali ya maisha.

Wapagazi ni watu maalum wanaofanya kazi ngumu ya kubeba mizigo ya watalii wanaopanda Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (Kinapa) au hifadhi nyingine 15 zilizopo chini ya Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa).

Raia huyo wa Uholanzi na watalii wengine 20 kutoka nchini humo ambao waliomsindikiza Vitaal kuadhimisha sherehe yake ya kuzaliwa yaani 'Birthday Party' baada ya kufikisha umri wa miaka 80, aliguswa na kazi ngumu anayofanya mwanamke huyo mwenye watoto watatu na kutangaza kufadhili masomo yake atakayochagua kusoma katika chuo chochote hapa nchini.

**Nimeona kazi ngumu wanayofanya wapagazi katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro, mtu kama Fatma ni wa kumsaidia kujiendeleza zaidi katika maisha yake. Birthday yangu itakuwa faraja ya maisha yake.**

Wakati Fatma anapata bahati hiyo, alikuwa mbeba mzigo pekee wa kike, kati ya wanaume 78 waliongozana na wageni hao wakiwamo waongoza watalii wapatao tisa.

"Niko tayari kufadhili masomo yake (Fatma), natambua kazi anayoifanya ni ngumu kupita uwezo wake, najua hata Kampuni yake ya Chagga Tours iliyomuona na kumpa nafasi ya kujituma ili kujipatia kipato kupitia sekta ya utalii inamthamini mwanamke. Msichana huyu nitamlipia gharama zote za masomo atakayotaka kusoma katika chuo chochote Tanzania, ni shupavu na jasiri," alieleza Vitaal.

"Nimeona kazi ngumu wanayofanya wapagazi katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro, mtu kama Fatma ni wa kumsaidia kujiendeleza zaidi katika maisha yake. Birthday yangu itakuwa faraja ya maisha yake."

Baada ya mzee huyo wa miaka 80 kutoa ahadi hiyo, Fatma alieleza kufurahishwa kwake na uamuzi wa mzee huyo pamoja na wageni wengine raia wa Uholanzi kwa kumpa fursa ya kujiendeleza na masomo ya lugha ili kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuwatunza watoto wake watatu wanaomtegemea kwa sasa.

Awali, muongoza watalii mkuu wa Kampuni ya Chagga Tours inayoratibu safari za utalii wa wageni katika Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro, Michael Nelson, alisema wageni hao wamefanikiwa kufika katika vituo tofauti mbalimbali ikiwamo kituo cha Stela point kilichopo mita 5,740 kutoka usawa wa bahari na watalii saba kufika kilele cha Uhuru.

Kwa kawaida, safari ya kupanda mlima Kilimanjaro humpitisha mpandaji katika kanda za hali ya hewa tofauti kuanzia ile ya nchi za tropiki hadi arktiki. Kilele cha Kibo chenye urefu wa mita 5,895, ndicho kivutio kikubwa kwa wageni kutokana na kufunikwa na theluji.

Katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro, kuna njia sita za kupanda hadi kileleni na njia iliyo rahisi na iliyo maarufu zaidi ni ile ya kuanzia lango la Marangu ambako ndiyo makao makuu ya hifadhi.




Mbeba mizigo pekee wa kike katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro, Fatma Halfan (katikati), anayefanya kazi Kampuni ya Chagga Tours, akiwa na Frank Vitaal (kushoto) aliyeahidi kugharamia masomo yake chuo chochote Tanzania. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Wananchi Bomang'ombe wapigwa butwaa

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

WAKAZI wa Kitongoji cha Kilimambogo kilichoko katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Bomang'ombe, Wilaya ya Hai, wamepigwa butwaa baada ya kushuhudia mwanafunzi wa Shule ya Msingi Elerai iliyoko eneo hilo akiwa anatapika mawe.

Tukio hilo la aina yake limewashangaza wananchi wengi, huku wengine wakilihusisha na imani za kishirikina.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kitongoji hicho, Ombeni Swai, aliiambia Nipashe jana kuwa mwanafunzi aliyekumbwa na hali hiyo na kuacha maswali yasiyo na majibu ana umri wa miaka 10.

"Ni kweli kuna mtoto hapa kwetu ametokewa na hilo jambo na mimi binafsi nilipigiwa simu na mwananchi wangu mmoja, akinijulisha kuwa kuna tatizo nyumbani kwa bibi Juliana Willbad, kwamba kuna mtoto anatapika mawe, kitu ambacho sio cha kawaida," alisema Swai.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, alipokwenda katika eneo la tukio alimkuta mtoto huyo akiwa anaendelea kutapika mawe, jambo ambalo lilimshangaza na kuagiza mtoto huyo kupelekwa hospitali mara moja kwa ajili ya uchunguzi.

Alidai kuwa baada ya kuona tatizo hilo, aliagiza mtoto huyo kupelekwa hospitalini kwa ajili ya uangalizi zaidi na kupata huduma. Hata hivyo mtoto huyo kwa sasa anaendelea na masomo yake akiwa hana tatizo.

Kwa mujibu wa Swai, mtoto huyo alipelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Hai kwa ajili ya uchunguzi.

# Jukwaa la majadiliano latia neno kutokomeza ukatili kijinsia

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKATI serikali ikiwa kwenye hatua za mwisho za maandalizi ya kupeleka katika Bunge la Bajeti mapendekezo ya bajeti ya wizara zake, jukwaa la majadiliano ya kisera mkoani Kilimanjaro limeitaka Wizara ya Afya kutenga ruzuku maalum kwa ajili ya kuziwezesha kamati zinazotekeleza mpango wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Tusonge linaloratibu jukwaa hilo, Agnatha Rutazaa, alisema mpango huo ulioanza kutekelezwa mwaka 2016 nchini kote na ambao utafikia ukomo mwaka 2022, haujatengewa fedha kwa ajili ya kuendesha kamati zinazowajibika kuutekeleza.

"Tunajua shughuli za Bunge la Bajeti zitaanza rasmi Aprili 2, mwaka huu na kila wizara itawasilisha mapendekezo ya bajeti yake. Sasa katika bajeti ya mwaka mpya wa fedha 2019/2020, tunaitaka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto itenge bajeti ya kuwezesha kamati za MTAKUWWA (Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili wa Wanawake na Watoto) kwa ngazi zote," alieleza Rutazaa.

Tangu kuanza kutekelezwa kwa mpango huo, inaelezwa kuwa serikali haijawahi kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza mpango huo ngazi za wilaya na mikoa nchini.


Katika jukwaa hilo, wadau hao wa maendeleo kutoka mashirika zaidi ya 12 ya kiraia, walishauri licha ya kutengwa kwa ruzuku hiyo, lakini pia utekelezaji wa mpango huo upewe kipaumbele katika ufuatiliaji na tathmini.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya ya Same, Johnston Mndeme akitoa mchango wake katika jukwaa hilo, baadhi ya changamoto zinazoukabili mpango huo ni pamoja na kukosekana kwa huduma rafiki wakati wa kushughulikia masuala ya wahanga wa ukatili.

Kwa upande wake, Ofisa Ustawi wa Jamii wa Manispaa ya Moshi, Magreth Reuben, alikiri kuwa kamati hiyo inakabiliwa na changamoto kutokana na kutokuwa na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake.

"Ni kweli baadhi ya wazazi wanakosa stadi za malezi na baadhi ya wanajamii wanakuwa hawana ushirikiano wa kutoa taarifa dhidi ya ukatii wa watoto na wanawake. Lakini wazazi wa kiume kutoa pesa za matumizi kwa familia," alisema Magreth.

Nipashe
# TESA
Jumanne Machi 12, 2019
TEKNOLOJIA . ELIMU . SAYANSI



Ukurasa 18

## JE, WAJUA?
WAWEZA KUJIFUNZA KITU CHOCHOTE KWA SAA 20 TU



## Maisha mapya kutoka umemejua kwa wasiojua umeme Korogwe

Ukurasa 15



# Kipaji cha kuandika mlemavu chamwacha Waziri Mkuu katika butwaa la simanzi

Ukurasa 16



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Kiswahili chazidi kuborongwa

'BORONGA' ni kitenzi elekezi na maana yake ni bananga kitu au jambo; haribu kazi au jambo; atili, vuruga. Ndivyo waandishi wa habari (hasa wa magazeti ya michezo) wafanyavyo katika zama hizi.

"Simba ndio habari ya mujini" ni kichwa cha gazeti maarufu humu nchini. Yashangaza na kusikitisha! Kwa nini mhariri wa michezo aliridhia neno 'mujini' badala ya 'mjini' ambalo ndilo sahihi? Ingeandikwa "Simba ndio habari ya mjini" wasomaji wasingeelewa?

Hushangazwa sana na waandishi wanaotumia maneno ya mitaani na kuiga maneno yasiyo ya Kiswahili halisi na kuyatumia kwenye habari na makala zao! 'Mujini' hutamkwa na watu wa baadhi ya mataifa jirani. Fuatilia mazungumzo ya kocha wa timu moja kubwa, utaelewa unachosoma hapa. Kiswahili chao, sicho kinachozungumzwa Tanzania!

Baadhi ya maneno ya Kiswahili, hutumiwa kwa maana tofauti na maudhui (wazo kuu linaloelezwa katika kazi ya fasihi. Wazo linaloelezwa katika maandishi au katika kusema).

"Mechi ya watani, matawi yamejipanga balaa." Habari iliyofuatia iliandikwa: "Watoto wa mjini wanakwambia mambo ni moto kuelekea mchezo wa watani wa jadi, Simba na Yanga utakaopigwa leo kwenye Uwanja wa Taifa, jijini Dar es Salaam, katika matawi ya mashabiki na wanachama wa timu hizo, hakupoi wala hakuboi."

"... matawi yamejipanga balaa." Maana ya 'Balaa' ni jambo, kitu au mtu anayefikiriwa kuleta maafa, mkosi au hasara; kisirani, nuksi. Jambo lenye kuleta hali ya kukosewana; kizaazaa, mtafaruku. Kwa hiyo neno 'balaa' halikutumiwa ipasavyo.

Aidha mwandishi ameandika: "... mchezo utakaopigwa ..." Nimeeleza mara kadhaa kuwa mchezo haupigwi bali unachezwa. Kinachopigwa uwanjani ni mpira.

"... hakupoi wala hakuboi." Mwandishi ametohoa neno 'boa' kutoka Kiingereza, 'bore' lenye maana tatu: 1) toboa, pekecha, chimba. 2) Chosha, sumbua (kwa mazungumzo yasiyovutia) na 3) ni wimbi kubwa sana la kuchanua. Kwa muktadha ninaoujadili, mwandishi angetumia angeandika: "hakupoi wala hakuchoshi" badala ya 'hakuboi.'

"Banka aitaka Simba hata leo, tizi la Moro balaa" ni kichwa cha habari. 'Tizi' ni neno lililozoeleka sana na waandishi wa michezo ingawa lina Kiswahili chake. 'Tizi' limetoholewa kutoka Kiingereza, yaani 'practice' na maana yake kwa Kiswahili ni 'mazoezi.' Hushangaa sana waandishi wanapotumia neno 'tizi' badala ya 'mazoezi!' Maana ya 'balaa' nimeeleza huko juu.

"Huyu ndiye MK14 bana hakuachii." "Ajibu kumbe alichemka bana." "Kumbe Ajibu alichemka hapa bana!" "Fedha ni sabuni ya roho buana ..." Yashangaza siku hizi waandishi wa habari za michezo kutumia neno 'bana' au 'buana' badala ya neno sahihi, 'bwana!'

'Bana' maana yake ni weka kitu katikati na kutumia nguvu kukisonga pande zote; gandamiza, fyanda; shika kwa nguvu kama vile mtego; nasa, kamata, funga. Pia ni neno la kutahadharisha kuhusu matumizi mazuri yaani tumia kwa uangalifu bila kufuja. 'Banana' ni kuwa karibu mpaka miili ikagusana; minyana. Kwa Kiingereza 'banana'ni ndizi.

"Huko Msimbazi shangwe kama lote unaambiwa. Hii ni baada ya chama lao la Simba kuizima Yanga, katika mechi yao ya 102 katika Ligi ya Bara tangu zianze kukutana mwaka 1965." Maana ya 'shangwe kama lote' ni nini? Twajua kuwa 'shangwe' ni mkusanyiko wa watu wanaokwenda pahala au wanaofurahia jambo kwa pamoja. 'Ote' maana yake ni bila ya kubakia. Nashindwa kuelewa maana ya 'shangwe kama lote!'

'Chama' ni muungano wa watu wenye lengo moja. Pia kitendo cha mtu kukatisha urafiki na mwingine; susia. Wingi wa 'chama' ni 'vyama.' Kwa hiyo husemwa 'chama changu au chetu,' (kimoja) na 'vyama vyetu' (vingi) Hata chama kingekuwa kikubwa (kwa maana ya wingi wa wanachama wake) sana hakiitwi 'chama langu' au 'chama letu!'

Mara kwa mara huandika kuwa maneno yanayozungumzwa si sawa na yanayoandikwa. Kwa mfano isemwapo: "wajua bwana, mh sijui nisemeje ..." huwezi kuandika maneno hayo gazetini kwani hayo ni mazungumzo. Wasomaji wanataka kujua yaliyozungumzwa badala ya porojo - "wajua bwana, mh sijui nisemeje!" Maneno haya yanamweleza nini msomaji?

"Tamasha la mkeka, mvinyo funika bovu." Haya ni maneno ya mitaani ingawa pia si wote (nikiwemo mimi) tunaofahamu maana ya 'funika bovu!' Ndo maana baadhi ya waandishi huandika kama wazungumzavyo mitaani!

"Funika" ni kitendo cha kuzuia kuonekana kwa kuweka kitu kingine (Wanzibari husema chengine) juu yake; fidika. Maana ya "bovu" ni -enye kutofanya kazi sawasawa kutokana na kuharibika; -lioharibika, -siopendeza, -sioweza kutumika. "Tamasha la mkeka, mvinyo funika bovu" maana yake ni nini?

"Achana na pambano la watani wa jadi unaambiwa juzi kati jijini Dar es Salaam, ile siku ya Wapendanao kulifanyika bonge la shoo bab'kubwa iliyopewa jina la Mkeka na Mvinyo na watu wakashangweka kinomanoma katika tamasha hilo." Haya ni maneno ya mitaani; siyo ya kuandikwa gazetini. Mwandishi anatakiwa kuwajuza wasomaji wake jambo au mambo yaliyotokea badala ya kuandika maneno yasiyoeleweka.

Kwa nini mwandishi aandike "unaambiwa?" Pili, "juzi kati" ni siku ipi kati ya saba zinazofanya wiki moja? "... wakashangweka" ndo kwanza nalisikia neno hilo! 'Shangwe' ni mkusanyiko wa watu wanaokwenda pahala au wanaofurahia jambo kwa pamoja. Hili la "wakashangweka kinomanoma" ndo kwanza nasoma gazetini! "Noma" lina maana mbili: 1) kipande anachopewa mtu kuthibitisha kwamba alikuwa kazini. 2) kizuizi; pingamizi.

**Methali: Usiache mbachao kwa msala upitao.**

***marobarnabas@yahoo.com***
***0715/0784 33 40 96***

## ELIMU KUTOKA POLISI



Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) Ahmed Msangi. **PICHA: MTANDAO**

# HAKUNA UHURU USIOKUWA NA MIPAKA

UHURU ni ile hali ya mtu mmoja au kundi kubwa la watu au taifa kuwa na uwezo wa kuamua mambo yao wenyewe bila ya kuingiliwa na mtu au watu wengine bila kuvunja sheria, taratibu na tamaduni zilizowekwa na jamii au taifa.

Kwa mtu binafsi, uhuru ni hali ya mtu kuwa na uwezo wa kuamua juu ya maisha yake mwenyewe, bila ya kuingiliwa na mwingine, huku akitii na kufuata sheria, kanuni na tamaduni za jamii yake.

Mtu aliye huru, anaamua afanye kazi gani, halazimishwi kuabudu dini fulani, na hazuiliwi kutoa maoni kuhusu nchi yake au jambo lolote katika jamii. Mtu huru hafundishwi kuogopa watu, bali hufundishwa kuheshimu watu.

Mpaka ni ukomo wa jambo au mwisho wa jambo fulani. Watu wanaoamini katika dhana ya mpaka wa uhuru, wanaeleza kuwa watu wako huru kwa kiasi fulani tu hivi au wako huru kwa masuala fulani tu, lakini hawako huru kwa masuala mengine.

Mtu anayetumia uhuru wake bila kuvunja sheria, taratibu na tamaduni za jamii yake, kwa kutumia uhuru huo, kamwe hawezi kuwekewa mipaka na mtu yeyote kwa sababu uhuru ni kufanya kile unachojisikia bila kuvunja sheria au kanuni zilizokubaliwa na jamiii au nchi.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, Naibu Kamishna (DCP) Ahmed Msangi, anayeeleza kuwa ni wajibu wa wananchi kuepuka kushiriki katika mikutano, maandamano na harakati za kuichokoza mamlaka ya dola kwa uwasilishaji wa malalamiko au kero kwa njia ambazo zinasababisha bughudha au karaha kwa wengine.

"Kamwe hupaswi kutumia njia, ishara au maneno ambayo yanaweza kutafsiriwa kwamba umevunja sheria za nchi, pia kuidhalilisha, kuikebehi au kuitukana mamlaka halali mbele ya macho ya umma," anasema DCP Msangi.

Sote tunaipenda nchi yetu na tunahitaji kuwa na maisha bora, kwa kuwa na misingi imara ya ustawi wa jamii. Lakini, kuipenda nchi si kigezo cha kufanya harakati ambazo jamii ya waliostarabika huziita 'za kihuni' kwa kudai haki bila ya kuzingatia wajibu wa kisheria katika kudai haki zao.

Uhuru unaopatikana kwa mujibu wa sheria katika kutoa maoni, malalamiko au mawazo mbadala haupaswi kutumiwa vibaya au kuwa kinga ya kukunja uso na ngumi, ili utambulike kwamba ni mjuzi wa kudai au kuwasilisha maoni, kero au malalamiko ya jamii. Njia hiyo sio ya kistaarabu na haitokani na misingi ya taifa letu.

Ni vyema jamii ikafahamu kwamba, uwasilishwaji wa hoja kwa njia ya hekima na busara huwezesha kupatikana kwa ufumbuzi wa kero au tatizo bila kuathiri misingi ya ustawi wa jamii na taifa kwa ujumla.

**Imetolewa na:**
**Kitengo cha Uhusiano,**
**Makao Makuu ya Polisi,**
**S.L.P 9141**
**Dar es Salaam.**
**Baruapepe:habariphq@yahoo.com**
**habari.phq@tpf.go.tz**

# TEKNOLOJIA

## NA JENIFER JULIUS, KOROGWE

# Maisha mapya kutoka umemejua kwa wasiojua umeme Korogwe

UMBALI wa kilomita 45 kutoka Korogwe Mjini, katika Kijiji cha Mpale kisichojua umeme wa Wakala wa Umeme Vijijini (REA), mwendo wa saa mbili kwa kutumia bodaboda, barabara ya vumbi.

Huko ndiko anapatikana Mahmud Athumani, fundi seremala anayetumia mashine ya kisasa ya kuranda mbao katika ofisi yake.

Akiwa na uso uliojaa furaha na shauku ya kueleza kwa kina mafanikio ya ofisi yake, anasema kuwapo umemejua kijijini hapo, ndio kumemwezesha kutumia kifaa hicho.

Mahmud, ambaye mara kwa mara alikuwa akitoa maelekezo ya kutumia kifaa hicho kwa wasaidizi wake, anasema alipata kifaa hicho kwa mkopo Novemba mwaka jana, kutoka kwa kampuni ya umemejua ya Ensol.

"Gharama ya mashine hii ni Sh.430, 000. Nilipewa kwa mkopo na ninalipa kidogo kidogo mpaka nitakapomaliza," anasema Mahamud.

Tangu aanze kutumia kifaa hicho, Mahmudu amekuwa akimaliza kazi za wateja kwa wakati na anakiri kipato chake kimeongezeka, tofauti na awali alipokuwa anatumia kifaa cha kawaida.

"Nashukuru Mungu sasa sina viporo. Mwanzo nilikuwa nalaza kazi mbili hadi tatu. Mashine niliyo nayo sasa, inafanya kazi mara tatu zaidi ya ile ya mwanzo," anasema.

"Kwa upande wa makusanyo 'alhamdulilah' (nashukuru Mungu) nakusanya Sh.50, 000 kwa siku tofauti na zamani nilikuwa napata Sh.20, 000", anaendelea.

Mahamud si peke yake katika wanufaika wa mradi wa umemejua uliowekwa na kampuni ya Ensol kijijini hapo mwaka 2017 baada ya kutimiza vigezo.


Kwa mujibu wa Prosper Magari, Mkurugenzi wa Miradi kutoka kampuni ya Ensol, walipofanya utafiti katika kijiji hicho waligundua kuwa kina wakazi zaidi ya 3000, kaya 500 na uchumi unaojitosheleza hivyo kupata sifa ya kufungiwa umeme.

Kuna jumla ya wakazi 156 wanaonufaika, huku vijiji jirani kama vile Mali, ewe na Kwemanoro, vikiwa na matumaini ya kupata umeme huo kwa kuwa bado havina umeme.

Bashiru Fenyang'e, anasema awali alikuwa akiuza vifaa vya pikipiki na baiskeli tu ila sasa anatumia kifaa maalum cha umeme, kujaza upepo matairi ya pikipiki na kufunga mipira, pamoja na kuchaji simu.

Huyo imemuongezea wateja kutoka wastani wa wateja watatu zamani hadi 10 kwa sasa.

Tangu kuweka kifaa hicho, Bashiru sasa pato lake limefikia Sh. 225, 000 kwa mwezi kwa kuwakuhudumia wateja watano wa kujaza upepo kila siku anaowatoza Sh.2, 500 kila mmoja pia hupata Sh.60, 000 kwa mwezi kutokana mauzo ya kuchaji simu.




Jedwali la takwimu linaloainisha upatikanaji umeme mkoa wa Tanga.

> "Tulipokuja kufanya uchunguzi tuligundua kuwa mwananchi wa kiwango cha chini alikuwa anatumia Sh.30, 000 kwa mwezi kwa huduma iliyohitaji nishati kama vile, taa za kuchaji, mafuta ya taa na kutoa kopi, sisi tunachaji Sh. 11,000 na kumpa uhuru wa kuutumia atakavyo,"



Bashiru Fenyang'e, akionyesha kifaa cha kujaza upepo pikipiki kinachotumia umemejua. **PICHA: JENIFER JULIUS**

Uwapo wa mradi huo, pia umesaidia kuleta mwanga majumbani na kupunguza majanga yanayosababishwa na matumizi ya taa za vibatari na chemli kama ajali ya moto na kuvuta hewa chafu.

Rehema Athumani, ni mwanakijiji anayeshukuru uwepo wa umemejua, kwa kuwa sasa anapata mwanga na uhakika na watoto wake kujisomea katika mazingira salama.

"Yaani nashukuru, maana watoto wangu sasa wanajisomea hadi usiku, Hapo kabla nilikuwa nahofu wanaweza kupata maradhi ya macho kwa sababu mwanga wa kibatari ni mdogo," anaeleza Rehema.

Mradi huo pia umehamasisha ulipaji wa kodi kijijini na serikali kwa jumla. Ni hoja inayothibitishwa na Mwenyekiti wa Kijiji Cha Mpale, Augustine Mganga, anayesema mwaka jana wamekusanya jumla ya Sh.1, 702,895,040.

Hiyo ni ongezeko la asilimia 70 ya malego ya mapato kiserikali, tofauti na kabla mradi huo kuwapo, walipokuwa wanakusanya kwa wastani wa asilimia 40 ya malengo hayo kwa mwaka.

### CHANGAMOTO

Kama waswahili wasemavyo, kila jambo zuri halikosi kasoro, baadhi ya wanakijiji wanatoa malalamiko yao kuhusu gharama za umeme huo kuwa juu, wakihitajika kulipa Sh.11,000 kwa mwezi ikiwa ni kiwango cha chini kwa mteja, wao wakitamani umeme wa Wakala wa Umeme Vijijini, ambao huuzwa kwa wastani wa chini zaidi.

Yusuph saidi, anasema gharama ya Sh.11, 000 anayolipia kwa mwezi, ni kubwa kwake kwa sababu hana matumizi mengine zaidi ya kuwasha taa na televisheni.

"Ingependeza zaidi kama tungelipa kadiri tunavyotumia kama ilivyo kwenye umeme wa REA (umeme wa gridi ta taifa). Hii staili wanayotumia sasa inatunyonya," anasema.

Lakini hali ni tofauti kwa baadhi ya wanakijiji wanaokubaliana na gharama hizo za umeme wakikiri kwamba zipo sawa na zinawanufaisha.

"Kwa upande wangu naona gharama zipo sawa, kwa sababu nikishalipia ninatumia nitakavyo na mimi kupitia hii biashara yangu, namudu kulipa gharama," anasema Mahmud.

### MAMLAKA ZA UMEME

Akijibu hoja ya uhitaji wa umeme wa REA katika kijiji hicho, Meneja wa Tanesco wilaya ya Korogwe, Julius Nyamarungu anasema wanasubiri taarifa kutoka REA.

Hata hivyo, kauli hiyo inapingwa na Injinia Elineema Mkumbo, Kaimu Mkurugenzi wa Uendelezaji Teknolojia na Masoko wa REA, anayesema kuwa hawajapata mapendekezo yoyote ya kupeleka umeme katika kijiji hicho, hali inayoleta mkanganyiko.

Akizunguzia hoja ya gharama kubwa ya umeme iliyotolea na wanakijiji hao, Prosper Magari, Mkurugenzi wa Miradi kutoka Ensol, anasema wamepeleka umemejua kijijini hapo, ili kuwapunguzia gharama za matumizi ya nishati walizokuwa wanazitumia awali.

"Tulipokuja kufanya uchunguzi tuligundua kuwa mwananchi wa kiwango cha chini alikuwa anatumia Sh.30, 000 kwa mwezi kwa huduma iliyohitaji nishati kama vile, taa za kuchaji, mafuta ya taa na kutoa kopi, sisi tunachaji Sh. 11,000 na kumpa uhuru wa kuutumia atakavyo," anasema.

Hata hivyo ufadhili uliotolewa na serikari pamoja na taasisi za kimataifa umechagia kwa kiasi kikubwa kupungua kwa malipo ya umeme.

Akitoa ufafanuzi wa ufadhili uliotolewa Prosper anasema:

"Taasisi ya Energy and Environment Partnership (EEP) walitoa yuro (Euro) 263,000 (Sh.mil 689), Taasisi ya Kuendeleza Mitaji ya Umoja Mataifa (UNCDF) dola 124000 (Sh.mil 285) na sisi tulitoa asilimia 20 ya fedha za mradi ambazo ni dola 120,000 (Sh.mil 276) ", anaongeza

Ripoti ya Hali ya Upatikanaji Nishati mwaka 2016, inaonyesha asilimia 30 ya wakazi wa mkoa wa Tanga wanapata umeme wa Tanesco, huku kwa upande wa vijijini ni asilimia 19.3 tu ya kaya zote ndizo zinazopata umeme.

Kati ya kaya hizo za vijijini, zaidi ya nusu (53.7%) zinatumia umeme wa gridi ya taifa huku asilimia 44.6 ikitumia umemejua na asilimia 1.7 zinatumia vyanzo vingine vya nishati.

Katika kuhakikisha kuwa wananchi wa vijijini wananufaika na nishati ya umeme sawa na wale wa mijini, serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (Ewura), imeweka kikokotoo ambacho kitapima na kudhibiti gharama za juu.

"Tulikuwa tunawaachia wawekezaji wapange bei, lakini sasa tunatengeneza (tariff models) kikokotoo ambacho kitatusaidia kudhibiti gharama za juu ili wananchi nao wapate kunufaika na umeme," anasema Vita Laabaa, Mhandisi Mwandamizi wa Masoko ya Umeme kutoka Ewura.

ELIMU

NA MARY MOSHA, HAI

# UZINDUZI SEKONDARI MAALUM

## Kipaji cha kuandika mlemavu chamwacha Waziri Mkuu katika butwaa la simanzi

- Hadhira kimya, wengi wadondosha machozi
- Askofu: Deni la miaka 8 kanipa binti mlemavu
- Shule ya kipekee nchini kwa mahitaji maalum

"HATIMAYE ndoto yangu imekuwa ya kweli, "anatamka Askofu Mkuu wa Jimbo Katoliki Arusha, Isack Amani, mbele ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipozindua Shule ya Sekondari Jumuisho Mtakatifu Pamachius (St. Pamachius Inclusive Secondary School).

Ni tukio la majira ya saa tano asubuhi, siku ya Feb 22 mwaka huu, Waziri Mkuu Majaliwa, alipokuwa mgeni rasmi kijijini Kimashuku, katika Kata ya Mnadani, wilayani Hai, mkoa wa Kilimanjaro.

Muda mfupi kabla ya kutolewa hotuba, ushuhuda wa 'walemavu wanaweza' kutoka kwa mwanafunzi wa kidato cha kwanza, Joseph Mtei, asiyekuwa na mikono, alipoandika mambo kadhaa, ilileta butwaa na simanzi ya ghafla katika jumuiya hiyo iliyokusanyika shuleni.

Joseph, alikaribishwa na Askofu Amani na alipopewa daftari, alionyesha umahiri wa kutumia vidole vya miguu kuandika jina kamili la Waziri Mkuu Majaliwa na mkewe, pia maneno ya kumkaribisha shuleni kwao.

Mgeni huyo rasmi naye alipigwa na butwaa, iliyoambatana na simanzi, hali iliyotawala wengine wengi katika hadhira hiyo na hasa pale kazi ya mwanafunzi huyo ilipozungushwa kwa wageni tofauti.

Baadhi walidondosha machozi, huku kiongozi huyo mkuu wa shughuli za serikali akitoa maagizo makali dhidi wanaowanyima walemavu fursa za elimu na mahitaji mengine muhimu kimaisha.

Uzinduzi huo, mbali na mahudhurio ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, pia uliwajumuisha viongozi wa kiserikali na kidini nchini.

Askofu Amani, anasema Sekondari Jumuisho ya Matakatifu Pamachius, inatarajiwa kuwa pekee nchini itakayochukua wanafunzi jumuishi zaidi ya 500, huku akifafanua kwa kina hisia zake na chimbuko la mradi huo wa elimu kwa kauli:

"Sio jambo rahisi kuielezea furaha yangu wakati wa uzinduzi wa shule, licha ya kuwa haijakamilika. Lakini, tayari ina wanafunzi 74 na wanaendelea na masomo.

"Ndoto yangu ya miaka nane sasa, ilitoneshwa na mwanafunzi mmoja wa kike mwenye ulemavu wa kuona kutoka Shule ya Msingi ya Mtakatifu Francis, alipofika ofisini kwangu anisalimie na kunieleza changamoto wanazokabiliana nazo wenzao, wanapohitimu darasa la saba.

"Wakati wa kuagana naye, nikiwa Askofu wa Jimbo Katoliki Moshi, aliniuliza ... sisi walemavu tunapomaliza darasa la saba, tunaenda wapi? Je, ni shule ngapi zipo tayari kutupokea? Miundombinu yake ni rafiki kwa ajili yetu? Tufikirie na sisi Baba.

> "Maswali haya yalininyima usingizi kwa muda mrefu, nikifikiria nini cha kufanya, ili kuliokoa kundi hili. Niliwatoa baadhi ya Mapadri kwenda kwenye mafunzo maalumu ili tuweze kulisaidia kundi hili."

"Maswali haya yalininyima usingizi kwa muda mrefu, nikifikiria nini cha kufanya, ili kuliokoa kundi hili. Niliwatoa baadhi ya Mapadri kwenda kwenye mafunzo maalumu ili tuweze kulisaidia kundi hili."

Anasema, pia ukaonekana umuhimu wa kuwatafuta walimu na kuwapa mafunzo maalumu yanayokidhi kuwahudumia kundi hili kubwa na muhimu kwa jamii.



Waziri Mkuu Kasism Majaliwa, akiangalia mwandiko wa mtoto Joseph Mtei, anayetumia mguu kuandika. PICHA ZOTE: MARY MOSHA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiongea na watoto wenye ulemavu.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akisoma jina lake kwenye daftari la Joseph Mtei.

**DIRA YA UTEKELEZAJI**

Anasema mpango mkuu uliopo sasa ni kwamba, miundombinu ya shule hiyo inatarajiwa kuwa jumuishi, kwa maana ya kuruhusu watumiaji wa kawaida na wenye mahitaji maalumu, bila ya usaidizi wa mtu mwingine.

Inaelezwa itakapokamilika, shule itakuwa ya kwanza nchini kuchukua walemavu wa aina zote na Askofu Amani anaiomba serikali kuweka jicho la pili linalohakikisha kundi hilo linapata haki sawa na wanafunzi wengine.

Askofu Amani anasema, wakati wanaendelea na maandalizi hayo, hatua ya kwanza ilianza kwa kusafisha eneo shamba ekari 11 mwaka 2015, kazi iliyofanywa kwa awamu kadhaa kulingana na upatikanaji wa fedha.

"Awamu ya kwanza ilihusisha ujenzi wa madarasa manne na matundu ya vyoo 13, ambayo iligharimu Sh. million 400," anaeleza askofu na kufafanua, awamu ya pili kwamba:

"Ilihusisha mabweni mawii kwa wavulana na mawili wasichana , vyumba vinne vya wanafunzi, chumba kimoja cha matroni kwa huduma ya kwanza, pamoja na matundu 13 ya vyoo na 13 bafu na sehemu ya kufulia, ambayo yaligharimu Sh. milioni 898.6."

Kwa mujibu wa kiongozi huyo wa kanisa, kila bweni lina uwezo wa kuchukua wanafunzi 64 na awamu ya tatu iligharimu Sh. milioni 271.3.

Askofu anasema, hiyo ilihusu utengenezaji ukumbi na awamu ya nne ilikuwa ujenzi wa jengo la utawala lililogharimu Sh. milioni 180.

Pia, anaufafanua mradi wa awamu iliyofuata ambayo ni ya tano, ilihusu ujenzi wa nyumba ya Masista watoa huduma shuleni, lenye vyumba vinane, sebule, kanisa dogo, stoo na jiko lililogharimu Sh.milioni 250.

"Ujenzi wa jiko la shule ulikadiriwa kutumia Sh.milioni 120, lakini kutokana na gharama za maisha utaweza kufikia milioni 200, hii ikiwa ni awamu ya sita na saba ilikuwa uwekaji wa mfumo wa maji kwa Sh.milioni 13 na mfumo wa umeme Sh. milioni 46.9," anasema

**WAZIRI MKUU**

Waziri Mkuu Majaliwa, hakuficha hisia zake kwa mwanafunzi, anayetumia miguu kuandika, alipowaagiza watendaji wote serikalini, kuwa mstari wa mbele kuwaelimisha wananchi wasiwafiche walemavu majumbani.

"Nawaagiza watendaji wote kuhakikisha kwanzia ngazi ya Kitongoji hadi taifa, kuhakikisha hakuna mtu mlemavu atakayefichwa ndani, kwa sababu zozote zile na ikiwa atabainika na wewe hujachukuwa hatua, tambua ya kuwa hutoshi kwenye nafasi uliyopo," anasema Majaliwa.

Kiongozi huyo ambaye kitaaluma ni mwalimu, anakiri watoto wenye ulemavu wana vipaji vingi, hiyo anawataka wazazi kuhakikisha wanakuwa mstari wa mbele kuwapa nafasi za kielimu, ili wajitegemee baadaye, pia kusaidia jamii.

"Narudia, ni hali ambayo haitavumilika, pale nitabaini watendaji wangu kuanzia ngazi ya kitongoji hadi taifa wamewatelekeza na kuwavumilia wazazi walioshiriki kuwaficha watoto ndani kwa kigezo cha ulemavu. Nitawachukulia hatua za kisheria haraka iwezekanavyo," anasisitiza.

"Halmashauri simamieni kuhakikisha, ikiwa hao watoto wapo kwenye elimu na kama hawana misaada, hakikisheni wanapata mahitaji yao yatakayowasaidia kupata elimu, kama vile baisikeli, miwani, vijiti ili wapate elimu sawa na wanafunzi wengine,"anasema Majaliwa.

**PROFESA NDALICHAKO**

Katika maelezo yake, Waziri wa Elimu na Mafunzo ua Ufundi, Profesa Ndalichako, anataja hatua kadhaa ambazo wizara yake inachukua, ikiwamo kuanzisha mtaalamu maalumu kwa ajili ya wanafunzi walemavu,

Anasema, kuna haja ya lugha ya walemavu kufahamika kwa walimu, kama njia mojawapo ya kufungua fursa za kuelimika kwa kundi hilo.

Pia, Waziri Profesa Nadichako, ambaye kama alivyo Waziri Mkuu Majaliwa, kitaaluma ni mwalimu aliyekwishafundisha katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuongoza Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), anaeleza mtazamo wa mipango mingi ya serikali kuhusu kada hiyo ya walemavu.

**WALENGWA WAZUNGUMZA**

Mzazi wa mtoto mwenye ulemavu, Elizabet Mussa, anasema ikiwa serikali itaanzisha shule mbalimbali za wenye ulemavu, itawasaida kupata elimu na kuwawezesha kujitegemea, wakaachana na maisha ya kuomba na kuwa mzigo kwa jamii.

Anasifu Sekondari Jumuisho Mtakatifu Pamachius , ina uwezo mkubwa wa kuleta mabadiliko kwa jamii na anaiomba serikali, kuhakikisha inawapatia mafunzo maalumu walimu, kwa ajili ya kuwahudumia watoto wenye ulemavu nchini kote.

"Tunaiomba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, kuangalia namna ya kuanzisha mitaala ili kuwasaidia wanafunzi wote na Watanzania kujua namna ya kuwasiliana na watu wenye ulemavu, kyanzia ngazi ya awali hadi vyuo vikuu,"anasema Elizabeth

Jenipher Massawe (37), ni mlemavu wa viungo na mama wa watoto watatu, mkazi wa wilayani hapa, anaelezea changamoto anazokutana nazo, hasa za miundombinu na ukosefu wa elimu kwa waendeshaji vyombo vya moto, ikiwamo kukaidi kanuni za vivuko

JIELIMISHE



Wachumba wakiwa katika eneo la wazi Iran, utamaduni unaoelezwa kukua nchini humo. PICHA: MTANDAO

## Wapenzi wakamatwa Iran kuchumbiana hadharani

WAPENZI wawili nchini Iran, wamekamatwa baada ya kuchumbiana hadharani, huku watu wakiwashangilia.

Kanda ya video ya tukio hilo lililofanyika katika mji wa Kaskazini wa Arak, iliyosambazwa katika mtandao wa kijamii, inawaonyesha wapenzi hao wakiwa wamesimama katika mduara uliyotengezwa kwa maua.

Baada ya mwanamke kukubali ombi la mpenzi wake na kumkumbatia, watu waliokuwa karibu nao waliwashangilia kwa furaha.

Hata hivyo, wachumba hao walikamatwa muda mfupi tu baadae, wakituhumiwa kukiuka maadili ya nchi na kidini. Kuonyesha uhusiano wa kimapenzi nchini Iran, ni marufuku kisheria.

Naibu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Markazi, ambako kumetokea tukio hilo, Mahmoud Khalaji, ameliambia shirika la habari la Fars, kuwa wachumba hao wako mbaroni kwa anachokiita 'maslahi ya umma.'


Anaainisha kigezo cha kukamatwa kwao ni ukiukaji mkubwa wa maadili, ambayo umechochewa na anachokiita utamaduni wa mataifa ya Magharibi.

Ni mkasa uliozua mjadala mkali katika mitandao ya kijamii, baadhi wakiunga mkono na wengine wanabeza kitendo hicho

Mwaka jana, ofisa mmoja wa kiserikali alikamatwa, baada ya watu kunaswa katika kanda ya video, wakicheza dansi katika mji wa Mashhad.

BBC

## JE, WAJUA?



Ubongo wa binadamu unaweza kujifunza kitu chochote kile, hata kiwe kigumu namna gani, tena kwa haraka. **PICHA: MTANDAO**

# Waweza kujifunza kitu chochote kwa saa 20 tu

IWE Kirusi, Kiarabu ama Kichina au hata fizikia ya maumbo. Ubongo wa binadamu unaweza kujifunza kitu chochote kile, hata kiwe kigumu namna gani, tena kwa haraka.

Utafiti unaonesha kuwa muda bora kabisa wa kujifunza kitu ni saa 20 za awali unapokutana na somo ama ujuzi mpya.

Wakati huo kasi ya ubongo kupata uelewa ni kubwa zaidi. Kutokana na hamu ya kung'amua mapya, uwezo wa ubongo kufahamu nao huwa mkubwa.

Mwanafalsafa wa karne ya 19 nchini Ujerumani, Herman Ebbinghaus ambaye pia alikuwa ni mwanasaikolojia, ni moja ya wasomi wa mwanzo ambao walitafiti juu ya namna ubongo unavyokusanya taarifa mpya.

Kulielezea hilo, Ebbinghaus alitengeneza kile alichokiita learning curve, yaani mchirizo wa kujifunza: ama uhusiano kati ya kupata stadi mpya na muda utumikao kujifunza.

Mchirizo huo una mihimili miwili wa wima ama Y ni wa maarifa na mhimili mlalo ama X ni wa muda.

Ebbinghaus aligundua kuwa kwa saa chache za mwanzo muda mwingi zaidi ukitumika kujifunza somo jipya na ndivyo hivyo maarifa zaidi hupatikana.

Lakini baada ya muda, kasi ya kujifunza huanza kushuka: japo ukiendelea kujifunza utapata uelewa zaidi lakini si kwa kasi kama ya saa 20 za mwanzo.

Katika wakati huu wa sasa, njia hiyo iliyobuniwa na Ebbinghaus inatumika kama kipimo cha kufahamu muda muafaka wa mtu kujifunza ujuzi mpya, na katika ulimwengu wa biashara hutumika kupima kasi ya utendaji kazi.

Saa 20 za mwanzo ndizo muhimu zaidi kwenye kujifunza kutokana na hamu ya ubongo kuwa juu, lakini kadri ubongo unavyozidi kung'amua somo hilo ndivyo pia unavyochoka na kufanya kasi ya kujifunza kupungua.

Ndio maana hata somo liwe gumu namna gani, athari kubwa zaidi za kuelewa hutokea mwanzoni na kwa haraka kabla kasi kupungua.

Tafuta mbinu yako ya kujifunza:

Josh Kaufman, mtunzi wa vitabu kutoka Marekani ni muumini wa nguvu ya kujifunza haraka kwa saa za mwanzoni.

Kigezo hicho ndiyo kilikuwa msingi wa kitabu chake maarufu 'The First 20 Hours: Mastering the Toughest Part of Learning Anything' Saa 20 za Mwanzo: Kuhimili sehemu ngumu ya kujifunza kitu chochote.

Ushauri wake ni kuwa, vunja vunja somo katika vipande vinavyoweza kumeng'enyeka, na jikite katika kujifunza vipande hivyo kwa dakika 45 kwa siku, kila siku.

Hautakuwa mahiri au gwiji lakini utakapokamilisha saa 20 zako za mwanzo za kazi ngumu (ambazo utazifikisha baada ya mwezi), utakuwa umepata ufahamu wa kutosha wa somo hilo.

Na pale utakapokuwa na ufahamu wa kutosha, njia ya kuwa mbobezi inakuwa nyeupe.

Njia nyingine inayopigiwa upatu ni kanuni ya saa tano ama 'Five-Hour Rule': ambapo mtu hutakiwa kutenga saa moja kujifunza kitu kipya katika siku tano za wiki.

Benjamin Franklin, ambaye ni moja ya waanzilishi wa taifa la Marekani, alikuwa ni mmoja ya wale waliokuwa wakiutumia mfumo huo na kuupigia chapuo kwa wengine. Mfumo huo pia huitwa kujifunza kwa dhamira.

Franklin alikuwa akipanga kila siku kuanzia Jumatatu mpaka Ijumaa saa moja kujifunza kitu kipya.

Na pale alipoona kuwa ameshapata uelewa wa kutosha alihamia kwenye somo jipya. Alifanya hivyo maisha yake yote.

Kwa mujibu wa wataalamu, iwapo utatumia njia hii ya kujifunza, utapata uelewa wa stadi mpya katika kila wiki nne maishani mwako. Cha muhimu zaidi ni kuwa na muendelezo na ari. Nadharia ya kujifunza kwa dhamira inatumiwa na maelfu ya watu duniani.

Baadhi ya watu mashuhuri na wafanyabiashara wakubwa duniani wameitaja njia hiyo kama siri yao ya mafanikio. Oprah Winfrey, Bill Gates, Elon Musk, Warren Buffett na Mark Zuckerberg ni miongoni mwa watu wanaotumia mfumo huo wa kujifunza.

Ukitaka kupata maarifa na stadi mpya kunahitajika vitu viwili vikuu: ari ya kujifunza na nidhamu binafsi ya kujisukuma ili utende uyatakayo.

**BBC**

## UTAFITI

# Si lazima usubiri kwa muda mrefu baada ya kupoteza ujauzito

TATIZO la mimba kuharibika na kutoka kabla ya umri wake unaotakiwa kukamilika, limekuwa likiwasumbua wanawake wengi.

Mara nyingi wanawake wanapata hali hiyo hushauriwa kusubiri kwa angalau mwaka mmoja kabla ya kupata ujauzito tena.

Hata hivyo, hakuna ushahidi wa kimatibabu unaothibitisha ushauri huo.

Utafiti wa kimatibabu uliyofanywa kuhusiana na suala hilo na kuchapishwa katika jarida la Lancet, unaashiria hakuna haja ya mwanamke kusubiri kwa muda mrefu baada ya kupoteza ujauzito.

Mwanamama Dorothy Stephen, aliyewahi kupoteza mimba, ili kubaini ilimchukua muda gani kupata ujauzito mwingine. Dorothy anasema, alipatwa na tukio la kupoteza ujauzito wa miezi mitano mwaka 2013.

"Nilijiona na dalili ambazo si za kawaida, nikaenda kumuona daktari akanipima na kuniambia kuwa sio tatizo"

Alirudi nyumbani na kuendelea na shughuli zake za kila siku, kwa sababu daktari alimhakikishia kuwa kila kitu kiko shwari.

"Nilikuwa na safari ya kwenda mikoani na nilitumia ndege, lakini nilipofika kule nilikuwa nikienda nilijisikia maumivu makali sana," anasema Dorothy

Amelazimika kuenda kliniki mara kwa ya pili ambapo alifahamishwa kuwa yuko katika hali mbaya na kwamba anahitaji matibabu ya dharura.

"Nilizalishwa lakini mtoto alifariki saa moja baadae kwasababu viungo vyake vya kusaidia kupumua vilikua havijakua tayari kufanya kazi"

Dorothy anasema tukio hilo lilimfanya kukumbwa na hisia za majonzi na uwoga kwa muda mrefu.

Alihofia huenda akapoteza tena ujauzito hali ambayo ilimfanya kukaa karibu mwaka mmoja.

Daktari alimpatia ushauri wowote?

"Nilishauriwa na daktari nimpumzike kwa muda na kwamba nikipata ujauzito ni hakikishe nafika kliniki kwa uchunguzi wa karibu"

Licha ya ushauri huo alikaa karibu mwaka kabla mmoja kabla ya kupata ujauzito tena.

Bi Dirothy anasema kuwa alipata ujauzito tena mwaka 2015 lakini alikuwa na wasiwasi kuanzia mwanzo wa ujauzito hadi alipojifungua.

"Miezi mitatu ya kwanza nilikuwa hatari kwangu kwasababu nilikua napata dalili hatarishi"

Daktari wake alimhudumia kwa karibu na hatimaye alijifungua salama na anasema mtoto wake ambaye sasa ana miaka mitatu, amemfanya asahau majonzi aliyopata wakati alipopoteza mimba yake ya kwanza.

Nini husababisha mimba kuharibika?

Kwa mujibu wa wataalamu wa afya ya uzazi kuna sababu nyingi zinazosababisha mimba kuharibika kisha kutoka.

Umri mkubwa-kwa kawaida, mwanamke anapofikisha umri wa miaka 35 au zaidi, misuli ya mji wake wa uzazi hulegea na kupungua nguvu za kuweza kuhimili na kutunza kiumbe kinachokuwa ndani ya mji wa uzazi. Kulegea kwa misuli hii husababisha mimba kutoka kwa urahisi.

Magonjwa-wanawake wanaosumbuliwa na magonjwa kama kisukari, unene kupindukia, malaria kali, magonjwa ya zinaa na mengineyo huwa katika hatari kubwa ya mimba zao kutoka.

Hitilafu za kizazi-baadhi ya wanawake huwa na mfuko wa mimba ambao muundo wake siyo wa kawaida. Wanawake wenye tatizo hili, huwa na hatari kubwa ya mimba zao kuharibika kabla ya kutimiza umri wa miezi tisa.

Maambukizi ya bakteria au fangazi-maambukizi hayo husababisha misuli ya kizazi kushambuliwa na kisha kupoteza uwezo wake wa kuhifadhi ujauzito, jambo ambalo husababisha mimba kutoka.

Sababu nyingine ni pamoja matumizi ya pombe kali, uvutaji sigara, matumizi ya dawa za kulevya, kemikali, matatizo ya kurithi na kadhalika.

**BBC**



# ELIMU

NA YASMINE PROTACE, MKURANGA

# Diwani ajitosa kuhamasisha ufaulu wa shule za kata yake

## ■ Ajigamba kuvuna mageuzi miaka 3
## ■ Aandaa kongamano darasa la elimu

MOTISHA ni moja ya mafanikio katika kuleta mabadiliko sehemu husika na kunapokuwapo motisha katika sehemu yoyote, ushindani wa kufanya jambo unakuwa mkubwa, ili mtu anufaike na motisha hiyo.

Hivi karibuni, Diwani wa Kata ya Tengelea Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani, Shabani Manda, aliandaa kongamano la elimu lililoendana na utoaji zawadi mbalimbali kwa shule na wanafunzi waliofanya vizuri katika mitihani ya taifa mwaka jana na kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu.

Manda aliamua kufanya kongamano hilo la elimu katika kata, akiwashirikisha, wazazi, walezi, wananchi mbalimbali na viongozi wa kisiasa mkoa wa Pwani na watumishi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga.

Katika zawadi alizotoa Diwani Manda, ni pesa taslimu na anaahidi mwaka ujao wanafunzi watakaofaulu, atawasaidia kuwasomesha kwa kuwachangia vifaa vitakavyohitajika katika maandalizi ya shule.

Mbali na kuchangia pesa taslim kwa wanafunzi, pia alitoa msaada kwa mlemavu wa miguu, ikiwamo kuwapatia tanki la kuhifadhi maji.

Akizungumzia haki ya elimu katika kata yake, Diwani Manda anajigamba tangu mwaka 2015, ameweza kuleta mabadiliko makubwa katika elimu, kilimo maji miundombinu na afya ndani ya kaya yake.



Diwani wa Kata ya Tengelea, Shabani Manda (kushoto), akikabidhi baiskeli ya mtoto mlemavu (hayupo pichani) Kwa Katibu wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Pwani, Juma Ghana. **PICHA ZOTE: YASMINE PROTACE**

**MAFANIKIO**

Anasema hali ya elimu aliyoikuta mwaka 2015 katika Shule ya Msingi Dondwe, ilikuwa na walimu wanane na sasa wako walimu 12; Shule ya Msingi Tengelea, mwaka 2015 ilikuwa na 24 na sasa wapo 27; Shule ya Msingi Hoyoyo ilikuwa na walimu 16 na sasa wapo walimu wapo 21.

Pia, anasema kwamba ameshawezesha Shule ya Tengelea, kupata kisima cha Maji, Korogwa ameipatia vyumba vitatu vya madarasa na kisima kimoja katika Shule ya Msingi Hoyoyo.

Akizungumzia ufaulu, Diwani Manda anasema katika shule za kata hiyo, katika matokeo yaliyotokea hivi karibuni, ufaulu umeongezeka, akitaja shule ya Tengelea imefikisha asilimia 85; Hoyoyo asilimia 45; na Dondwe asilimia 85.

Anasema, katika matokeo kidato cha kwanza mwaka huu, wanafunzi walioмaliza katika shule ya msingi, wanne walichanguliwa kwenda shule za watoto wenye vipaji maalum.

Kuhusu changamoto, anasema kwamba kuna baadhi ya shule ambazo kwa sasa zinakabiliwa na uchakavu wa vyumba vya madarasa,walimu na upungufu wa miundombinu ya kuhudumia wanafunzi na walimu.

Mwajuma Juma, ni mmoja wa wanafunzi aliyefanya vizuri katika ufaulu wa kuingia kidato cha kwanza mwaka huu, anayekiri jitihada za diwani na walimu wao zilizaa matunda, pamoja na shule kutokuwa na umeme, walifanikiwa kuuvuta, iliyowasaidia kusoma hadi usiku.

Ofisa Elimu Msingi wa wilaya hiyo, Cosmas Magig, kwanza anazipongeza shule za kata hiyo kwa kufanya vizuri mitihani ya darasa la saba mwaka jana.

Anasema katika shule za msingi kwa darasa la nne, ufaulu usiwe chini ya asilimia 100, darasa la saba usishuke asilimia 80 na ufaulu unaposhuka, walimu wakuu husika wanachukuliwa hatua, zikiwamo kushushwa vyeo.

> Jackson anasema, kuwa watoto wasichangishwe chochote na kama kuna michango ya chakula, wazazi wanatakiwa kuitwa na kuzungumzia gharama hizo za chakula.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Tengelea, Abeid Msemwe (kushoto), akikabidhiwa tangi la maji na diwani wa Kata ya Tengelea, Shabani Manda.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Mkuranga, Akimu Jackson, katika kongamano hilo ana maoni: "Siri ya mafanikio ya maendeleo ya mtoto katika shule yoyote ni mzazi au mlezi kufuatilia maendeleo ya mtoto wake katika shule anayosoma."

Anasema, pia wazazi wanapaswa kushirikiana na walimu, ili kuwawezesha kuwa na urafiki na kumuwezesha mwalimu kuwa na moyo wa kutoa elimu bora kwa mtoto huyo.

Kwa mujibu wa Jackson, baadhi ya wazazi na walezi huwa hawafiki shule kuona maendeleo ya watoto wao na hawashiriki katika mikutano, hali inayochangia mzazi kushindwa kujua mwenendo wa mtoto wake shuleni.

Jackson anampongeza Diwani Manda, kwa kuandaa kongamano la elimu na kuwapatia zawadi wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo yao katika mtihani wa mwaka jana, hata wakafanikiwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu.

Pia, anawataka madiwani kumuiga Manda, ili kuongeza idadi ya ufaulu kila mwaka katika kata zao.

Akizungumzia dhana ya 'elimu bure' anasema kuwa, kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule ana haki ya kusoma, hivyo ni jukumu la wazazi kuhakikisha wanafunzi wanasoma bila ya kubughudhiwa.

Pia, anawaonya walimu watakaojihusisha na kuwachangisha wazazi, wakati serikali imeshatamka elimu kutolewa bure kwa watoto shuleni.

Jackson anasema, kuwa watoto wasichangishwe chochote na kama kuna michango ya chakula, wazazi wanatakiwa kuitwa na kuzungumzia gharama hizo za chakula.

Anasema mtoto atakayeonekana kuwa na tatizo la sare, yaani zimechanika, ni marufuku kwa mwalimu kumfukuza shule, bali kinachotakiwa ni kumuita mzazi kujadili naye suala hilo na kutafuta namna ya kumsaidia.

Pia, anawataka wajitahidi chochote kwa watoto ambao wanafanya vizuri katika mitihani, hatua itakayosaidia kuongeza ufaulu wa kila mwaka.

"Kuna baadhi ya wazazi wanashindwa kuwapongeza watoto wao kwa zawadi, lakini kinachoshangaza wanatumia fedha nyingi kwenda kuwatunza watu ambao wana shuhuhuli za 'kicheni pati' na arobaini (sherehe za mtoto mchanga kutolewa nje), " anasema.



WADAU
**SABATO KASIKA**

# KWA sasa majoho yanavaliwa hata na wahitimu wa ngazi za chini katika elimu, lakini Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, amewahi kuchukua hatua ya kupiga marufuku utaratibu huo.

Wadau wanasemaje?



**AMOS KASELA (MWANAFUNZI CHUO KIKUU ST. AUGUSTINO MWANZA)**

MAJOHO ni mavazi yanayofunika mwili kuanzia shingoni hadi chini ya magoti na kofia yake. Kwa jina lingine yanaitwa magauni. Mavazi haya yanavaliwa na watu mbalimbali kuonyesha hadhi na mamlaka walionayo.

Mavazi haya huvaliwa na watu kama wafalme, waamuzi/majaji, wanasheria, wanafunzi wanaohitimu kozi za ngazi mbalimbali. Hapa ngoja niongelee majoho kwa wanafunzi wanaohitimu, tumezoea kuona yakivaliwa na wahitimu wa vyuo wa ngazi mbalimbali kama vile astashahada, atashahada kwanza, shahada ya uzamili, stashahada ya uzamili na shahada ya uzamivu.

Majoho haya huwa yana alama au mshono unaotambulisha ngazi moja tofauti na nyingine. Elimu ni moja ya vitu vigumu sana kuvipata, hivyo mtu anayehitimu hatua moja kwenda nyingine ni jambo la heri na faraja kuvaa joho. Elimu ya ngazi yoyote iwe chekechea, msingi au sekondari ina manufaa kwa yule aliyeipata na jamii inayomzunguka, hivyo kwa maoni yangu ni sahihi kwa mwanafunzi aliyehitimu masomo katika hatua ya shule ya awali, msingi au sekondari kuvaa joho ili kusherehekea hadhi hiyo ya elimu.

Katika jambo hilo kunatakiwa kuwapo na utaratibu wa kurasimisha mavazi ya wahitimu, ili yawe tofauti kutoka ngazi moja ya elimu hadi nyingine, ili kusiwapo na mkanganyiko wa mhitimu wa ngazi fulani kuvaa joho ambalo siyo stahili yake.



**SUZAN LYIMO (MWALIMU NA MKAZI WA DAR ES SALAAM)**

KWANZA, kabisa hili suala la majoho kuvaliwa na watoto wa elimu ya chini linatakiwa kuchukuliwa kama jambo la kawaida, kwa sababu sidhani kama lina athari zozote kwenye elimu. Kwa nchi, zilizoendelea hawana tatizo nalo, kwa maana hiyo ni muhimu kutambua kwamba dunia hii ya utandawazi haya mambo ya majoho kwa wenzetu wa Ulaya, watoto wa shule za awali wanapohitimu wanavaa majoho.

Joho lile kwa vyuo vikuu linamaanisha kuhitimu elimu zote na kwamba hakuna shule tena mbele hasa ikizingatiwa hata shahada za uzamili na shahada za uzamivu zilikuwa nadra hapa nchini wakati huo tulikuwa na chuo kikuu kimoja tu.

Sasa shule za binafsi ni nyingi, kwa hiyo jambo kubwa ni uwezo pia wa kifedha. Ieleweke kuwa hayo majoho yana gharama kubwa. Kwa hiyo kwangu mimi sioni shida ila hayo mahafali yaende sambamba na uelewa na ubora wa elimu.

Ninasema hivyo kwasababu tumekuwa tukishuhudia uanzishwaji wa shule nyingi za awali ambazo baadhi yake wanafunzi wanaohitimu hawana uwezo wa darasani, nao wanavalishwa majoho ya kuhitimu, lakini kama ubora wa elimu utazingatiwa, uvaaji wa majoho utakuwa na maana zaidi kwa wahusika kuliko kuvalishwa tu huku wakiwa hawajui lolote. Maana yangu ni kwamba majoho yaendelee kuvaliwa lakini pia shule zijitahidi kuboresha elimu ili watoto wanaohitimu watoke wakiwa na kitu cha kujivunia wanapokwenda kwenye hatua nyingine ya elimu.




**JUDITH MREMI (MWALIMU SHULE YA SEKONDARI MNAZI MMOJA, DAR ES SALAAM)**

KITENDO cha kila mwanafunzi kuvaa joho, wakati wa kuhitimu ngazi fulani ni sawa na kulishusha hadhi vazi hili, pia linapunguza hamasa kwa wanafunzi kusoma kwa bidii, kwani hudhani kwamba wameshafika hatua ya kuvaa joho. Maoni yangu ni kwamba, ili kurudisha hadhi ya joho kwa wahitimu wa vyuo wa stashahada, shahada na uzamivu, vazi hilo livaliwe na wanavyuo tu. Hii itawasaidia watoto au wanafunzi wa ngazi ya chini kwa ujumla wao, kutamani kufikia malengo yao ikiwa ni pamoja na kufikia hatua ya kuvaa vazi hilo.

Vilevile wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wangevaa sare zao za shule katika mahafali yao kuliko kuwapa majoho wakati hawajafikia elimu ya chuo kikuu. Kwa maana nyingine, niseme kwamba kila ngazi ya elimu iwe na mavazi yake kwenye mahafali.

Majoho yamezoeleka kuwa ni ya wanafunzi wa vyuo vikuu, sasa yanapotumiwa pia na wa ngazi ya chini, ninaona ni kama kuyashusha hadhi yake. Huo ndio, mtazamo wangu kuhusu matumizi ya majoho katika mahafali ya shule za awali, msingi na sekondari.



**WOKOVU KITULE (TAWALA NA MWAJIRI MAPAMBANO YA KIFUA KIKUU NA UKIMWI)**

MAJOHO kuvaliwa na kila mhitimu wa ngazi zote za elimu ninadhani siyo vibaya ingawa kungekuwa na utaratibu maalumu wa kiutambuzi. Pia, ingekuwa na vyema zaidi kukawa na rangi maalumu ya kusaidia utambuzi huo, kama rangi fulani ikivaliwa ni mhitimu wa ngazi fulani ya elimu bila kujali ni shule au ni chuo gani.

Kwa mfano rangi nyeusi na kofia nyeupe, ni rangi ya joho linalovaliwa mhitimu wa digrii ya kwanza na joho la bluu bila kofia ni la mhitimu wa darasa la saba. Huo ni mfano tu.

Ninadhani hiyo ingesaidia kwa sehemu kubwa kuondoa huo mkanganyiko, ambapo kiukweli, watu wengi ni vigumu kutambua kwa sasa ya kwamba joho lipi na la rangi gani linastahili kuvaliwa na mhitimu wa ngazi ipi.

Njia hiyo itasaidia kumaliza mkanganyiko huo ambao kimsingi unaweza kumalizwa ili kila upande uwe na vazi lake wakati, wa kuhitimu elimu ya ngazi yoyote ile, ingawa ni kweli kwamba kwa muda mrefu majoho yamekuwa yakitumiwa na wahitimu wa vyuo vikuu, lakini sasa hata ngazi za chini kuanzia shule za awali hadi sekondari zinayatumia kwa nia njema tu kama ilivyo kwa wahitimu wa vyuo vikuu.



**DISMAS LYASA (MTALAAMU WA SAIKOLOJIA KATIKA TAASISI YA GLOBAL SOURCE WATCH DAR ES SALAAM)**

MIMI sioni kama kuna ubaya kwa wanafunzi wa shule za awali au za msingi kuvaa majoho, kwani kisaikolojia jambo hili halina athari yoyote, kwa watoto wala kwa wakubwa walioko kwenye vyuo vikuu, kwa sababu hata vyeti na nguvu zao katika jamii vipo tofauti.

Hawa wengine ni watoto ambao bado wanaendelea kuwa tegemezi, lakini hao wengine wanapaswa sasa kuanza kulitumikia taifa, kwa maana ama ya kuanza miradi yao au kuajiriwa. Sijajua ni nani hasa anayeumia kwa hili, lakini ninafikiri lililo la msingi ni kwa elimu yenyewe kuboreshwa.

Kwa mfano, kuwafanya wahitimu vyuoni kuajirika au kuwa na uwezo wa kujiajiri, suala la majoho ni dogo na halina maana kwa taifa. Nimekuwa nikifuatilia mataifa mengine yakoje, wengi hawana shida na majoho, yeyote anaruhusiwa iwe ni mtoto wa chekechea au yule anayehitimu chuo kikuu.

Nafikiri kama kuna hoja, basi tujadili kuhusu mavazi kwa ujumla, kwamba kuna watu siku hizi wanavaa nguo za kwenda kuogea na wanatembea nazo barabarani, lakini suala la majoho halina shida. Itakuwa tu kama chekechea nazo zitaitwa vyuo vikuu na kupewa vyeti vya vyuo vikuu wakati wao ni chekechea.





# Walimu sekondari waibua mazito wazazi kukwepa majukumu

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WALIMU wa Shule ya Sekondari Nsongwe Juu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya wamewalalamikia baadhi ya wazazi wa wanafunzi kwa kushindwa kuwapatia watoto wao wa kike mahitaji muhimu ikiwamo nguo za ndani.

Walitoa kauli hiyo jana na kudai kwamba asilimia 90 ya wanafunzi wa kike shuleni hapo hawavai nguo za ndani, jambo ambalo lina hatarisha afya zao na pia kuwafanya wasisome kwa utulivu pale wanapokuwa kwenye siku zao za hedhi.

Akizungumza na Nipashe, mwalimu wa afya shuleni hapo, Ramla Lui, alisema kuwa wazazi wengi wanawanunulia watoto wao mahitaji ya shule kwa maana ya vitu vya kutumia darasani lakini hawajali kuwanunulia mahitaji yao binafsi hususan mavazi.

**Wazazi wamekuwa mbali na watoto wao, kwa sababu hawawapatii elimu ya kujisitiri hasa pale wanapoanza kupata hedhi kutokana na kutokuwa na nguo za ndani na pedi.**

Alisema hali hiyo inaathiri mazingira ya watoto hao kusoma kwa utulivu na kuwaweka katika hatari ya kupata maradhi ya aina mbalimbali.

"Wazazi wamekuwa mbali na watoto wao, kwa sababu hawawapatii elimu ya kujisitiri hasa pale wanapoanza kupata hedhi kutokana na kutokuwa na nguo za ndani na pedi."

Alisema utaratibu wa kuwakagua watoto wa kike mara kwa mara umesaidia kubaini changamoto mbalimbali zinazowakabili ikiwamo kubeba jukumu la kujitafutia mahitaji ya shule kwa kufanya vibarua.

Tumekuwa na utaratibu wa kuwakagua watoto wa kike, tumeona wengi wao hawavai chupi badala yake wanavaa kaptula ambazo ni kubwa, tulibaini hali hiyo tulipowaita wazazi kuwaeleza, lakini mwitikio wake umekuwa mdogo kwa kuwa wengi hawajatekeleza na kuwaachia watoto wajinunulie wenyewe.

Miongoni mwa wanafunzi hao walidai wazazi hawana muda wa kukaa karibu nao kusikiliza au kujua mahitaji yao badala yake wamejikita zaidi kwenye shughuli za kilimo.

Miongoni mwa wanafunzi hao, Elemetia Mashazo wa kidato cha kwanza alisema wazazi wake hawajawahi kumnunulia nguo za ndani badala yake hulazimika kufanya vibarau ili kujinunulia nguo za ndani kama vile chupi.

Elementia alisema hulazimika kufanya vibarau kujinunulia nguo za ndani kwa sababu wazazi wake hawana utaratibu huo na kwamba mwaka huu tayari alikwisha nunua chupi mbili na atajitahidi kuongeza na nyingine ili kukidhi mahitaji kama walimu walivyoelekeza kuwa kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na chupi tano na taiti tano.

Mwenyekiti wa vituo vya taarifa na maarifa wilayani Mbeya, Flora Mlowezi, alisema katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani wamezindua kampeni ya ulinzi wa mtoto dhidi ya ukatili wa kingono shuleni.

Alisema lengo la kuzindua kampeni hiyo shuleni ni kuongeza na kujenga nguvu za pamoja ya ulinzi wa mtoto dhidi ya ukatili wa kingono na kuhakikisha kila mtu katika jamii anajisikia kuwajibika kumlinda mtoto.

Aliongeza kuwa kampeni hiyo itamjenga na kumpa ujasiri mtoto wa kike kuripoti bila woga vitendo mbalimbali vya ukatili pindi wanapofanyiwa.

"Tumeamua kuanzisha kampeni hii ili kumlinda mtoto wa kike dhidi ya vitendo vya ukatili, tunaimani itasaidia kuibua na kuripoti masuala hayo pindi yanapotokea na lengo letu ni kuhakikisha jamii inaguswa na tatizo la ukatili wa kingono dhidi ya watoto wakiwa ndani na nje ya shule," alisema Flora.

Aidha, aliitaka serikali na vyombo vya dola kusimamia kikamilifu Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 kikiwamo na kipengele cha kuthibiti uchawi namba 12 ambayo imeainisha adhabu kwa watu wanaondesha vitendo vya kishirikina vinavyoweza kuwadhuru watoto.

Mwenyekiti wa klabu ya genda katika Shule ya Nsongwe Juu, Faines Jackson ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha tatu alisema vitendo vya ukatili wa kingono bado ni changamoto kwa kuwa vimesababisha baadhi ya wanafunzi wenzao kukatishwa masomo.

Alisema kupitia klabu hiyo wataweza kupeana elimu ya masuala mbalimbali ya ukatili wa kijinsia na kuungana kwa pamoja kukemea vitendo hivyo.

## Huruma ya wazazi yatajwa kikwazo kwa mtoto wa kike

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

VITENDO vya wazazi kuwahurumia watuhumiwa wanaowapa mimba wanafunzi wa kike na kuamua kufanya mazungumzo kwa ngazi ya familia bila kuwafikisha kwenye vyombo vya dola, imetajwa kuwa chanzo cha watoto wa kike kukosa haki ya kupata elimu na usawa wa kijinsia kwenye jamii mkoani Mbeya.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanamke Duniani ambayo kimkoa yalifanyika katika mji mdogo wa Makongorosi wilayani Chunya, Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, alisema mkoa huo ni miongoni mwa mikoa inayoongoza nchini kwa kuwa na mimba nyingi za ututoni.

Alisema katika utafiti wake aligundua familia nyingi zinafanya mazungumzo na wanaume waliowapata mimba wanafunzi, wakishinikiza kupewa mahari ili suala hilo walimalize.

Alisema kitendo hicho ni cha kumdhulumu mtoto wa kike kupata haki yake ya kielimu licha ya familia kutaka kunuifaika, aliitaka jamii kubadilika na kuachana na mtindo huo ambao unalenga kumkandamiza mtoto.

"Wazazi wamekuwa chanzo cha wanafunzi wa kike kushindwa kutimiza ndoto zao hii inatokana na tamaa za kupata mali haraka na kusahau wajibu wao na kuwaachia huru wanaume wanaowapa mimba mabinti," alisema Chalya.

Aidha, mgeni rasmi kwenye maadhimisho hayo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson alikemea vikali tabia ya wanaume kufanya ngono na watoto wa kike akiwataka kuwaacha wasome ili wafikie malengo yao.



Mshauri katika taasisi ya vijana isiyo ya kiserikali ya AfriYAN, Shadrack Msuya, akiwasilisha utafiti kuhusu afya ya uzazi kwa vijana, wakati wa semina kwa waandishi wa habari jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU.**

## Mradi wa umeme kugharimu dola mil.450

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI kupitia Shirika la Umeme nchini (Tanesco), imepokea fedha zaidi ya dola za Marekani milioni 450 kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa njia kubwa ya umeme wa msongo wa kilovoti 400 kuanzia mkoani Iringa kupitia Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Tanesco, Alexander Kyaruzi, aliyasema hayo jana, wakati alipotembelea eneo lililoandaliwa kwa ajili ya kujenga kituo cha kupozea umeme huo jijini Mbeya.

Alisema lengo la mradi huo ni kuunganisha gridi ya taifa na nchi za Kusini mwa Bara la Afrika ili ziweze kuuziana umeme pale itakapotokea kuna nchi ina upungufu wa nishati hiyo.

"Tayari tumeshapokea fedha kiasi cha dola za Marekani milioni 453 kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kujenga kipande cha njia ya umeme mkubwa kuanzia Iringa hadi Tunduma ili tuunganishe gridi yetu ya taifa na nchi za Kusini mwa Afrika," alisema Kyaruzi.

"Tukishafika Tunduma tutaendelea hadi Sumbawanga ili na wao tuwaunganishe na gridi ya taifa kwa sababu hivi sasa wanatumia umeme tunaounuua kutoka nchini Zambia," aliongeza.

Kyaruzi alisema kuwa mradi huo ni mwendelezo wa mpango wa serikali kuunganisha njia za umeme wa Tanzania na nchi jirani kwa lengo la kufanya biashara ya kuuza nishati hiyo pale ambapo nchi itazalisha ziada na pia kurahisisha ununuzi wa nishati hiyo endapo ikitokea taifa lina upungufu.

Alisema mbali na kuuza ama kununua, miundombinu hiyo, inaweza kutumika kusafirisha umeme unaonunuliwa kutoka taifa moja kwenda taifa lingine kupitia Tanzania na nchi ikapata fedha kupitia tozo zitakazolipwa.

Meneja mwandamizi wa miradi kutoka makao makuu ya Tanesco jijini Dar es Salaam, Emmanuel Manilabona, alisema baada ya kupokea fedha hizo, Tanesco imeanza mchakato wa manunuzi na kuwapata makandarasi kwa ajili ya utekelezaji.

Alisema mchakato huo utachukua muda mrefu kidogo, lakini akadai makandarasi wakishapatikana ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kuanza rasmi mwezi Januari mwakani.





# Dk. Gwajima atoa agizo kamati huduma za afya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu anayeshughulikia Afya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Dorothy Gwajima, ameziagiza Kamati za Huduma za Afya Mkoa (RHMT) na Wilaya(CHMT), kuhakikisha zinasimamia kwa weledi huduma zinazotolewa katika vituo vya afya nchini.

Gwajima, aliyesema hayo alipokuwa katika ziara ya kikazi ya kukagua utendaji wa vituo vya afya vya Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma.

Dk. Gwajima alisema kuwa ni kazi ya kamati za kutoa huduma za afya nchini kuhakikisha wanasimamia kwa umakini mkubwa huduma ambazo zinapaswa kutolewa kwa wananchi.

"Serikali imejenga miundombinu ya afya nchini kwa sasa, lakini wananchi wanachohitaji ni uhakika wa huduma bora za afya ambazo zinakidhi mahitaji yao, hivyo ni vyema kamati hizo zikahakikisha huduma zinaboreshwa katika vituo vyote vya afya nchini," alisema Dk. Gwajima.

**Tunatambua nchi yetu inataka kufikia uchumi wa viwanda wito wangu kwa serikali itukusanye wanafunzi sisi wenye bunifu zetu mbalimbali za kusaidia kufikia azima hiyo.**

Dk. Gwajima alifafanua kuwa watoa huduma za afya wote nchini wanatakiwa kutumia taaluma walizonazo katika kuwahudumia wananchi ili kupunguza malalamiko yanayotolewa katika sekta ya afya.

"Watoa huduma za afya nchini wanapaswa kuhakikisha wanakuwa wazalendo, kuwa na huruma na wagonjwa ili kujenga imani kwa wananchi kwa kuwa huduma za afya zimeboreshwa,"alifafanua.

Alisema kuwa kuwapo kwa miundombinu ni jambo la muhimu sana, lakini ifike mahali ambapo sekta ya afya ijitathmini kwa kina kama kweli inatoa huduma stahiki kwa jamii hasa katika utendaji kazi, hivyo ni wajibu wa kila mmoja kuhakikisha anatumia weledi katika utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

Aidha, alisema kuwa miundombinu ya vituo vya afya nchini imeboreshwa kwa kiwango kikubwa kinachohitajika ni mabadiliko katika utendaji kazi hasa katika utoaji wa huduma kwa jamii ili vituo vya serikali visiwe magofu.

"Ili kuongeza idadi ya wateja katika vituo vya afya nchini lazima kuwapo na ukarimu, lugha nzuri kwa mteja, uwajibikaji bila kusahau uzalendo ambavyo hivi vyote vitaleta chachu katika matokeo bora kwenye utoaji huduma za afya kwa jamii," aliongeza Dk. Gwajima.

Pia aliviagiza vituo vyote vya afya nchini kuhakikisha wanakuwa ma mpango kazi ambao utawaongoza na kuwawezesha kufanya tathmini ya kilichofanyika kutafutiwa ufumbuzi ili kufikia malengo waliojiwekea kama kituo.

Aidha, ameagiza kudumisha uhusiano mzuri baina ya watumishi katika ngazi ya zahanati, kituo cha afya, halmashauri, mkoa na wizarani kwa kuwa mabadiliko yakifanyika kutaongeza uwajibikaji na utoaji wa huduma bora utaongezeka.



Mwenyekiti wa Taifa wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Heri James (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu mikakati mbalimbali ya umoja huo. Wengine ni Makamu Mwenyekiti wa umoja huo, Tabia Mwita (kushoto) na Katibu Mkuu, Raymond Mwangala. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Walimu wakabidhi mifuko 130 ya saruji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amepokea msaada wa mifuko 130 ya saruji kutoka Shirikisho la Walimu Wazalendo Mkoa wa Dodoma ikiwa ni mchango wao katika kuunga mkono juhudi za serikali katika sekta ya elimu.

Akipokea mifuko hiyo jijini hapa Waziri Jafo, aliwapongeza walimu hao kwa moyo walionao wa kujitoa bila kujali hali ya kipato chao pamoja na changamoto nyingine zinazowakabili.

"Niwapongeze sana kwa hiki mlichokitoa kwa moyo wenu wa kujitolea katika sekta hii ya elimu, mmetambua changamoto zilizoko na mkaona mtoe mchango wenu ili muunge mkono juhudi za serikali za kuinua kiwango cha elimu nchini kupitia shule za serikali, niwashukuru sana," alisema Jafo.

Aidha, alisema katika kuinua kiwango cha elimu nchini kupitia shule za serikali, wanaendelea kuboresha miundombinu, ufundishaji wa wanafunzi ili kuzifanya shule hizo kuongoza katika mitihani ya kuhitimu elimu ya msingi na sekondari.

Alisema kasi waliyonayo anaimani matokeo ya kidato cha sita mwaka 2020 kati shule 10 za kwanza, shule saba zitakuwa za serikali.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Dodoma, Anthony Mavunde, alisema hatua waliyoifikia walimu hao inatakiwa kupongezwa na kila mtu anayependa maendeleo katika sekta ya elimu.

Hata hivyo Mavunde aliahidi kutoa mifuko mingine 70 ya saruji ili kuongezea kwenye mchango wa walimu hao ili kufikia 200 na kuwataka wadau wengine kujitokeza kuunga mkono juhudi za serikali.

Mwenyekiti wa shirikisho hilo, Mwalimu Wenslaus Mazanda, alisema wameanza kujipanga kupandisha kiwango cha elimu katika mkoa wa Dodoma kutoka nafasi za tano za mwisho ambayo imekuwa ikishika katika mitihani ya darasa la saba kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo.

Alisema wamepanga kufanya kongamano litakalo wakutanisha walimu ili kujadili suala hilo ili kuweza kuuutoa mkoa wa Dodoma katika nafasi za mwisho katika ufaulu.

# Wajane wafundwa kijikwamua kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WANAWAKE wajane wa Mkoa wa Dodoma wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali ili waweze kujikwamua kiuchumi ili kuendsha familia zao.

Mafunzo hayo yametolewa na chama cha wanawake wa Tasnia ya Filamu Tanzania (CWTF) kwa wajane mkoani hapo, huku kikiwataka kuacha kutumia vibaya fedha za mikopo wanazozipata kwa kununua vitu vya anasa.

Akizungumza jijini hapa wakati akitoa mafunzo hayo katika kongamano la 'Mwanamke Zinduka', Mkurugenzi wa Taasisi ya kuwezesha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu (YEMCO –Vicoba) Mohamed Bassanga, alisema wapo ambao wanapenda kuonekana kwa watu bila kuangalia hali yao kiuchumi.

"Unakuta mtu kavaa wigi la Sh. 300,000 halafu hana hata biashara ya Sh. 200,000, tusipende kuishi maisha kiutajiri wakati uwezo wetu ni mdogo, hiyo hela ukiitumia kuanzisha biashara yako itakusaidia katika maisha yako."

Bassanga aliwataka wanawake kujiamini kuwa wanaweza kufanya kila kitu, huku akisisitiza suala la kuwa na mtizamo linganifu ambao utamwezesha mtu kufanya shughuli zake bila kujiona yeye ni bora kuliko wengine.

Kwa upande wake mwenyekiti wa chama hicho, Vanitha Omary, alisema wameamua kutoa mafunzo hayo ili kuwanyanyua wamawake hao na kuwawezesha mitaji kupitia mfumo wa Vicoba.

Hata hivyo amesema ni mara ya kwanza kutoa mafunzo hayo na lengo ni kuwafikia wanawake wajane Tanzania nzima, huku wakiamini kupitia mafunzo hayo yatasaidia kuwatoa hatua moja hadi nyingine katika kujiinua kiuchumi.

Naye mwigizaji wa wa filamu nchini, Snura Mushi, akizungumza na waandishi wa habari wakati wa mafunzo hao aliwataka wanaume kuacha tabia ya kumnyima uhuru mwanawake kujishughulisha katika mambo ya ujasiriamali.

"Wapo wanaume ambao hawataki wake zao wajishughulishe na ujasiriamali au unakuta kama mwanamke anafanya kazi mwanaume anamwambia aache kazi, nyie wanaume tambueni kuwa kuna leo na kesho, ukiwa haupo mkeo atapata shida ya kulea watoto, acheni tabia hiyo ya kizamani," alisema.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo Sharifa Maganga alisema elimu aliyoipatia ataitumia vyema katika biashara yake anayofanya ya mboga mboga ili kukuza mtaji wake.





## Tamwa yazindua timu ya wanaume wa mabadiliko

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa), Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, amesema wamegundua kuwa kikwazo cha mwanamke katika kupata mabadiliko ni wanaume, hivyo wamezindua timu ya wanaume wa mabadiliko.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa timu hiyo huko ofisini kwao Tunguu, alisema kuwa timu hiyo itaenda kutoa elimu kwa jamii kuhusu mifumo dume, mila potofu na mifumo kandamizi dhidi ya wanawake ambayo imekuwa ikirejesha nyuma maendeleo ya wanawake.

Alieleza kuwa mwanamke anakazi nyingi katika jamii, hivyo lazima heshima, nafasi yake na uwezo wao kuonekana na kuthaminiwa.

Aidha, alieleza kuwa ushiriki wa wanawake ni mdogo walioshiriki kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, hivyo timu hiyo itaenda kufanya kazi kwa jamii kuwahamasisha wanawake ili idadi hiyo kuongezeka.

Alieleza kuwa kati ya wanawake 85 waliotangaza nia ya kugombea nafasi mbalimbali za uchaguzi na kuwapa mafunzo, wanawake 10 tu ndio waliofanikiwa kushinda kwa nafasi za ubunge, uwakilishi na udiwani.

Dk. Mzuri alisema kuwa bado hawajaridhishwa na kiwango hicho na ndio maana wameanza harakati mapema ili kuhakikisha katika uchaguzi ujao wa mwaka 2020 wanawake wengi wanajitokeza kugombea nafasi majimboni na kushinda.

Mkurugenzi huyo aliwapongeza wanawake wote waliothubutu kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi uliopita akiwamo Balozi Amina Salim Ali ambaye aligombea nafasi ya urais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania katika uchaguzi uliopita.

Akizindua timu hiyo ya wanaume wa mabadiliko, mwanachama mkongwe wa Tamwa Ummie-Mahfoudha Alley Hamid, alisema kuwa suala la uongozi halina jinsia, hivyo jinsia zote zinahaki sawa katika kugombea nafasi hizo.

# Wakulima Tumbatu walia wanyama waharibifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKULIMA wa Kisiwa cha Tumbatu Kaskazini Unguja, wamesema kuwa wanyama waharibifu wa mazao wamekuwa wakirejesha nyuma shughuli za kilimo.

Wakizungumza na Nipashe huko Tumbatu, walisema kuwa wanyama hao waharibifu ni pamoja na kima ambao wamekuwa wakishambulia mazao na kusababisha hasara.

Akizungumza kwa niaba ya wakulima wenzake, Juma Haji, alieleza kuwa kila wanachokipanda kimekuwa kikishambuliwa na wanyama hao na kurudisha nyuma jitihada zao katika kilimo.

**Ni kweli wakulima wanaathirika sana kutokana na wanyama hao waharibifu kwa kuwa hawana cha kukivuna.**

Alieleza kuwa wanyama hao wapo kwa muda mrefu kisiwani humo na hawana cha kufanya ili waweze kuwatokomeza.

"Kama unavyoona mazingira ya kisiwa chetu kimezungukwa na bahari na shughuli kubwa ni uvuvi na kilimo, lakini kwenye kilimo hatuna tunachokipata maana tunatumia nguvu nyingi, lakini hakuna manufaa," alieleza.

Aidha, alisema kilimo chao ni cha maweni ambacho ni kigumu na wanyama hao wanakatisha tamaa kuendelea na shughuli hizo.

Naye Katibu Tawala wa Wilaya ndogo ya Tumbatu, Khatib Habibu, alisema idadi ya wanyama kisiwani hapo ni kubwa zaidi kuliko idadi ya watu wanaoishi katika kisiwa hicho.

Alieleza kuwa kisiwa hicho kina wakazi wapatao 21,000, lakini idadi ya kima hao ni zaidi ya idadi hiyo ya watu na wamekuwa wakirejesha nyuma juhudi za kilimo.

Alisema kuwa kila msimu wa kilimo wamekuwa wakifanya zoezi la kuua wanyama hao na huua kima zaidi ya 500 lakini bado wapo wengi.

"Ni kweli wakulima wanaathirika sana kutokana na wanyama hao waharibifu kwa kuwa hawana cha kukivuna," alieleza.

Aidha, alisema kuwa kitendo cha kufanya zoezi la kuwaua kima hao kila kipindi cha kilimo kimekuwa kikilalamikiwa na jumuiya za kutetea haki za wanyama.



Wananchi wakipita kwenye daraja linalounganisha eneo la Mwananyamala kwa Manjunju na Tandale jijini Dar es Salaam jana, ambalo linahitaji ukarabati haraka kutokana na kuharibiwa na mvua zinazoendelea kunyesha jijini. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# Bunge la Afrika Mashariki sasa laja kivingine

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

BUNGE la Afrika ya Mashariki linakusudia kuwasilisha muswada wa kupambana na rushwa ikiwa ni moja ya hatua za kuunga mkono juhudi zinazochukuliwa na viongozi wa nchi hizo wanachama.

Mwenyekiti wa kamati za Bunge la Afrika ya Mashariki, George Odongo, akizungumza kwa niaba ya Spika wa Bunge hilo alisema Bunge limefurahishwa na juhudi zinazochukuliwa na viongozi wa nchi hizo katika mapambano dhidi ya rushwa.

Alisema rushwa ni tatizo kubwa ambalo limezorotesha shughuli nyingi za kiuchumi na maendeleo ikiwamo wananchi kushindwa kupata haki za msingi za kijamii na kimaendeleo.

Aliongeza kuwa njia pekee ya kukomesha mapambano hayo ni Bunge la Afrika ya Mashariki kuwasilishwa muswada ambao utaunga mkono juhudi zinazochukuliwa na viongozi wa nchi za Afrika ya Mashariki.

Alisema tayari juhudi za mapambano ya rushwa zimechukuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, John Pombe Magufuli, ambaye katika nyakati tofauti alifanya marekebisho mbalimbali katika mamlaka ya kupambana na rushwa (Takukuru).

Alisema kwa upande wa Zanzibar Rais Ali Mohamed Shein, ameunda Taasisi ya Kupambana na Rushwa (ZAECA), ambayo imepewa uwezo wa kushughulikia suala hilo.

"Bunge la Afrika ya Mashariki limefurahishwa na juhudi zinazochukuliwa na viongozi wa nchi hizo katika mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi ambayo lengo ni kuwawezesha wananchi kupata huduma muhimu za jamii," alisema.

Alieleza kuwa muswada wa kupambana na rushwa unatarajiwa kuwasilishwa na Mbunge Victor Burikukiye ambaye alisema maandalizi ya muswada huo yamekamilika.

Alisema anakusudia kuwasilisha muswada huo kwa ajili ya kuunga mkono juhudi za viongozi wa nchi za Afrika ya Mashariki katika vita dhidi ya rushwa.

Aliongeza kwamba ni muhimu kuunga mkono mapambano hayo kwa sababu athari za rushwa kwa kiasi kikubwa hurudisha nyuma juhudi za uwekezaji wa nchi na miradi ya kiuchumi.

"Mchakato wa matayarisho ya muswada wa kupambana na rushwa upo katika hatua za mwisho ingawa siwezi kusema utawasilishwa katika kikao kipi cha Bunge," alisema.

Kuhusu sarafu moja katika nchi wanachama, Mwenyekiti wa Wabunge wa Afrika ya Mashariki, Abdalla Hasnuu Makame, alisema utekelezaji wa sheria hiyo bado haujakamilika kwa sababu unakabiliwa na mchakato mrefu.

Makame alivitaja vikwazo vinavyokwamisha mchakato huo ikiwamo sheria za ndani za fedha kwa kila nchi kwanza zinatakiwa kufanyiwa marekebisho ili ziweze kwenda sambamba na malengo ya sarafu moja.

Alisema mchakato wa sarafu moja ulitarajiwa kukamilika ifikapo mwaka 2024, lakini kutokana na kuwapo kwa vikwazo vingi vya sheria za ndani za kifedha kwa nchi wanachama utalazimika kuchelewa.

"Mchakato huo unahusisha mambo mengi ikiwamo sheria za ndani za fedha kwa kila nchi mwanachama ambapo zinatakiwa zirekebishwe kwanza kabla ya kuwa na sarafu ya pamoja," alisema.

Bunge la Afrika ya Mashariki lilikuwa na kikao cha wiki moja, ambapo visiwani Zanzibar lilipitisha bajeti ya Bunge hilo huku likizitaka nchi wanachama kulipa madeni yao kwa ajili ya kuendesha Bunge hilo kwa ufanisi.

Aidha, Bunge hilo liliwapongeza wanawake wa nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na kufuruhishwa na juhudi zao za kupambana na umaskini kwa kujikita zaidi katika kazi za ujasiriamali.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 11 March**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 12 March**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 13 March**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 14 March**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 15 March**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 16 March**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Ode To Joy
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Grindstone road
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 17 March**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Telenovela: Ode To Joy
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 11 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Kesho Leo
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 12 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum: Ewura
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 13 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Kesho Leo rpt
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 14 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Elininyo
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Elininyo
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Kipindi Maalum rpt: Ewura
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Riziki
09:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 15 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: Tanesco
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi rpt
13:45 Kesho leo rpt
13:55 Habari za saa
14:00 Kesho leo rpt
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Shamba shape up
19:00 Uchumi na biashara
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 16 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Elininyo
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 17 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Tafrija ya chakula cha mchana kwa watu wenye ulemavu
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Hard Price 2
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)







## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

**TUESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**WEDNESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**THURSDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**FRIDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**SATURDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

**SUNDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO

### CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
### FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

## China yasitisha matumizi ya Boeing 737 max 8

**BEIJING, China**

SERIKALI ya China imeagiza kampuni zote za ndege nchini humo kusitisha safari za ndege aina ya Boeing 737 Max 8 baada ya ajali ya ndege ya Ethiopia ambayo ni ya muundo sawa na hizo.

Taarifa iliyotolewa jana ilieleza kuwa "Kampuni za ndege ni lazima zisitishe usafiri wa abiria wa ndege zote za Boeing 737 Max 8 kufikia saa 18:00" Ilisema taarifa kutoka halmashauri ya usafiri wa ndege ya China.

Ajali ya Ethiopian Airlines ni ya pili ya ndege aina hiyo chapa 737 Max 8 katika muda wa miezi mitano iliyopita.

Taarifa kutoka halmashauri ya usafiri wa ndege China, ilisema huduma za ndege hiyo zitarejeshwa baada ya kuthibitisha hatua za kiusalama zimeimarishwa.

Mamlaka hiyo pia ilisema itashauriana na halmashauri ya safari za ndege nchini Marekani na wasimamizi wa Boeing.

Pia ilitaja ndege ya Indonesia ya Lion iliyoanguka muda mfupi baada ya kupaa kutoka mjini Jakarta Oktoba mwaka jana na kuwaua abiria wote 189.

China ni soko kubwa la kampuni ya kuunda ndege ya Marekani na ni moja ya mataifa iliyo na ndege nyingi aina ya Boeing 737 MAX-8.

Kampuni hiyo imeiuzia Shirika la Ndege la China ndege 76 aina ya Boeing 737 MAX, na tayari ilikuwa imeagiza ndege zingine 104, kwa mujibu wa data kutoka mtandao wa kampuni ya Boeing.

Boeing kwa ushirikiano na shirika la ndege la kibinafsi la China (Comac) inaendesha kituo cha kutengeneza muundo wa ndani wa ndege za 737 MAX katika mji wa mashariki wa Zhoushan.

Kampuni hiyo imewasilisha ndege za kwanza za MAX 8 kwa shirika la ndege la China Desemba mwaka jana.

*BBC*

# Ajali ndege ya Ethiopia: Kisanduku cha kunakili taarifa kimepatikana

**ADDIS ABAB, Ethiopia**

SIKU moja baada ya ndege aina ya Boeing 737 Max mali ya Shirika la Ndege la Ethiopia kudondoka na kusababisha vifo vya watu 157, kisanduku cha kurekodi safari ya ndege kinachojulikana kama 'Black box' kimepatikana eneo ambalo ajali ilitokea.

Hivyo, sababu ya ajali hiyo inaweza kufahamika baada ya uchunguzi kukamilika.

Ndege hiyo ilianguka juzi mjini Bishoftu Ethiopia umbali wa kilometa 60 kusini mashariki mwa mji mkuu Addis Ababa, dakika sita bada ya kuondoka katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Bole kuelekea nchini Kenya.

Taarifa iliyotolewa jana na Shirika hilo la ndege ilieleleza kuwa kisanduku hicho kiichwacho 'Black box' kimepatikana lakini kimeharibika kidogo.

Kifaa hicho ndicho kitakachotoa taarifa muhimu zitakazosaidia kupata picha halisi ya nini hasa kilichotokea kabla ya ndege hiyo kuanguka.

Nguo, Pasipoti, Kompyuta zapatikana

Siku ya jana zoezi la kuokoa miili kutoka eneo ambalo ndege ilipodondoka lilikuwa linaendeshwa na mafisa wa uchunguzi na vikosi vya uokoaji, ambapo mali binafsi za abiria waliofariki vimepatikana.

Kampuni iliyotengeneza ndege hiyo imeeleza kuwa itatuma wachunguzi wake kujumuika na kikosi kilichopo eneo la tukio kutafuta sababu kwa nini ndege hiyo ilianguka.

Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed ameahidi uchunguzi wa kina kuhusu ajali hiyo pamoja na kuweka wazi matokeo ya uchunguzi huo.

Siku ya maombolezo

Serikali ya Ethiopia jana ilitangaza siku moja ya maombolezo kuwakumbuka waliofariki katika ajali hiyo, sambamba na bendera kupepea nusu mlingoti.

Nayo nchi ya Kenya imetangaza siku moja ya maombolezo baada ya raia wake 32 kuwa miongoni mwa abiria waliofariki katika ajali hiyo.



Waokoaji wakiendelea na zoezi la kuokoa miili ya watu waliofariki katika ajali ya ndege ya Ethiopia jana. **PICHA : REUTERS**

Wafanyakazi wa tume ya uchumi katika Umoja wa Mataifa kwa bara la Afrika mjini Addis Ababa Ethiopia walikusanyika kuwakumbuka wafanyakazi waliofariki katika ajali hiyo.

UN waomboleza maafisa wake

Katibu mtendaji wa tume ya uchumi katika Umoja wa mataifa kwa bara la Afrika, Songwe Vera ameeleza kushtushwa kwa mkasa huo wa ndege uliosababisha vifo vya maafisa kadhaa wa mashirika ya Umoja huo wa mataifa.

"Tunawafikiria na kuziombea familia, marafiki wa karibu na wafanyakazi wenza wa waathiriwa wa mkasa wa ndege" alisema Vera.

Safari za ndege zasitishwa

Shirika la ndege la Ethiopia limetangaza kusitisha safari za ndege zake zote chapa Boeing 737 Max 8 kuanzia jana hadi taarifa zaidi itakapotolewa.

Limesema kwamba licha ya kuwa chanzo cha ajali hakijajulikana, wameamua kuchukua hatua hiyo kama tahadhari ya ziada.

Mojawapo wa watu waliofariki katika ajali hiyo ni Afisa wa itifaki wa Somalia. Shirika la Umoja wa mataifa linaloshughulikia elimu (Unesco) limeeleza masikitiko kwa kumpoteza mwanaharakati anayetetea uhuru wa vyombo vya habari na usalama wa waandishi kwa habari Kenya, Anthony Ngare.

Ndugu kusaidia utambuzi

Waziri wa Usafirishaji nchini Ethiopia, James Macharia alisema serikali itawasafirisha ndugu wa waliopoteza maisha kwenye ajali hiyo kuelekea Ethiopia ili waweze kusaidia kutambua miili.

Akizungumza na waandishi wa habari, macharia alisema familia 25 kati ya 32 tayari wamepatiwa taarifa na taratibu za kupata familia zilizobaki zinaendelea.

Macharia alisema zoezi la usafirishaji litafanywa kwa ushirikiano wa serikali ya Ethiopia na Kenya.

Shirika la ndege la Ethiopian lilitangaza kusafirisha miili kuelekea Kenya baada ya kumaliza shughuli za uthibitisho.

*BBC*

# Kagame afunguka chanzo mgogoro na Uganda

**KIGALI, Rwanda**

RAIS wa Rwanda, Paul Kagame amesema kuwa chimbuko la mgogoro baina ya nchi yake na nchi ya Uganda lilianza miaka 20 iliyopita, wakati nchi ya Uganda ikitaka kuangusha utawala wake.

Amesema mgogoro huo ulishika kasi miaka ya hivi karibuni kutokana na serikali ya Uganda kuunga mkono kundi la RNC linalopinga Rwanda, pia linatumiwa na Uganda kuwanyanyasa raia wa Rwanda wanaotembelea au wanaoishi nchini Uganda.

Akihutubia mkutano wa kitaifa unaomkutanisha na viongozi wengine kuanzia ngazi za chini, Rais Kagame alizungumza kwa undani mgogoro baina ya Rwanda na nchi ya Uganda na kusema mgogoro huo ni wa tangu miaka 20 iliyopita.

Akifafanua mgogoro huo, Rais Kagame alirejea kitabu kinachoitwa 'From Genocied to continental War" ambacho kiliandikwa na Gerard Prunier mwandishi wa vitabu kutoka Ufaransa.

Rais Kagame alisema kwamba mwandishi huyo aliandika kwamba alikutana na waziri wa zamani wa mambo ya ndani wa Rwanda, marehemu Seth Sendashonga mwaka 1998 pamoja na maafisa wakuu wa jeshi la Uganda na kuzungumzia mipango ya kumsaidia Sendashonga ili kuangusha utawala wa Kagame.

Mwandishi huyo katika kitabu hicho kulingana na maelezo ya Rais Kagame, Uganda ilikuwa imemuahidi kumsaidia kijeshi.

"Sababu ya mimi kurejelea kuzungumza haya nimetaka kuwaonyesha mfululizo wa jinsi mambo yalivyokwenda mnamo miaka 20 iliyopita. Tulijaribu kufanya mikutano ya hapa na pale ili kutafuta suluhu lakini matatizo hayo hayaishi, ukweli ni kwamba Seth Sendashonga alifariki dunia kwa kuwa alivuka mstari mwekundu, sifurahii kusema hivyo lakini pia sijutii kifo chake" alisema Rais Kagame.

Seth Sendashonga aliuawa katika mazingira ya kutatanisha mwaka 1998 mjini Nairobi alipokuwa uhamishoni baada ya kutofautiana na utawala wa Rwanda.

Rais Kagame alisema mgogoro huo ulishika kasi hivi karibuni baada ya wananchi wa Rwanda wanaoingia nchini Uganda ama kufanyia kazi kushikwa na kuzuiliwa sehemu ambazo hazijulikani na kufanyiwa vitendo vya mateso, huku akishtumu utawala wa Uganda kutoa nafasi ya ushirikiano kwa kundi la Rwanda National Congress linaloongozwa na mkuu wa zamani wa majeshi ya Rwanda Jenerali Kayumba Nyamwasa.

"RNC wanafanya kazi kwa ushirikiano na vyombo vya usalama vya Uganda, kilicho wazi ni kwamba wanachokifanya ni kunyanyasa wanyarwanda ambao hawataki kuungana nao huku wakiwasingizia kwamba wametumwa na utawala wa Kigali kuhujumu usalama wa Uganda na kuuwa wanyarwanda wa upinzani, ni madai yasiyo na msingi lakini haya yote yanaonyesha ushirikiano wa dhati uliyopo baina ya serikali ya Uganda na kundi la RNC" alisema Rais Kagame.

Uganda imekuwa ikiishutumu Rwanda kuwatuma majasusi na kufanyia vitendo vya ujasusi kwenye ardhi yake, tuhuma ambazo Rwanda inakanusha.

Rais Kagame alisema kwamba mara kadhaa amekuwa akiwasilisha malalamiko hayo kwa Rais mwezake wa Uganda, Yoweri Museveni na kwamba hakuonyesha utashi wowote wa kuyatatua.

Wiki iliyopita serikali ya Rwanda iliwakataza wananchi wake kwenda nchini Uganda na kusababisha mkwamo wa biashara.

Rwanda inasema inatoa kipaumbele kwa maisha ya raia wake zaidi kuliko biashara baina ya nchi mbili.

*BBC*

# Hospitali yajikomboa kwa kero sugu ya maji

**Na George Tarimo, MAFINGA**

HOSPITALI ya Wilaya ya Mufindi iliyoko katika mji wa Mafinga, imetatua kero ya maji baada ya kuchimba kisima ambacho kimewasaidia kupata maji ya uhakika.

Akizungumza mwishoni wa wiki, Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Victor Msafiri, alisema mradi huo umewasaidia kupunguza matumizi makubwa ya fedha kununua maji katika mamlaka ya maji ya mji wa Mafinga.

Msafiri alisema mradi huo umejengwa chini ya mradi wa maji wa Water for Africa na kuongeza awali hospitali ilikuwa ikinunua maji ya zaidi ya Sh. milioni moja kwa mwezi kwa ajili ya matumizi ya hospitali, ambapo kwa sasa fedha hizo zinatumika katika matumizi mengine.

Alisema kabla ya mradi huo, hospitali hiyo ilikuwa na matumizi ya lita 100,000 kwa siku sawa na uniti 21 ambazo zote zilikuwa zinalipiwa katika mamlaka ya maji.

Alisema maji katika mji wa Mafinga hayapatikani saa 24 kutokana na hitilafu ya umeme inayotokea mara kwa mara.

"Baada ya kuchimbwa hiki kisima mwaka jana fedha zilizokuwa zinatumika kulipia maji kwa sasa hatuzitumiki tena kununua maji na badala yake fedha hizo tunazipeleka katika matumizi mengine kama ununuzi wa dawa kwa ajili ya wagojwa wetu," alisema Dk. Msafiri

Alisema kisima hicho kimewasaidia kwa kiwango kikubwa katika kupunguza gharama za uendeshaji wa hospitali hiyo na kufanya baadhi ya huduma ambazo zilikuwa hazipatikani kwa muda wote.

Naye Meneja wa Shirika la Water for Africa Tanzania, Nestory Sanga, alisema shirika hilo kupitia Mbunge wa Jimbo la Mafinga Mjini, Cosato Chumi (CCM), liliona umuhimu wa hospitali kuwa na maji ya uhakika na kuamua kuchimba kisima hicho.

Sanga alisema shirika limekuwa likifanya kazi za kusaidia upatikanaji wa maji katika vijiji ambavyo vinamatatizo makubwa ya maji ikiwamo kuchimba visima virefu zaidi ya 24 kwa Wilaya ya Mufindi kwa mwaka 2018/19. Alisema kuwa shirika hilo pia limekuwa likisaidia katika masuala mengine ikiwamo afya, ambapo kwa mwaka wamekuwa wakileta madaktari kutoka Australia kwenda kutoa huduma vijijini.



Magari yakiwa kwenye foleni Mbezi Mwisho, Dar es Salaam jana. Barabara za eneo hilo kwa sasa zinafanyiwa matengenezo makubwa hali ambayo insababisha foleni za mara kwa mara. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Zitto awekwa mtegoni kutofika mahakamani

INATOKA UK 3

hospitalini kupata matibabu katika kituo cha afya Nguruka, polisi wakapata taarifa kuwa kuna watu wanne wamekwenda hospitali kituo cha afya Nguruka kupata matibabu wakawafuata kule wakawaua."

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa mshtakiwa alizidi kunukuliwa kuwa: "Lakini tumefuatilia kwa kina jambo hili, taarifa ambazo tumezipata kutoka kijijini Mpeta, Nguruka Uvinza ni mbaya. Ni taarifa ambazo zinaonyesha wananchi wengi sana wameuawa na Jeshi la Polisi, pamoja na kwamba Afande Sirro amekwenda kule, halijatoa taarifa yoyote kuhusu wananchi. Kama hawa Wanyantuzu walivamia eneo la ranchi, kuna taratibu za kisheria za kuchukua na si kuwaua, wananchi wengi sana wamekufa."

Ilidaiwa kuwa, Zitto aliendelea kuwahimiza wananchi kwa kusema: "Tumekuwa tukifuatilia kwa kina yanayojiri yote huko Uvinza tunasikitika kusema kuwa taarifa tunazozipata kutoka Uvinza zinaogofya mno kwa kuwa tunaambiwa kuwa wananchi zaidi ya 100 wa kabila la Wanyantuzu wamepoteza maisha kwa kupigwa risasi na polisi, wengine wakisemwa kuuawa hata wakiwa kwenye matibabu hospitalini baada ya kujeruhiwa kwenye purukushani na Jeshi la Polisi."

Wankyo alidai kuwa maneno hayo si tu yalichochea chuki bali pia yalitengeneza uhasama kwenye mamlaka halali na kusababisha mijadala miongoni mwa makundi mbalimbali katika jamii na kwenye mitandao na vyombo vya habari kwa ujumla.

Pia alidai kuwa maneno hayo yaliwafanya watu wafikirie kuwa serikali haiwajali raia wake.

Zitto aliposomewa mashtaka yake alikana na yuko nje kwa dhamana.

# Wanafunzi walia uhaba wa vyumba vya faragha

**Na Happy Severine, BARIADI**

WANAFUNZI wa kike katika wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu, wamelalamikia ukosefu wa chumba cha kubadilishia taulo za kike shuleni hususan wawapo katika siku za hedhi.

Wanafunzi hao waliyasema hao juzi wakati wa mazungumzo yao na waandishi wa habari, yaliyofanyika katika Shule ya Sekondari ya Bariadi, mjini hapa.

Hawa Hussen, mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari ya Kidinda, alisema anakerwa na changamoto ya kukosekana kwa chumba hicho hali inayowalazimu wengi wao kutohudhuria masomo pindi wawapo katika hedhi.

Alisema changamoto hiyo imewafanya mabinti wengi kushindwa kufuatilia masomo yao vizuri pindi wawapo hedhi kwa sababu ya kukosa vyumba maalumu vya kubadilishia taulo na kufikia uamuzi wa kutoroka shule ili kutafuta sehemu stahiki za kujisitiri.

Naye Judith Issa (12) mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Somanda B, alisema suala la vyumba maalumu vya faragha ni changamoto shuleni kwao kwa kuwa vyumba havipo na anatamani jambo hilo lipewe kipaumbele zaidi kwa kutazamwa zaidi kwa jicho la ziada.

Aliongeza kuwa mbali na uhaba wa chumba hicho, bado kuna tatizo kubwa la vyoo hali ambayo inawawia vigumu kuwa na sehemu walau ya kujisitiri.

Kutokana na changamoto hiyo, aliiomba serikali kwa kushirikiana na wazazi kuliangalia suala hilo kwa kuwa limekuwa kikwazo kikubwa katika maendeleo yao.

Naye Afisa Elimu, Afya na Mazingira wa Mkoa wa Simiyu, Juslin Gilbert, alisema kumekuwapo na jitihada kwa baadhi ya shule mkoani hapa kutenga asilimia ya fedha za ruzuku kutoka serikalini kwa ajili ya kuwahudumia wanafunzi wa kike.

Alisema shule zimeanza kutenga fedha kuwahudumia wanafunzi wa kike katika masuala ya hedhi salama kutokana na agizo la serikali linalowataka wafanye hivyo.

Hata hivyo, alisema mpaka sasa utekelezaji wa agizo hilo bado ni changamoto ingawa tayari mwongozo umekwishatolewa na ni lazima lifanyiwe kazi.

**Aliongeza kuwa mbali na uhaba wa chumba hicho, bado kuna tatizo kubwa la vyoo hali ambayo inawawia vigumu kuwa na sehemu walau ya kujisitiri.**

# MATANGAZO


# MATANGAZO MCHANGANYIKO

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311

## VYETI VIMEPOTEA



**ONG'HOLO MAGASEDI** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo; Kidato cha Nne chenye index namba s 115/0084 kilichotolewa na Baraza la Mitihani tanzania NACTE na Kahororo Secondary School mwaka 2010.

Na cheti cha Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira Arusha mwaka 2016 index namba **TUMA/BAED/13/1272.**

**YEYOTE ATAKAYEVIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI AU APIGE SIMU NAMBA 0744515473, 0759747273**

215109402

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika Mahakama ya Mwanzo: DODOMA MJINI
Usimamizi wa Mirathi No. 14/2019
Ombi la (1) MWANAHAMISI RAJABU (2) PETER NICHOLAUS kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu IDDY RAJABU DOMOGAZI

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 21/03/2019. kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

215109302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 11/03/2019.

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe 16/03/2019 kampuni ya **KUKU NZITO** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **SANYA JUU** kuelekea **MAILI SITA - MOSHI** gari hilo lenye namba za usajili:

   **T 724 BDR – TRAILER T 301 BEA**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu - mita 19.90
   Upana - mita 2.80
   Kimo - mita 4.40

3. Njia itakayotumika: **SANYA JUU** hadi **MAILI SITA** kupitia **ARUSHA ROAD.** Gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115109102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;58/2019

Ombi la **MERISIANA ANTHONY** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **ATHANAS SALEHE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 29/03/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/03/2019.

115108302

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKKI


**LUCY PAULO KESSY** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 112 BPV. Engine namba PFZWGJ91407.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **URP/RB/5278/18.**

115108402

---

## VYETI VIMEPOTEA




**EMELIA NJELENJE ANYIGULILE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0913-0011** kilichotolewa na USONGWE SEKONDARI mwaka 2010. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0330-0524** kilichotolewa na MBEYA SEKONDARI mwaka 2013.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **MBI/RB/306/2019.**

115107101

---

## CHETI KIMEPOTEA



**MASAM JOHN END** wa S.L.P. 200 Magu, Mwanza. Anatangaza kupotelewa na Cheti cha kuhitimu Elimu ya Mafunzo ya Misitu mwaka 2004 Chenye namba ya usajili **10285/T2001** kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA).

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kwenye kituo cha Polisi kilicho karibu.

Taarifa ya Polisi:
**MOR/RB/1968/2019.**

115107902

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**Domiana Gabriel** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0361-0505 kilichotolewa na Baraza la Taifa mwaka 2013 katika shule ya Singe Sekondari .

Yeyote atakaekiona atoe taarifa katika kituo chochote cha Polisi.
**Polisi Taarifa: BI/RB/1542/2018**

115107702

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**Abeid A. Kaduma** anatangaza kupotelewa na vyeti vya kidato cha nne vifuatavyo, Cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.3148/0034 kilichotolewa na Baraza la Taifa mwaka 2010 katika shule ya Makungu Sekondari, cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P1378/0488** kilichotolewa na Baraza la Taifa mwaka 2011 katika Shule ya Kleruu Teachers Center, Cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P.0443/0093** kilichotolewa na Baraza la taifa mwaka 2012 katika shule ya Sekondari Meta.


Yeyote atakaeiona atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi

Polisi Taarifa:
DOM/4072/2017

115107602

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**Nikola P. Maganga** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0693-0118 kilichotolewa na Baraza la Taifa mwaka 2013 katika shule ya Sekondari Manyara .

Yeyote atakaekiona atoe taarifa katika kituo chochote cha Polisi.
**Polisi Taarifa: KRT/RB/915/2019**

115107202

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;59/2019

Ombi la **MARIA HOSENI MGONELA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **LUCAS PETER MKEKA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 22/03/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 06/03/2019.

215108602

---

**IN THE DELIGATE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE ADMINISTRATION CAUSE NO 15 OF 2019**
**In the matter of the Estate of the late AGNES PAULO KAZINGOMA- DECEASED**
**AND**
**In the matter of the Application for letters of Administration by EDGER ANDERSON LUPANGA**

## GENERAL CITATION

All person claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named petitioners.

Objections to the grant should be filled on or before 27TH /03/2019.

The will if any of the said deceased is deposited and open for inspection of the court.

Dated….7TH /03/2019

115107302

---

## KUPOTELEWA KWA KADI YA PIKIPIKI

**FAIR DEAL AUTO PVT LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya PIKIPIKI aina BAJAJI yenye namba za usajili MC 263 ASK Chassis MD2A21B28FWA51202, Engine Namba PFZWFA35687.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOM/TR/RB/108/2019.**

115107502

---

**IN THE DELIGATE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE ADMINISTRATION CAUSE NO 08 OF 2019**
**In the matter of the Estate of the late SIMON MTOSHI**
**AND**
**In the matter of the Application for letters of Administration by JENIPHER JUSTIN**

## GENERAL CITATION

All person claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named petitioners.

Objections (if any) to the grant should be filled on or before 13th/03/2019.

The will if any of the said deceased is deposited and open for inspection of the court.

Dated….28TH /02/2019

115107402

---

Uza,
Chenye Thamani
Kubwa Kwa Kutangaza
Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0767 223 311

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku
Tupigie 0767 223 311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI MICHEZO

# KLOPP SASA AIONYA MANCHESTER CITY

**LIVERPOOL, Englad**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema amewaonya washindani wao kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu, Manchester City na kudai kwamba hakuna mtu anayeweza kuwazuia, baada ya kushuhudia timu yake ikiifunga Burnley mabao 4-2 juzi, Jumapili.

Liverpool ilitoka nyuma kwa bao la Ashley Westwood baada ya dakika sita, lakini mabao mawili kutoka kwa Sadio Mane na Roberto Firmino yaliwapa 'Wekundu' hao ushindi huo.

Matokeo hayo yanaifanya Liverpool sasa kupitwa pointi moja na Man City iliyopo kileleni, huku zikiwa zimebaki mechi nane kumalizika kwa ligi hiyo.

"Ujumbe wangu wa leo ni kwamba hakuna mtu anayeweza kutuzuia kama tukicheza kama ambavyo tumecheza leo (juzi), kwa sababu tulikuwa na wakati mgumu dhidi ya wapinzani wetu."

Akizungumza baada ya mchezo huo, Klopp aliwasifia wachezaji wake kwa kucheza kwa kujituma na kwamba, kama wakicheza katika kila mchezo kwa staili ile, watakuwa na nafasi kubwa zaidi ya kushinda kila mchezo.

"Ujumbe wa leo, hakuna wa kutuzuia," alisema kocha huyo raia wa Ujerumani.

"Tulikuwa na nafasi nzuri ya kucheza, na hakika kabisa kwamba tulikuwa kwenye wakati mzuri zaidi wa kucheza."






# SOLSKJAER: HATUNA NAFASI NNE BORA

**LONDON, England**

KOCHA wa muda wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amekubali kuwa ana mlima wa kupanda kuingia nne bora kwenye Ligi Kuu ya England, baada ya juzi kufungwa na Arsenal mabao 2-0.

Solskjaer amesema kuwa sasa ni wazi kwamba michezo iliyobaki ni migumu kwao kuweza kumaliza katika nne bora.

Baada ya kucheza michezo 12 bila kupoteza wakiwa chini ya Ole Gunnar, Man United imeshuka kwa nafasi moja hadi ya tano baada ya kupoteza mchezo wa kwanza kwenye ligi chini kocha huyo raia wa Norway.

Baada ya matokeo hayo, Solskjaer amekiri kwamba Man United wana mlima mrefu wa kupanda mpaka kuingia nne bora ya ligi hiyo.

Ole alisema: "Ni ngumu sana," alijibu, alipoulizwa na waandishi wa habari.

"Spurs walipotea, sisi tumepotea, na Chelsea imetufanya tutoke nje ya namba nne na ni ngumu kurudi.

"Tumejitoa katika vita hivyo, tuna pointi mbili nyuma ya timu iliyopo nafasi ya nne, na tatu kutoka timu iliyopo nafasi ya tatu ambayo ni nafasi nzuri ya kuwa ndani."

Ole aliongeza, "Tulitengeneza nafasi nyingi zaidi leo (juzi) kuliko wakati tulipowafunga kwenye Kombe la FA. Wakati mwingine hutokea, tumegongesha mwamba mara mbili na tulikuwa na fursa tano kubwa sana za kupata mabao.

"Tulipaswa tu kwenda mwisho, lakini hatukuwapo na ni mojawapo ya siku hizo ambapo unapaswa kujivunia.

"Mchezaji huyo atakuwa na tamaa wakati anajiona kama sifikiri ni adhabu, lakini huo ndiyo uamuzi aliyoufanya mwamuzi."

# United yamnyima usingizi Mbappe

**PARIS, Ufaransa**

NYOTA wa klabu ya Paris Saint Germain, Kylin Mbappe, amekiri kwamba, hakuweza kulala baada ya kufungwa na Manchester United kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Licha ya PSG kuwa mbele ya mabao 2-0 katika mchezo wa kwanza wa hatua ya mtoano ya 16-bora, Man United ilipindua matokeo na kuwafunga 3-1 kwao na kufuzu hatua ya robo fainali.

Katika mahojiano yake na Kituo cha Telefoot cha nchini Ufaransa mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, Mbappe alisema alishindwa kulala.

"Sikuweza kulala nilishindwa kabisa, kwa sababu ya kutolewa na Manchester United kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya," alisema Mbappe.

Aliongeza kusema: "Ulikuwa wakati mgumu zaidi kwenye maisha




yangu ya soka, maana ndoto yangu ilikuwa kucheza fainali ya Ligi ya Mabingwa msimu huu.

Akizungumza kwa mara ya kwanza tangu kutolewa kwenye michuano hiyo, Mbappe alisema: "Kwanza nilibaki nimeshangaa tu halafu nikaishiwa na maneno na baada ya hapo sikuweza kulala na nadhani imekuwa sawa kwa kila mtu mwingine ambaye yuko hapa PSG."

Mbappe alizidi kufunguka: "Uwanja ulijaa mashabiki wetu tu na mashabiki walifanya kazi yao ya kushangilia, kweli ilikuwa hali ya kimiujiza, tuliharibu sherehe yetu wenyewe.

"Kuna watu wengi sana ambao wanatutukana, lakini bado ninaamini timu yangu, nina uhakika tutafanya kitu kizuri kwa klabu yetu pia na msaada wa mashabiki wetu, natumaini kwamba wanaendelea kuwa nyuma yetu."

HABARI MICHEZO



# SARRI ATETEA MBINU ZAKE CHELSEA

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri kwa mara nyingine tena ametetea mbinu zake za kimchezo wakati timu yake ikitoka sare ya bao 1-1 na Wolverhampton Wanderers juzi Jumapili, akisisitiza kwamba Blues hao walijikuta kwenye wakati mgumu kutokana na staili ya ulinzi.

Sarri alisisitiza kwamba, Chelsea walistahili kushinda mchezo huo, lakini walishindwa kuweza kuipenya safu ya ulinzi ya Wolves.

Alinukuliwa na mtandao wa football london akisema: "Nafikiri tulifanya makosa mengi, lakini tulistahili ushindi.

"Mwanzo hali ilikuwa mbaya kwenye eneo letu la penalti, lakini pia hatukuwa na bahati, ila tunahitaji kujiimarisha hasa katika safu ya ushambuliaji, lakini kama timu inacheza kwa kujilinda inakuwa kwenye tatizo kubwa.

"Tulihitaji kucheza kwa kasi, kuna wakati tulikuwa hatuna mpira. Tulicheza kwa pasi fupi na kwetu ilikuwa vigumu kufunga. Na wapinzani wetu walikuwa imara zaidi na wenye nguvu."

Sarri aliendelea kuelezea sababu ya kumbadilisha Jorginho, huku akisema kwamba kutokana na kiungo huyo kushindwa kuzunguka kwenye dimba la kati.

"Tulibadili mfumo kwa mara ya kwanza na kuwa 4-2-3-1. Haikuwa kazi rahisi mfumo huu mpya ulikuwa mgumu zaidi kwetu, lakini kwa namna tulivyocheza ilikuwa ni tofauti.

"Ni vigumu kufunga mabao kama unacheza pasi fupi na huwezi kumiliki mpira kwa muda mrefu.

"Kwa mara ya kwanza tulikuwa tunacheza dhidi ya timu ambayo ilikuwa na staili tofauti ya uchezaji kushinda sisi."

## DE LIGT ASUBIRI OFA YA BARCA

**AMSTERDAM, Uholanzi**

BEKI wa Ajax, Matthijs de Ligt, atakataa ofa kutoka klabu yoyote ya Ulaya ili kusubiri ofa ya kujiunga na Barcelona.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, ni mmoja wa wachezaji wanaotajwa kuwa na kipaji cha hali ya juu Ulaya na alionyesha kiwango bora zaidi wakati wakiifunga Real Madrid mabao 4-1 kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

De Ligt amekuwa akitajwa kuwa anataka kuondoka hapo Ajax na anawaniwa na klabu za Juventus, Paris Saint-Germain, Bayern Munich na Atletico Madrid.

Gazeti la Mundo Deportivo limedai kwamba De Ligt mwenyewe anataka kwenda Barcelona na kwa sasa anasubiri ofa kutoka kwa miamba hao wa Catalunya.

Mapema wiki iliyopita, Rais wa Barcelona, Josep Maria Bartemou, alitamka hadharani kwamba klabu yake inafikiri kumsajili De Ligt wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Imedaiwa kwamba kuna uwezekano mkubwa wa De Ligt kupata nafasi ya kucheza kikosi cha kwanza hapo Barcelona, sambamba na Gerard Pique.



## SOLARI AKATAA KUFUNGUKA MAJALIWA YAKE MADRID



**MADRID, Hispania**

SANTIAGO Solari amebainisha kwamba bado yupo gizani kuhusu majaliwa yake ya baadaye hapo Real Madrid baada ya kuishuhudia timu yake ikiibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Real Valladolid Jumapili usiku.

Real ililazimika kutoka nyuma baada ya Anuar kufunga bao la ufunguzi, huku mabao kutoka kwa Raphael Varane, Karim Benzema na Luka Modric yakiipa pointi tatu.

Ushindi huo umekuwa mzuri kwa timu hiyo ambayo ilikuwa na wiki mbaya, lakini alipoulizwa kuhusu majaliwa yake kama ataendelea kubakia hapo Real, Solari alijibu kwamba hajui hatima yake.

"Siwezi kujibu hilo," alijibu akiwaambia waandishi wa habari.

"Kesho tuna mazoezi, hivyo kwa sasa hilo ndilo ambalo naliangalia, siwezi kuzungumzia lolote.

"Ilikuwa wiki ngumu kwa kila mmoja na bila shaka kwa kila mchezaji. Dakika 25 ndizo zilionyesha hali halisi.

"Wakati wote wa mchezo nilijua kwamba tutapitia hapo, na ndio ilionyesha kwamba tunacheza soka la kishindani."

Licha ya hali ya hewa ilivyo hivi sasa hapo kwenye dimba la Bernabeu, Solari pia alikuwa na furaha kuzungumzia kuhusu ushindi wa mchezo huo.

"Ulikuwa mchezo mgumu, baada ya wiki mambo yalikuwa tofauti," aliongeza. "Hivyo tulikuja kwenye uwanja mgumu dhidi ya hali ngumu."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BENZEMA ATAKA MOURINHO ASUBIRISHWE KUTUA MADRID

**MADRID, Hispania**

Mshambuliaji wa Real Madrid, Karim Benzema, amewataka wakosoaji wa klabu hiyo kukumbuka mafanikio yao ya hivi karibuni huku akikataa kukaribisha swali kuhusu Jose Mourinho kurudi Santiago Bernabeu, lakini akafunguka kuwa hakuna sababu ya ujio wa kocha mpya kwa sasa.

Benzema ameendelea kuonyesha uwezo binafsi kwa kucheka na nyavu mara mbili katika kipindi cha pili wakati wakishinda 4-1 dhidi ya Real Valladolid.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Jose Zorrilla, Madrid ilitokea nyuma na kushinda hivyo kupooza machungu baada ya kikosi hicho cha Santiago Solari kupoteza mechi mbili mfululizo nyumbani dhidi ya Barcelona na Ajax ambazo zilihitimisha matumaini yao ya kutwaa ubingwa wa msimu.

"Tulipoteza mechi muhimu dhidi ya Ajax na inaonekana kama hatujawahi kushinda chochote," Benzema alisema, akinukuliwa na Gazeti la Marca.

"Usisahau kwamba tumeshinda mengi miaka hii. Hiyo ni vigumu sana na muhimu sana."

Lakini kukosa kombe msimu huu kutoka kushinda taji la Ulaya mara nne katika kipindi cha miaka mitano hakuonekani kuwa swari kwa Solari, na baadhi ya taarifa zikidai kuwa nafasi yake inaweza kuzibwa na Mourinho mapema. "Natumai Solari yupo hapa hadi mwishoni mwa msimu, lakini hilo ni suala la klabu na sitaki kulijadili," Benzema alisema.

"Tupo na Solari. Kama kikosi hakipo na kocha wao, tusingeweza kucheza mechi kama tulivyofanya leo [juzi].

"Kwa nini mabadiliko sasa? Tunayo michezo 11 iliyobaki na tunatumai atabaki nasi."

Alipoulizwa kuhusu Mourinho kuwa kocha wa Madrid ajaye, mshambuliaji huyo mzoefu raia wa Ufaransa, alijibu: "Siwezi kukujibu, ninaye kocha sasa na ni suala la klabu.

"Kutolewa kwenye kinyang'anyiro cha Kombe la Mfalme ['Copa del Rey'], Ligi ya Mabingwa Ulaya na wakati huu ubingwa wa La Liga ukiwa hauwezekani, ni vigumu.

"Soka ni kama hivyo. Tunapaswa kuendelea na kusubiri kushinda mechi 11 tulizobakiza na kufurahia soka, kitu ambacho ndicho muhimu zaidi.

"Mara zote tunapaswa kushinda, tunayo timu kubwa na watu wanapaswa kuwa zaidi pamoja nasi kwa sababu, katika soka, kuna mabadiliko mengi."

Benzema aliongeza: "Simaanishi mashabiki pekee, waandishi wa habari pia. Wakati ninapozungumza kuhusu watu, ninazungumza kuhusu kila mmoja.

"Sijasema kuwa waandishi wa habari wanapaswa kuwa pamoja nasi, bali tunapaswa kukumbuka kwamba tumeshinda vitu vingi tofauti na hilo ndilo muhimu. Ni vigumu kila mwaka, wapinzani ni wagumu zaidi."

## KWA UFUPI

### MOURINHO KUMKIMBIZA RAMOS
BEKI Sergio Ramos, 32, atataka kuondoka Real Madrid majira haya ya joto kama klabu hiyo itamteua kocha wao wa zamani, Jose Mourinho kuinoa. ***(Mail)***

### GUARDIOLA AIKANA JUVE
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, ambaye amekuwa akihusishwa na kwenda kuinoa Juventus, amewaambia marafiki zake kuwa yupo wazi kuhusu kubaki hapo Uwanja Etihad kwa miaka mingine minne ijayo. ***(Telegraph)***

### RANIERI AITAKA ROMA
KOCHA wa zamani wa Fulham, Claudio Ranieri, amesema miamba ya Italia, Roma ni klabu pekee ambayo anaweza kukubali kuinoa muda. ***(Goal)***

### CHELSEA YAMTAKA KOCHA WOLVES
Chelsea imemuweka kocha wa Wolves, Nuno Espirito Santo, katika orodha yake ya makocha inaowawinda. ***(Star)***

### GUNDOGAN KUJIFUNGA CITY
PEP Guardiola ameondoa hofu kuhusu mustakabali wa baadaye wa kiungo Ilkay Gundogan, 28, na kufunguka kuwa Mjerumani huyo atasaini mkataba mpya na Manchester Cit. ***(Mirror)***

### ISCO AVUTA VIGOGO EPL
KLABU za Ligi Kuu England zikiwamo Arsenal, Manchester United na Tottenham, zimeongeza nia yao ya kumsajili kiungo wa Real Madrid na Hispania, Isco, 26, baada ya uhusiano wake na kocha Santiago Solari kuanza kuwa mdogo. ***(Football.London)***

### OZIL KUMPISHA FORNALS
Tottenham na Arsenal zinaweza kuingia katika mbio moja ya kuiwania saini ya kiungo wa Villarreal, Pablo Fornals, 23. Hata hivyo 'Gunners' itapaswa kumuuza kwanza kiungo wao Mjerumani Mesut Ozil kabla ya kuanza safari hiyo. ***(Express)***

### MBAPPE AITOLEA NJE REAL
MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain na Ufaransa, Kylian Mbappe, 20, anayehusishwa na kujiunga na Real Madrid, amezikana tetesi hizo za kuachana na mabingwa hao wa Ligue 1 majira haya ya joto. ***(Squawka)***

### CITY, JUVE, SPURS VITANI
Manchester City inamfuatilia kiungo wa Lyon, Tanguy Ndombele, lengo likiwa ni kumnasa katika usajili wa majira ya joto nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22, ambaye amekuwa pia akitolewa jicho na Tottenham, Manchester United na Juventus. ***(Express)***

### ERIKSEN KUMPIKU CELSO SPURS
Tottenham inaweza kumfuata kiungo wa Argentina, Giovani lo Celso, ambaye ametupia mabao 12 wakati akiichezea Real Betis kwa mkopo akitokea Paris St-Germain msimu huu, endapo tu nyota wa kimataifa wa Denmark, Christian Eriksen, 27, atatimkia Real Madrid. ***(Talksport)***

### WEST BROM YAMGEUKIA JOKANOVIC
West Brom jana ilitarajiwa kuwa na mazungumzo zaidi na kocha wa zamani wa Fulham, Slavisa Jokanovic wakati huu klabu hiyo ya Championship ikisaka kocha mpya kufuatia kumtimua Darren Moore. ***(Telegraph)***

### MATONDO AFUNGUKA SCHALKE
WINGA wa zamani wa Manchester City, Rabbia Matondo, 18, amesema amejiunga na Schalke katika dirisha la Januari kwa sababu kunamuongezea nafasi ya kuitwa kuitumikia timu yake ya Taifa ya Wales. ***(Manchester Evening News)***

HABARI MICHEZO

# NINJA, TINOCCO 'WAENDA JELA' MECHI TATU BARA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Nidhamu ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), imemfungia rasmi beki wa Yanga, Abdallah Shaibu 'Ninja' kucheza mechi tatu za Ligi Kuu Bara, baada ya kubainika kumpiga kiwiko mchezaji wa Coastal Union katika mechi iliyozikutanisha timu hizo.

Licha ya kufanya kosa hilo tangu Februari 3, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga, Ninja aliendelea kuitumikia timu yake ikiwamo mchezo dhidi ya watani zao, Simba baada ya kuandika barua ya kutoa udhuru wa kushindwa kuhudhuria katika wito wa kwanza.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Boniface Wambura, alisema Ninja alikiri kufanya kosa hilo katika kikao cha Kamati ya Nidhamu na hivyo kuchukua uamuzi huo wa kumfungia.

Wambura alisema licha ya Ninja kujitetea kuwa alikuwa anajaribu kumzuia asipite kupiga pasi, kamati hiyo ilipitia ushahidi na utetezi na kamati imemtia hatiani.

Alisema pia kamati hiyo imemfungia golikipa wa Mtibwa Sugar, Benedict Tinocco mechi tatu kwa kosa la kumkanyaga kwa makusudi mchezaji wa Biashara United ambaye alianguka baada ya kufanyiwa faulo.

Pia kamati hiyo imemfungia kucheza mechi tatu mfululizo mchezaji wa Alliance FC, Juma Nyangi, baada ya kumfanyia kitendo cha udhalilishaji beki wa Yanga, Gadiel Michael, wakati timu hizo zilipokutana katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliochezwa Machi 2, mwaka huu.

"Mchezaji huyu alikiri na kuomba msamaha kwa kosa hilo na mbali na kumfungia, pia kamati imempiga faini ya Sh. milioni mbili na adhabu hizo zote zinakwenda kwa pamoja," alisema Wambura.

Aidha, Yanga nayo imepigwa faini ya Sh. milioni sita kutokana na kuingia uwanjani kwa kupitia mlango usio rasmi, kutoingia katika vyumba vya kubadilishia nguo na kutopita njia isiyo rasmi katika mechi ya watani wa jadi, wakati Simba nayo ikitozwa faini ya Sh. milioni tatu kutokana na kuingia uwanjani wakitumia mlango usio rasmi na kutotumia njia maalum kuelekea eneo la kuchezea.

Kadhalika, Klabu ya Azam nayo imepigwa faini ya Sh. milioni tatu kwa kutotumia mlango usio rasmi katika mechi yake dhidi ya Simba, wakati aliyekuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Hans van der Pluijm na wachezaji Ramadhani Singano na Stephen Kingue watapelekwa katika Kamati ya Nidhamu kwa kosa la kuwazonga waamuzi baada ya filimbi ya mwisho.




Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, Profesa Dadivis Mwamfupe (katikati aliyevaa kofia baada ya mtoto), akiwa na timu ya Capital City Marathon mara baada ya kuwavisha nishani ikiwa ni ishara ya kuwapongeza kwa kuendeleza michezo na kuuwakilisha mkoa kwenye mbio za Kili Marathon 2019 zilizofanyika mkoani Kilimanjaro hivi karibuni. **PICHA NA IBRAHIM JOSEPH**

# Coke Studio Africa yaigusa Siku ya Wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

ILI kuadhimisha na kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani, Coke Studio Africa 2019, imetangaza kuwa kwenye kipengele chake muhimu katika fainali za msimu huu, itahusisha wanawake tu kwenye taarifa yake muhimu na hoja ya kijasiri, imeelezwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari nchini, ilieleza kuwa hii itakuwa ni mara ya kwanza katika historia ya muziki wa Kiafrika kushirikisha wasanii wa kike wote katika kipengele hicho ambacho kitawajumuisha waimbaji, marapa, waandaaji wa muziki, wahandisi wa studio, bendi kamili wakiwamo wanaokaa nyuma ya kamera kama wakurugenzi wa maudhui, watungaji wa nyimbo, wahariri, waongozaji wa kamera, mameneja waongozaji na wengine wengi.

Kwa misimu sita ya Coke Studio Africa, shoo hiyo imeendelea kuainisha vipaji mbalimbali Afrika na fursa kwa wanawake katika sanaa na burudani kupitia tasnia ya muziki, ambapo kwa sasa asilimia 60 ya wanataaluma mbalimbali wanaofanya kazi Coke Studio Africa inawajumuisha wanawake.

"Coke Studio Africa itaendelea kutoa nafasi na fursa za ushindani kwa wanawake waliopo katika sanaa na muziki kupitia jukwaa hili," ilieleza sehemu ya taarifa hiyo.

Aidha, ilieleza kuwa miongoni mwa wanawake nyota kutoka Kenya ambao watakuwa sehemu ya 'Coke Studio Africa All Women Band' katika kipengele cha fainali yupo Kasiva Mutua (Percussions), Wendy Kemunto (Vocals), Ivy Alexander (Guitar), Naomi Ziro (Bass Guitar) na Mutindi Tindi Muasa (Keyboard).

Kwa upande wa wasanii nyota wa kike kutoka pande mbalimbali za barani humu ni pamoja na Nazizi (Kenya), Lioness (Namibia), Boity (Afrika Kusini), Sheebah (Uganda), Nandy (Tanzania), Mahlet (Ethiopia), Lourena Nhate (Msumbiji), Tamy (Zimbabwe) na muandaaji wa muziki Viola Karuri (Kenya), hao wakiwa ni baadhi tu.

Mkuu wa Ubora wa Maudhui na Kitengo cha Biashara wa Coca-Cola Kusini na Mashariki ya Afrika, Monali Shah, alisema: "Tunafarijika sana kutangaza wanawake wote katika fainali ya kipengele hiki kwa msimu wa Coke Studio Africa 2019.

"Hii ni mara ya kwanza kwa utawala kufanya uamuzi huu wa kijasiri katika historia ya Coke Studio Africa kwa kuwa imetukutanisha na vipaji vya kipekee sana katika kutoa burudani.

"Aina ya vipaji na wasanii tuliokutana nao na kugundua mchakato ni mzuri na wamejipanga vilivyo, inatuwia vigumu kusubiri hadi kusanyiko kubwa la mashabiki wa muziki wakati wa shoo kwa ajili ya kuja kutazama kipengele hiki cha nguvu kitakachorushwa katika mataifa 40 kuanzia Machi 29, mwaka huu."

Kuhusu Coke Studio Africa, ni show isiyokuwa ya ushindani wa ushirikiano wa muziki, ambayo inaleta pamoja na kusherehekea vipaji na tofauti ya muziki wa Afrika. Pia inawapa wasanii chipukizi fursa ya kufanya kazi na baadhi ya wasanii wa ndani na kimataifa. Wasanii hutolewa kutoka kwenye maudhui mbalimbali na maeneo tofauti na kuwaweka pamoja kutengeneza sauti ya kisasa na ya kweli ya Afrika kupitia mseto wa muziki.

Aidha, ikiwa wasanii wanakaa pamoja na kufanya muziki ulioandaliwa na wazalishaji wa onyesho, pia hujifunza muziki wa kila mmoja na mtindo wakibadilishana utamaduni. Onyesho huwachukua watazamaji ndani ya studio kuangalia aina mbalimbali za wasanii.

## Simbu, Sulle wafuzu Olimpiki Japan

**Na Renatha Msungu**

WANARIADHA wa Tanzania, Alphonce Simbu na Agustino Sulle wamekuwa wa kwanza kufuzu michezo ya Olimpiki itakayofanyika jijini Tokyo, Japan mwakani.

Wanariadha hao wamefanikiwa kukata tiketi hiyo jana nchini Japan, baada ya kukimbia muda mzuri katika mbio za Lake Biwa Marathon, ambazo zinatambulika na zimepitishwa na Shirikisho la Riadha la Kimataifa (IAAF).

Katika mbio hizo zilizokuwa na ushindani wa hali ya juu kutokana na kujumuisha washiriki kutoka nchi mbalimbali, Simbu wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), na mshindi wa medali ya Shaba ya Dunia, alikamata nafasi ya sita akiandika rekodi yake mpya, akitumia Saa 2:08.27.

Rekodi ya awali ya Simbu kabla ya jana ilikuwa ni Saa 2:09.10 aliyoiweka London Marathon.

Kwa upande wake, Sulle wa Klabu ya Taleny ya jijini Arusha, ambaye anashikilia rekodi ya Taifa Marathon ya Saa 2:07.45 aliyoiweka Toronto Marathon Canada mwaka jana, alishika nafasi ya 17 akitumia Saa 2:12.42.

Muda wa kufuzu kwa Olimpiki ambao unaanza kutambuliwa kuanzia Januari mwaka huu ni Saa 2:14. kwa wanaume Marathon.

Katika mbio za jana Lake Biwa, Tanzania iliwakilishwa na wanariadha watatu mwingine akiwa Gabriel Geay, ambaye alikwenda maalumu kama 'Pace Maker'.

Katika mbio hizo, mshindi wa kwanza alikuwa ni Salah Eddine-Bounasr wa Morocco aliyetumia Saa 2:07.52 akifuatiwa na Asefa Tefera wa Ethiopia 2:07.56, huku nafasi ya tatu ikienda kwa Stephen Mokoka wa Afrika Kusini 2:07.58.

Katibu Mkuu wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), Wilhelm Gidabuday, amewapongeza wanariadha hao na walimu wao kwa mafanikio hayo na kwamba yamekuja wakati mwafaka.

Gidabuday alisema RT chini ya Rais wake Anthony Mtaka na Kamati nzima ya Utendaji, hivi sasa wako kwenye mikakati ya kuhakikisha mwaka huu 2019, unakuwa ni wa kazi kutokana na kukabiliwa na matukio matatu makubwa kimataifa kabla ya Olimpiki 2020.

Katibu huyo, aliongeza kuwa ni matarajio yao vijana wengi zaidi watazidi kufuzu kwa mashindano mbalimbali ya kimataifa ikiwamo ya Dunia Doha Qatar na Olimpiki Tokyo 2020.

## MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.Yanga SC | 27 | 21 | 4 | 2 | 45 | 18 | 67 |
| 2.Azam FC | 27 | 16 | 8 | 3 | 42 | 18 | 56 |
| 3.Simba SC | 20 | 16 | 3 | 1 | 43 | 7 | 51 |
| 4.Kinondoni MC | 29 | 9 | 14 | 6 | 32 | 20 | 41 |
| 5.Lipuli FC | 30 | 9 | 12 | 9 | 24 | 26 | 39 |
| 6.Mtibwa Sugar | 27 | 11 | 5 | 11 | 28 | 21 | 38 |
| 7.Coastal Union | 29 | 8 | 13 | 8 | 27 | 30 | 37 |
| 8.Mbao FC | 29 | 9 | 10 | 10 | 19 | 26 | 37 |
| 9.JKT Tanzania | 30 | 8 | 12 | 10 | 18 | 24 | 36 |
| 10.Alliance | 29 | 9 | 9 | 11 | 23 | 30 | 36 |
| 11.Mbeya City | 27 | 9 | 7 | 11 | 27 | 29 | 34 |
| 12.Ruvu Shooting | 29 | 8 | 10 | 11 | 27 | 35 | 34 |
| 13.Mwadui | 29 | 9 | 6 | 14 | 31 | 36 | 33 |
| 14.Kagera Sugar | 28 | 7 | 12 | 9 | 21 | 26 | 33 |
| 15.Ndanda | 27 | 8 | 9 | 10 | 17 | 27 | 33 |
| 16.Stand Utd | 30 | 9 | 6 | 15 | 27 | 39 | 33 |
| 17.TZ Prisons | 28 | 7 | 11 | 10 | 20 | 24 | 32 |
| 18.Singida Utd | 27 | 8 | 8 | 11 | 20 | 26 | 32 |
| 19.Biashara Utd | 27 | 5 | 9 | 13 | 18 | 29 | 24 |
| 20.African Lyon | 29 | 4 | 10 | 15 | 18 | 36 | 22 |

Michezo
Jumanne Machi 12, 2019
Nipashe

Benzema ataka Mourinho asubirishwe kutua Madrid



HABARI UK. 30

BINJUKA...



Mshambuliaji wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang, akijaribu kufunga kwa kubinjuka, lakini mpira ukatoka nje ya lango la David de Gea, kwenye mechi hiyo ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Emirates juzi na Manchester United kukubali kipigo cha mabao 2-0. **HABARI UK. 28**

# SIMBA WASIKIENI KAGERE, MANULA

## ●●● Wafunguka vikali, AS Vita washtuka sasa kutua kesho, kuziona Jumamosi buku tatu huku...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI wapinzani wa Simba, AS Vita kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) wakitarajia kutua jijini Dar es Salaam kesho mchana, wachezaji wa kikosi cha 'Wekundu wa Msimbazi' wameendelea kusisitiza kuwa ushindi katika mchezo wao huo wa mwisho ni lazima.

Simba itawakaribisha AS Vita kutoka Kinshasa Jumamosi kwenye Uwanja wa Taifa kuanzia saa 1:00 usiku.

Akizungumza na gazeti hili jana, mshambuliaji, Meddie Kagere, alisema kufungwa ni sehemu ya mchezo na sasa wanajipanga kuhakikisha wanashinda mechi yao inayofuata na kutimiza ndoto za kucheza hatua ya robo fainali.

Kagere alisema bado hawajakata tamaa ya kusonga mbele kwa sababu wanaamini mbali na ubora waliokuwa nao, wanaamini hawawezi kuwaangusha mashabiki wao kwenye uwanja wa nyumbani.

"Kufungwa ni sehemu ya mchezo, tumekubali na sasa tunajipanga kurekebisha makosa yetu, tunaamini tutawasimamisha wapinzani wetu katika mchezo unaofuata, tuna kila sababu ya kufanya hivyo, asante Mungu," alisema Kagere.

Naye kipa chaguo la kwanza la timu hiyo, Aishi Manula, aliliambia gazeti hili kuwa wanajipanga kupambana ili kuweka historia katika kizazi chao.

"Tunaamini nafasi bado ipo, tutajipanga ili kusaka ushindi, kwa sababu tunahitaji kuweka historia na rekodi, hili ndilo muhimu kwetu kwa sasa," alisema kipa huyo ambaye alitua Simba akitokea Azam FC.

Wakati huo huo, Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema kikosi chao kitatua nchini leo mchana na kitakwenda moja kwa moja kambini kuendelea na mazoezi kwa ajili ya kuwavaa AS Vita.

"Tutafika huko kesho (leo) saa 9 mchana, hapa saa 4 usiku tutaelekea Dubai tukitokea Algiers," alisema kwa kifupi meneja huyo.

Taarifa kutoka Kinshasa zimeeleza kuwa kikosi chao kitatua nchini kesho na lengo la kuja mapema ni kuanza kufanya mazoezi jioni kwenye uwanja ambao watakuwa wameandaliwa na wenyeji wao.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Haji Manara, alisema kuwa kiingilio cha chini katika mechi hiyo ya Jumamosi kitakuwa ni Sh. 3,000 na cha juu kwa tiketi maalum zinazojulikana kwa jina la Platinumz zitauzwa Sh. 100,000.

# Zahera aanika ufundi Yanga

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Yanga, Mwinyi Zahera, amesema sababu kubwa iliyochangia timu yake kupata ushindi kwenye mchezo wa juzi dhidi ya KMC ni kutokana na wachezaji kutimiza vema majukumu yao kwa kufuata maelekezo aliyowapa.

Akizungumza na Nipashe jana, Zahera alisema katika kile alichowaelekeza wachezaji wake kwa asilimia 70 walikifanikisha na kuweza kupata ushindi huo wa mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Katika mchezo huo mabao ya Yanga yalifungwa na kiungo Papy Tshishimbi na lingine la kujifunga la Ally Ally.

Akizungumza na gazeti hili jana, Zahera, alisema kiufundi aliitazama KMC na kufahamu aina ya mpira wanaocheza, hivyo alijipanga vema kuwadhibiti.

"KMC ina wachezaji vijana wengi na wana kasi, aina yao ya mchezo ni kuanzisha mashambulizi kuanzia nyuma... wanapasiana sana kuanzia nyuma wanakuja mbele, mimi niliwasoma na niliwaambia wachezaji wangu wawaache wachezee mpira wakiwa langoni kwao, lakini wakishafika mstari wa kati tuhakikishe kila mchezaji wao anakabwa na ndicho kitu wachezaji wangu wamefanya na tumefanikiwa," alisema Zahera.

Alisema kuwa pamoja na ushindi huo, bado tatizo la waamuzi limekuwa kikwazo katika mechi mbalimbali.

Alisema kuwa mchezo wa juzi walistahili kupewa penalti, lakini mwamuzi aliminya na kukiuka sheria 17 za soka.

"Ni tatizo..., unajua hata ukiangalia mpira wa nje kama kuna mchezaji kafanya makosa awe amemchezea mpinzani wake vibaya au kuunawa ndani ya eneo la hatari inatakiwa itolewe penalti bila kuangalia lolote, hata kama timu inastahili kupata penalti zaidi ya moja refa anapaswa kutoa," alisema.

Alisema mchezo huo umepita na wanashukuru kupata pointi tatu muhimu na kwa sasa wanaangalia mbele mchezo unaofuata.

Ushindi huo wa juzi umeifanya Yanga kufikisha pointi 67 ikizidi kusalia kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >